

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10. Mhe. Abubakar Khamis Bakary MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13. Mhe. Juma Duni Haji MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14. Mhe. Zainab Omar Mohammed MBM/Waziri wa Uwezesaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15. Mhe. Abdillah Jihad Hassan MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16. Mhe. Ali Juma Shamuhuna MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17. Mhe. Suleiman Othman Nyanga MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe.
18. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19. Mhe. Said Ali Mbarouk MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20. Mhe. Haroun Ali Suleiman MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi

	Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake

44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 19 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati zako za Baraza la Wawakilishi naomba kuwasilisha mezani ripoti mbili, Ripoti ya Kamati ya Wenyeviti ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/2015, lakini pia, kwa ruhusa yako naomba kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati zako za Baraza uniruhusu kwa mara nyengine tena kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Wenyeviti ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuhusu Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla swali langu Nam. 46 kujibiwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Muyuni kwa umakini wake na umahiri wake katika kuiuliza serikali maswali hapa Barazani. Nadhani ukiachia yeye na mimi humu Barazani ni watu wawili ambao tunaongoza katika hilo. Kwa hiyo, nashukuru sana. Baada ya hilo, naomba swali langu Nam. 46 lipate jibu.

Nam. 46

Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Bunge Maalum la Katiba kukebehi Katiba ya Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika kutekeleza kazi zake tumekula kiapo cha kulinda, kuitunza pamoja na kuitetea Katiba yetu ya Zanzibar. Kwa kuwa kuna baadhi ya Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi la Zanzibar ambao pia ni Wajumbe wa Bunge la Katiba wamethubutu kukebehi Katiba ya Zanzibar kwa kulinganisha na Katiba ya Timu za Mpira, sambamba na kulinganisha na Bendera za Simba na Yanga pamoja na ile ya Uamsho.

Je, sheria za Zanzibar zinasemaje kwa Waheshimiwa wanaokwenda kinyume na kiapo walichoapa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Sheria ya Baraza la Wawakilishi ya Kinga, Mamlaka na Fursa Nam. 4 ya mwaka 2007 kifungu cha 3 na cha 4 kimeweka kinga kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa na uhuru wa kuzungumza na kujadili wakiwa ndani ya Vikao vya Baraza na uhuru huo hautohojiwa na Mahakama yoyote au taasisi yoyote nje ya Baraza.

Aidha, sheria hiyo imetoa kinga ya mashtaka kwa Mjumbe yeyote wa Baraza hili kuweza kuzungumza ndani ya Baraza maelezo yake yote aliyosema na hatofunguliwa mashtaka ya madai au jinai endapo amekwenda kinyume na utaratibu au Kanuni, lakini utaratibu wa kikanuni ndio unavyotumika pale panapotokea kufanya makosa.

Mhe. Spika, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya sura 83 kifungu cha 27 (2) imetoa kinga ya kuwa na uhuru wa mawazo na majadiliano kwa Wajumbe wote wa Bunge Maalum la Katiba. Hivyo, inapotokea kuwa Mjumbe kwenda kinyume na Kanuni zilizowekwa, basi ni utaratibu wa Kanuni ndio unaotumika ndani ya Bunge Maalum. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kutumia fursa hiyo pale inapotokea kama Mjumbe ametenda kosa au amesema maneno yasiyostahiki kwa mujibu wa Sheria au Kanuni ziliopo. Kwani Mabunge yote duniani yanaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni zake na si vyenginevyo. Hivyo, si vyema kulalamika nje ya Bunge pale yanapotokea makosa ndani ya Bunge.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kanuni hizi hizi Mhe. Spika, zinasisitiza lugha ya staha katika vyombo hivi na kwa kuwa lugha zinazotumika sio tu kama zinakebehi nchi hii ya Zanzibar ambayo kuna watu wanaitetea kwamba haikupatikana kwa vikaratasi badala yake ikapatikana kwa mtutu wa bunduki. Leo mtu huyo huyo kuja akatoa lugha chafu dhidi ya SMZ na viongozi wake baadhi, narudia na baadhi ya viongozi wake wakuu. Je, tuseme watu hawa wana akili timamu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni utaratibu wetu kuwa na lugha ya staha, kuwa na lugha za heshima kwa viongozi wetu ndio utaratibu tuliojiwekea katika Mabaraza yetu na hata katika Bunge Maalum la Katiba. Kama nilivyosema kwenye swali la msingi pale inapotokea mmoja wetu akavunja utaratibu huo, basi inapaswa yeyote yule anayemuona mtu amevunja utaratibu anapaswa kunyanyuka na kueleza fulani amevunja utaratibu. Ukiona hakuna aliyenyanyuka akasema amevunja utaratibu maana yake maelezo yaliyotolewa wakati huo yalikuwa hayakwenda kinyume na utaratibu wa Kanuni. Ama waliokuwemo ndani ya Baraza hili au Bunge hilo wote walipitikiwa.

Mimi Mhe. Spika, wakati wote nikisikia hapa utaratibu umevunjwa na kama naelewa Kanuni imevunjwa nanyanyuka nasema na baadhi ya Wajumbe wanafanya hivyo na ukiona hakutokea mtu kusema maana yake kuna uwezekano wa kuwa haukuvunjwa utaratibu, lakini kila mmoja hapa ndani anajua nchi yetu Zanzibar ina haki zake na utaratibu wake.

Nam. 57

Udhibiti wa Mabadiliko ya Tabia Nchi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Mabadiliko ya tabia nchi mbali na kuleta athari za kimazingira kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakileta athari za kiuchumi katika nyanja mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo na uvuvi.

- (a) Ni kwa kiasi gani serikali imepanua Bajeti ya Idara ya Mazingira katika suala zima la kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.
- (b) Ni kwa kiasi gani serikali imeanzisha na kuboresha mitaala ya mazingira kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu vyetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais -Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi, napenda kukubaliana naye kuwa mabadiliko ya tabia ya nchi ni tatizo kubwa linaloikabili dunia hivi sasa. Nchi za Visiwa kama Zanzibar ni maeneo ambayo yapo hatarini zaidi kuathiriwa na athari za mabadiliko hayo. Sekta mbali mbali za kiuchumi, kijamii na kimazingira zimekuwa zikiathirika kwa kiasi kikubwa. Mabadiliko ya tabia nchi yamekuwa na tishio kwa maendeleo endelevu ya dunia na kikwazo kikubwa cha kufikia malengo ya Milenia yaliyowekwa (*MDGs*). Chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabia nchi ni kuongezeka kwa gesi ya ukaa (au gesi joto - yaani *green house gases*) kwenye usawa wa dunia.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na kwa lugha ambayo inaruhusiwa na Kanuni zetu, naomba sasa kwa ruhusa yako kujibu swali Nam. 57 la Mhe. Mwakilishi lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kutambua kuwa suala la mabadiliko ya tabia nchi ni suala kubwa linalohitaji fedha nyingi kulishughulikia, serikali iliandaa mradi na kuhamasisha rasilimali fedha za kuweza kutekeleza mradi huo. Mwaka 2012 serikali ilitiliana saina na Shirika la *UNDP* kupitia programu ya *UNDP* kwa ajili ya kuendesha mradi wa miaka minne wa mabadiliko ya tabia nchi. Lengo kuu la mradi huu ni kujenga uwezo wa kuhimili na kusimamia mabadiliko ya tabia nchi hapa Zanzibar. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita jumla ya shilingi 1,316,752,700.0 zimeshatumika kwa shughuli mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kupitia taasisi sita zinazohusika katika kutekeleza mradi huu. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2014/2015 shilingi 577,500,000/= zinategemewa kutumika kwa ajili ya kazi za mradi huo.

Sambamba na fedha hizo, serikali kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 imeweza kutenga fedha kiasi cha shilingi 400,000,000/= kwa ajili ya programu maalum ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Fedha hizo zitapatikana kupitia programu ya kuendeleza Utalii Zanzibar na zitalenga zaidi katika kuendeleza ustawi wa matumbawe ambayo yamekuwa yakiathiriwa na kupanda kwa joto la bahari na hatimaye kufa hali ambayo imekuwa ikileta usumbufu kwa wavuvi wetu kwa kukosa maeneo ya kuaminika ya uvuvi pamoja na kupunguza haiba kwa watalii wetu wanaopenda kuogelea na kuzamia kwa ajili ya kuangalia matumbawe.

Mhe. Spika, Serikali inaelewa fika kuwa kiasi hicho cha fedha ni kidogo mno kukidhi angalau sehemu ndogo ya mfano (*pilot area*). Hata hivyo, imeamua kuanza kwa uwezo wake mdogo na kuendelea kufanya hivyo kadiri hali itakavyoruhusu. Kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha za mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Spika, Serikali imeanza utaratibu wa kuanzishwa Mfuko wa Fedha za Mabadiliko ya Tabia Nchi. Uanzishwaji wa Mfuko huo unaratibiwa na Wizara ya Fedha na fedha za mfuko huo zitatumika kwa ajili ya kutekeleza programu za kujihami na kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa kufuata vipaumbele vya maeneo yaliyotajwa kwenye Mkakati wa Zanzibar wa mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, mwaka jana serikali ilikamilisha mradi wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi wa maji safi na salama katika Shehia ya Nungwi ambao uligharimu zaidi ya shilingi milioni mia tano.

Sambamba na hayo, siku za hivi karibuni serikali kupitia vyanzo mbali mbali vya fedha ikiwa ni pamoja na mfuko wa *TASAF* imewezesha kujengwa matuta kwa baadhi ya maeneo ya kilimo yanayoingia maji ya chumvi yenye wastani wa jumla ya mita 1,840 katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Matuta hayoyamejengwa ili kupunguza athari za kupanda kwa kina cha bahari na kuwawezesha wananchi wa maeneo husika kuendelea na shughuli za kilimo.

(b) Serikali imekuwa ikiendeleza jitihada mbalimbali za kuhakikisha kuwa mitaala ya skuli za msingi hadi vyuo vikuu inahusisha masuala ya mazingira. Kwa kuanzia serikali imeingiza somo la mazingira katika ngazi ya skuli za msingi na kwenye ngazi za sekondari mada za masomo yanayohusiana na mazingira zimeingizwa kwenye somo la Jiografia na Uraia. Aidha, kwa kuwa somo la mazingira ni somo pana linalojitegemea, serikali imehamasisha Vyuo Vikuu mbali mbali Tanzania kufundisha fani za mazingira kwenye vyuo vyao. Hivi sasa fani mbali mbali za mazingira zinafundishwa kwenye Vyuo Vikuu vya Tanzania.

Sambamba na hilo, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kimeshaanza kusomesha Shahada ya Kwanza ya fani ya Afya ya Mazingira. Ni imani serikali kuwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kitaongeza fani nyengine za mazingira hatua kwa hatua ili kuhakikisha kuwa Chuo hicho kinatoa wataalam mbali mbali wa fani za aina tofauti za mazingira.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana na lugha ya staha aliyoitumia Mhe. Waziri katika kilijibu swali langu, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ametwambia hapa kwamba tayari Chuo Kikuu hiki cha serikali wameshaanzisha *degree* ya *Environmental Science* na kwa kuwa vijana wetu mara nyingi huwa wanapenda kwenda katika masomo mengine pale wanapotakiwa kwa mfano masomo ya *Arts* pamoja na masomo ya *Science* za kawaida hizi. Je, serikali imechukua hatua gani katika kuhamasisha wanafunzi wetu wanaomaliza kidato cha sita na wale wanaomaliza Stashahada katika vyuo mbali mbali kwenda pale *SUZA* kufanya *Environmental Science* kusudi kuweza kuinusuru Zanzibar hapo baadae kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na upungufu kwa kiasi fulani kwa wanafunzi wanaopenda kusoma masomo ya *Science*. Serikali imeliona hilo na kwa kweli inatoa kipaumbele cha kuwapa mikopo zaidi wanafunzi wanaokwenda kusoma masomo ya *Science*, ili wanafunzi wengi zaidi waweze kuvutika kusoma masomo hayo.

Lakini pia, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya jitihada za pekee za kuhakikisha kwamba inajenga skuli za mfano katika kila wilaya zenye vifaa vya kutosha kwa ajili ya kufundishia masomo ya *Science* ili kuweza

kuwasaidia wanafunzi wengi zaidi kujiunga na masomo ya *Science* na pia kuwahimiza kuchagua masomo ambayo yatakuwa na manufaa zaidi kwa nchi yetu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri.

(a) Mhe. Spika, pamoja na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala zima la kupambana na mazingira. Je, serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasaidia vipi katika suala hilo.

(b) Kama inasaidia ni maeneo yepi na yepi yameweza kusaidiwa katika Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali mawili (a) na (b) ya Mhe. Salmin Awadh Salmin kama ifuatavyo:-

Kwa kweli tuna mashirikiano ya karibu na Afisi ya Makamu wa Rais Mazingira katika masuala mbali mbali ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, lakini vile vile katika suala zima la mazingira. Katika maeneo ambayo moja kwa moja Ofisi yetu ilishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais ni pale Zanzibar ilipokumbwa na athari ya kuwa na unga mbovu ambao ulishindwa kupata sehemu ya kuweza kuuharibu. Kwa hivyo, tulishirikiana nao na kuweza kuupeleka katika kiwanda cha saruji kuweza kuharibiwa, kwa sababu katika kiwanda kile kuna vifaa hivyo.

Lakini la pili, vile vile, kupitia miradi mbali mbali ya kimataifa ambayo inakuja kwa jina la Tanzania. Tayari kuna mradi ambao ulitegemewa kuanza muda mrefu, lakini kwa kweli taarifa tunazopata ni za utatanishi kwamba umeanza haujaanza, pesa zimekuja, pesa hazijaja. Ni mradi wa nchi ambazo zinaendelea unaojulikana kwamba *Global Environmental Fund* ambao ulitegemewa kulipa Tanzania Dola laki tatu, mia tatu na hamsini na sita kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na fedha hizo zilitegemewa kugawiwa katika maeneo ya Bagamoyo, Rufiki, Pangani na kwa upande wa Zanzibar fedha zingetumika kama zingekuwa zimepatikana katika maeneo ya Kilimani, Chumbe na Ukele pamoja na Kisiwa Panza katika shughuli nzima ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

Lakini hadi hii leo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar haijapokea hata shilingi moja kutokana na mradi huu pamoja na kauli zinazotolewa na Afisi ya Makamu wa Rais kwamba fedha hizi zimeletwa tayari Zanzibar.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru na mimi asubuhi kuweza kuniona. Mhe. Spika, kwanza mimi namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Ikiwa chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabia nchi inatokana na hewa ukaa. Mhe. Waziri nilisikia hapa kwamba kuna taasisi sita zilizoshughulikia katika tatizo hili. Nikiomba kujua kwamba taasisi hizo zimezingatia maeneo gani?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ahsante sana kwa idhini yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Rufai Said Rufai kama ifuatavyo:-

Taasisi nyengine ambazo zilihusika katika mradi huu ni Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha *role* yake ilikuwa ni katika kuanzisha mfuko wa mazingira kwenda ku-*study* katika nchi za wenzetu na kupitia mifuko ya kimataifa kuona ni jinsi gani Zanzibar yenyewe inaweza kuanzisha mfuko wake wa kuweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Lakini pia, *KODECO* ambayo ni Jumuiya ambayo si ya kiserikali, ambayo nayo kazi yake ni kutoa elimu kwa jamii. Utakumbuka kwamba nilieleza kwamba madhumuni makubwa ya mradi huo ilikuwa ni kujenga uwezo wa kuhimili na kusimamia mabadiliko ya tabia nchi. Fedha hizo pia zimetumika na Idara ya Nishati. Pia, wao ni wadau kwa kuweza kuona jinsi gani wanaweza ku-*study* utumiaji wa nishati mbadala, badala ya kutegemea miti kukata kwa wingi.

Lakini vile vile, fedha hizo zimetumiwa na Chuo Kikuu (*SUZA*) kwa ajili ya kufanya tafiti mbali mbali katika kusaidia mabadiliko ya tabia nchi. Kupitia Idara ya Mazingira fedha hizo hasa ndio zilizotumika katika ku-*study* suala zima kwanza la kuweza kujua jinsi gani tatizo la mabadiliko ya tabia nchi lilivyo hapa katika visiwa vyetu,

lakini vile vile, limeweza kupitia mradi huo kuandaa mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Spika, suala hili ni refu sana na ingependeza zaidi kama Mheshimiwa angelileta kama swali mama, kwa sababu ni refu mno.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru, ahsante sana. Tunaendelea.

Nam. 16

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibuwa swali langu Na. 16 naomba uniruhusu nusu dakika tu. Swali hili Mhe. Spika, lilipokuja Mhe. Naibu Waziri alikuwa shahidi katika Kamati yako ya Wizara ya Kilimo, Biashara na Fedha, kilio hichi kilikuwa mbele ya Kamati ikiwa ziarani Pemba. Ninataka nikumbushe tu Mhe. Naibu Waziri kilio hichi anakielewa na wananchi wa Pemba hivi sasa wapo tayari, serikali itoe jawabu swali Nam. 16.

Kumekuwa na kilio cha wakulima na wauzaji wa karafuu hasa kisiwani Pemba wakati wanapopimiwa karafuu zao na pale zinapofikia bakaa ya nusu au robo ambayo huwa hawalipwi na badala yake hulipwa kwa kilo nzima na kuendelea. Malalamiko haya yamekuwepo siku nyingi na wizara inayafahamu.

a) Kwa nini serikali haitowi kauli juu ya malalamiko haya ya wakulima na wauzaji wa karafuu kupata haki yao hata kama kiwango kidogo.

b) Kutokana na wauzaji wa karafuu kutolipwa bakaa ya nusu au robo ya karafuu zao, serikali haioni kuwa inadhulumu haki za wakulima hawa kwa vile mizani inatakiwa ilipwe kama ilivyo kwa haki.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana. Kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 16 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kweli ni sahihi tulikuwa wote wakati tunatembelea vituo kule Pemba pamoja na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakubaliana naye kabisa Mhe. Mwakilishi kwamba katika siku za nyuma kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima na tulishuhudia malalamiko hayo pale wamapouza karafuu zao hasa Kisiwani Pemba kwamba zinapimwa, basi karafuu hizo katika vituo na kubakia bakaa la nusu kilo au robo kilo walikuwa hawalipwi na badala yake, walikuwa wanalipwa kilo zile zinazotimia tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kufuatia malalamiko hayo ndipo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia Shirika lake la ZSTC likaamua kwa makusudi kabisa kununua mizani mpya za kisasa na zenye mfumo wa kieletroniki. Kwa mizani hizi Mhe. Spika, wakulima wa karafuu wanapimiwa karafuu zao zote na zinalipwa karafuu zote kama ambavyo inasomeka katika mizani hizo za eletroniki.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitomshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa umakini wake na kwa ukweli wake na baada ya kuona suala hili kuna tatizo na kujipanga kupeleka mizani mpya. Mhe. Spika, nimshukuru sana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umeuliza swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aah! hamna swali la nyongeza isipokuwa ninamshukuru tu Mhe. Naibu Waziri kwa umakini, umahiri na ukweli wake aliouonesha juu ya suala hili.

Mhe. Spika: Haya ahsante. Mhe. Salma Mohamed Ali. Shukurani utazipokea wakati ukijibu swali la nyongeza la Mhe. Salma Mohamed Ali.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa wauzaji wa karafuu pia wana malalamiko ya kukatawa kilo mbili za gunia. Ninamuomba Mhe. Naibu Waziri atufahamishe gunia tupu lina uzito gani.

b) Thamani yake ni kiasi gani hilo gunia tupu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ahsante sana. Kama nimemsikia vizuri Mhe. Salma Mohamed Ali swali lake anaulizia uzito wa gunia ambalo halina karafuu.

Mhe. Spika, lina uzito wa kilo moja, ile huwa inapunguzwa wakati wa kutoa hesabu ya kumlipa mkulima karafuu zake.

Mhe. Spika: Swali. Eeh! Mheshimiwa Salma Mohamed Ali.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, mimi nilielezea hapa kwamba wakulima wa karafuu wana malalamiko kama wanakatwa kilo mbili za gunia na nilitaka nijue hilo gunia tupu lina uzito ambalo tayari nimeshajibiwa, lakini ile thamani ya gunia hilo ni bei gani bado sijapata jawabu yake.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri thamani ya gunia.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, wakati ninamjibu Mhe. Salma swali lake, kwa kuwa bei ya karafuu huwa inatofautiana kwa kilo kufuatana na soko la dunia. Kilo moja ile ya gunia huwa inapunguzwa wakati wa kufanya hesabu ya kilo za karafuu ziliosomeka kwenye mizani.

Mhe. Naibu Spika, Mathalani kama kilo zimesomeka ni mia moja na moja, ile kilo moja huwa inatolewa haipigiwi thamani kwenye kumlipa yule mkulima, ndio nilivyokusudia Mhe. Spika, na ndivyo inavyofanyika.

Mhe. Spika: Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali yake mazuri. Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu maswali mama alieleza kwamba kuondoa tatizo hilo, shirika liliweza kununua mizani mpya za eletroniki. Je, ni mizani ngapi zilizounuliwa za eletroniki ili kuondoa tatizo hilo kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mizani ambazo ZSTC imenunua ni 40 za eletroniki na mizani hizi zimepelekwa kwenye vituo vyote, lakini zimeanza kufanya kazi kwenye vile vituo tu ambavyo tayari kuna miundombinu ya umeme kwa sababu mashine hizi zinatimia umeme katika ufanyaji kazi wake.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri tunakushukuru ahsante sana.

Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi ya kuwashukuru na kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata, ninafikiri mutakumbuka kwamba katika Kamati ya Uongozi tulikubaliana baadhi ya mambo wakati wa mjadala, tutakubaliana, basi yafaa taratibu zetu kidogo tuzitengue kwa mnasaba wa haja ya shughuli yetu ya Baraza hili la bajeti.

Kwa hivyo, kabla hatujaendelea na hoja iliyokuwepo mbele yetu, naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Kanuni ya 96 (2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinaelekeza kuwa Waziri atawasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yake kwa muda usiozidi saa mbili na kwa kuwa Kanuni ya 58 (6) inaelekeza kwamba wakati wa mkutano wa bajeti kila Mjumbe anayejadili hoja atatumia muda usiozidi dakika 30 na kwa kuwa baadhi ya Wajumbe wa Baraza na Sekretarieti ya Baraza wanakabiliwa na shughuli mbali mbali za Kitaifa katika mwezi wa Julai ikiwemo shughuli za maandalizi na shughuli za baadhi ya Kamati katika Bunge Maalum la Katiba na hivyo kuwepo umuhimu wa kumaliza mkutano wa bajeti mwisho mwa mwezi wa Juni 2014.

Mhe. Spika, na kwa kuwa ili kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kutumia muda vizuri zaidi na kumaliza shughuli za mkutano wa bajeti kwa wakati ambapo Baraza limejiweka kwa mujibu wa ratiba na hivyo kutoa fursa kwa Wajumbe wa Baraza na Sekretarieti ya Baraza hilo kutekeleza majukumu mengine ya Kitaifa, yakiwemo maandalizi ya Bunge Maalum la Katiba, upo umuhimu mkubwa wa kutenga Kanuni kando ili kutekeleza hayo niliyoyaeleza.

Mhe. Spika, hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 156 (1) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012, naomba kutoa hoja ya kutenga kando Kanuni ya 96 (2) na Kanuni ya 58 (6) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi na badala yake utumike utaratibu ufuatao:-

- a) Kwamba kila waziri anapowasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yake atatumia muda usiozidi saa moja,
- b) Kwa Mwenyekiti wa Kamati anapowasilisha maoni ya Kamati yake atumie muda usiozidi dakika 40, na
- c) Kila Mjumbe anayejadili hoja atumie muda usiozidi dakika 20.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, naomba sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa hoja. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe katika mtiririko wa shughuli zetu, utaratibu utakaokuwa unatumika badala ya utaratibu wa kawaida wa ndani ya Kanuni, ni huu ulioelezwa katika vijifungu vya hoja hii (a), (b) na (c). Hata hivyo, kuna jambo moja ambalo hatukujiweka, lakini hilo kimsingi hata ndani ya Kanuni halimo na kwa hivyo, itategemea kiti kinaelekezaje. Nayo ni suala zima la utaratibu wa kufanya majumuisho. Kwa kawaida wakati mwengine muda mrefu sana huwa unakwenda katika kutayarisha majumuisho ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Niwaomba basi Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wao wahakikishe wanahudhuria kwenye vikao vyetu wakati mjadala unaendelea ili waweze kumsaidia Mhe. Waziri pale hoja zinapoanza kutolewa ili mara tu baada ya mjadala kufungwa, basi Mhe. Waziri awe tayari kufanya majumuisho kwa kipindi kifupi kadiri inavyowezekana.

Basi niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri muwahimize watendaji wenu wawepo pale juu, wawe wanasikiliza mjadala ili kuweza kumsaidia Mhe. Waziri kwa wakati. Hatutokuwa na muda wa kumsubiri Mhe. Waziri akajitayarisha.

Kwa mnasaba huu, mjadala unamalizika basi tunamuomba Mhe. Waziri aweze kutoa majibu hapo hapo. Kwa sasa ninaona pale juu pana watu wachache sana, sijui kama wanahusiana na hoja ziliopo pale mbele yetu, lakini basi niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wawahimize watendaji wao wawepo hapa ili kusikiliza mjadala wa hoja mbali mbali ambazo zinafika katika Baraza letu.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nimuombe Katibu tuendele ili baada ya hapo tuanze mjadala wetu. Katibu.

(Majadiliano yanaendelea)

Waheshimiwa Wajumbe hoja zote mbili hizi ziliungwa mkono mara baada zilipowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri, kwa maana hiyo sasa zipo tayari kuweza kujadiliwa. Kama kawaida nafasi ya kwanza namkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati zako tukufu za Baraza la Wawakilishi, naomba kuwasilisha ripoti mbili kwa kila ripoti moja dakika 40. Kwa hivyo, nitakuwa nina dakika 80.

Vile vile, kuna dakika zangu kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Kwamtipura. Kwa hivyo, ninaamini utanipa dakika 120 ili niweze kutawala jukwaa hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa tuna utaratibu wa kuendesha shughuli zetu za Baraza na kawaida mkutano wetu huu inapokuwa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi hawajatimia ndani ya ukumbi huu, basi huwa Baraza unaliahirisha ili kuwaita. Sasa Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ndio Mwenyekiti wa Wenyeviti na hapa sasa hivi nasoma bajeti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo kuna mpango wa maendeleo ambao umekusanya wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, haya tunayoyazungumza hapa na bajeti tunayoipitisha hapa, inakwenda zaidi kusimamiwa na Makatibu Wakuu.

Mhe. Spika, lakini nikiangalia kule juu ambapo kuna ile *floor* ambayo Makatibu Wakuu wanatakiwa wawepo, hayupo hata mmoja. Sasa Mheshimiwa Spika, mimi sitoridhika kusoma hotuba hii ya bajeti ambapo watendaji hawa hawapo.

Mhe. Spika, Sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wenyeviti, naomba kutoa hoja uliahirishe Baraza lako kwa muda wa dakika 10, ili Makatibu Wakuu wote na Wakurugenzi wapigiwe simu waje katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, kuja kusikiliza ni namna gani Wawakilishi wao wanayachambua, lakini vile vile, wanawaelekeza na pia kupitisha bajeti ya serikali ambayo wao watakuwa ni wasimamizi wakubwa.

sasa Mhe. Spika, kabla hujaanza kunihesabia dakika zangu, naomba kutoa hoja uliruhusu kuliahirisha Baraza hili kwa muda wa dakika 10 ili tuwasubiri wenzetu waje wapokee ripoti hii. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Haya Waheshimiwa Wajumbe, shughuli zetu zinakwenda kunapokuwa na mahudhurio ya Waheshimiwa Wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe wapo, *quorum* imetimia, jambo hili la kutoa hoja kwamba tuahirishe shughuli zetu kuwangoja wale watendaji, huo ni wajibu wa mawaziri wenyewe watawatafuta. Shughuli hii iendele, hoja hiyo siitowi ili ikaungwa mkono. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti, uje usome ripoti ya Wenyeviti, karibu sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi): Mhe. Spika, baada ya kuikataa hoja yangu. Sasa kwa ruhusa yako naomba nianze kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Wenyeviti ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, kwanza hatunabudi sote kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia sote kukutana tena tukiwa wazima wenye afya njema, kuja kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar, walituchagua kuja kuwakilisha hapa kwenye chombo hiki kikubwa cha Baraza la Wawakilishi la wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pili, naomba kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza, kuichambua bajeti hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhata kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (D.k Ali Mohd Shein) kwa uongozi wake bora wenye hikma, busara, huruma na imani kubwa kwa wananchi wake wa Zanzibar anaowaongoza kwa kushirikiana na wasaidizi wake wakuu. Makamo wa Kwanza wa Rais (Maalim Seif Sharif Hamad) na Makamo wake wa Pili (Balozi Saeif Ali Iddi). Tunawaomba wananchi wote wa

Zanzibar kuwapa mashirikiano makubwa ili waweze kutekeleza malengo yao ya kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Zanzibar bila ubaguzi na upendeleo wa aina yoyote.

Mhe. Spika, nne pia, napenda kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na timu yake kuanzia Katibu Mkuu, Mkurugenzi, Tume ya Mipango yote, ambao ndio walioandaa mipango hii tunayoijadili hapa leo. Pia, sikuwasahau watumishi wote wa wizara hii pamoja na madereva wao wote.

Mhe. Spika, pia nawapongeza wenyeviti wenzangu wote ambao tumeshirikiana kuandaa ripoti hii ya Kamati ya Wenyeviti, kuichambua ripoti hii iliyowasilishwa kwetu na Waziri wa Nchi Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Spika, pia, nitakua mwizi wa fadhila kama sikuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, walionileta hapa kuja kuwakilisha hapa Barazani, kama kawaida yangu nawaahidi kuendelea kuwa mwaminifu kwao na kutumia maarifa na bidii zangu zote, ili kuwaondolea kero zao jimboni kwangu na zile zilizomo ndani ya uwezo wangu na pia kuishauri serikali ipasavyo kuwaletea maendeleo jimboni kwetu na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, baada ya shukrani hizo, sasa naomba kuanza kuichambua hotuba ya Mhe Waziri, kuhusu Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa hapa Zanzibar kwa mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, lakini kabla kuanza kuzichambua hotuba mbili za Mawaziri wa Fedha na wa Mipango, ningeliomba tukapata taarifa ya serikali kuhusu maradhi mapya ya Dengue, yaliyoingia huko kwa majirani zetu Tanzania Bara. Nilitaka kujua, je, serikali yetu imejipanga vipi kuhusu kuwalinda wananchi wetu na maradhi haya ambayo kwa taarifa tunaambiwa hayana kinga wala tiba.

Mhe. Spika, naungana na Mhe. Waziri kuwapongeza Wazanzibari wote, kwa kusherehekea Mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar, yaliyotutoa kwenye unyonge wa kutawaliwa na kujitawala wenyewe Zanzibar kuwa Jamhuri na kuepukana na kuitwa raia wa Sultan, ambapo wananchi wamejitawala wenyewe bila ya usimamizi wa mtu yeyote kutoka nje, jambo ambalo hadi leo tunajivunia. Naomba wananchi sote tuendeleo kuyalinda Mapinduzi yetu hayo, kwani ndio kielelezo cha utu wetu, lakini pia, tuhakikishe na kizazi chetu kinachokuja na kusherehekea miaka mia moja ya Mapinduzi ijayo, tukiwa pamoja na sisi kwa wale Mwenyezi Mungu atakaotuweka hadi siku hiyo.

Mhe. Spika, lakini isiwe ni kusherehekea tu bali ni kuyalinda na kudumisha dhamira na malengo ya Muasisi wetu wa Mapinduzi ya Zanzibar, Sheikh Abeid Aman Karume, ambapo alileta Mapinduzi ili kuondoa ubaguzi wa rangi, kabila, dini au asili ya mtu na kutufanya sote kujiona kuwa ni wamoja na kusaidiana kwa hali na mali, kwa kheri na shari.

Mhe. Spika, kwa kuwa hivi sasa viongozi wetu wametuletea Serikali ya Umoja wa Kitaifa, basi hili ndilo lililokuwa lengo la Mapinduzi ya mwaka 1964, kwani wakati huo wananchi walilazimishwa kuvunja vyama vyao, ili kuwa wamoja na kuondoa kufarikiana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu za kisiasa. Kwa hivyo, tunaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dk. Ali Moh'd Shein, kwa kuendeleza malengo hayo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Waziri kwenye kitabu chake cha pili, kuhusu hali ya uchumi na mpango wa maendeleo kwa uchumi wa Zanzibar, unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.8 kutoka asilimia 7.4 ya mwaka uliopita. Kwa kuendelea kuendeleza utekelezaji wa mpango mkuu wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar wa awamu ya pili. Malengo ya Milenia 2015 na Dira ya Maendeleo ya *vision 2020* na vile vile ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/15.

Mhe. Spika, kutokana na muda sitoweza kuzungumzia hali ya uchumi duniani na mfumko wa bei duniani pamoja na Afrika, isipokua nitajikita moja kwa moja kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza waziri kuwa uchumi wetu unategemea kukua kwa kiwango cha asilimia 7.8 kwa mwaka 2014/15, hasa kwa matarajio ya kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za utalii hapa Zanzibar. Pia, kuwashirikisha wananchi moja kwa moja kapitia utalii kwa wote, kwa kuulinda na kuwashirikisha moja kwa moja wananchi.

Mhe. Spika, kwa kuwa hivi sasa utalii kwa kiasi kikubwa ndio tegemeo la uchumi kwa nchi yetu, basi iko haja kwa serikali yetu kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wote, ili kujua umuhimu wake kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwani hata sekta ya huduma ambayo ndio inachukua nafasi kubwa zaidi ya asilimia 44 katika uchumi wetu, basi inachangiwa zaidi na kuimarika kwa sekta ya utalii.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha Sekta ya Utalii inaimarika, basi kwanza ni lazima kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yote ya utalii, kwani katika siku za hivi karibuni kumekua na vitendo vya uhalifu kwenye maeneo ya utalii, jambo ambalo kama halikuchukuliwa hatua linaweza kuvuruga uimarikaji wa utalii wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pili, ili kuhakikisha utalii unaimarika hapa Zanzibar, kwa kuwa tumeona ndio tegemeo kubwa kwa uchumi wetu, basi ni lazima kuhakikisha suala la amani na utulivu linaimarika hapa Zanzibar, kwani kukiwa na vurugu na mifarakano, basi hata hao watalii wataogopa kuja na kuvuruga mapato yetu ya hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, utalii unatoa ajira nyingi sana hapa Zanzibar hata kule Tanzania Bara, kwani wakulima wa mboga mboga, wauza samaki, wauza matunda, wenye magari ya *Tour Operators*, magari ya mizigo, *taxi*, wavuvi, wafugaji kuku wa nyama na mayai, watembeza wageni, wauzaji vinyago, wauzaji vitu vya asili ya Kizanzibari, wapiga ngoma za utamaduni, waajiriwa mahotelini, wenye boti za kutembeza wageni, wauza vyakula mbali mbali, wauza maji, walinzi, mafundi ujenzi, wauza mafuta ya *petrol* na *diesel*, wasuka makuti, warushaji vishada, wakandaji yaani (*massage*), vinyozi, wauzaji wa vifaa vya ujenzi, vyo vyenye kutoa taaluma ya utalii, nakadhalika.

Mhe. Spika, hawa wote tegemeo lao kubwa ni Sekta ya Utalii. Kwa hivyo, ikiwa utalii haupo, basi na wao vile vile wataweza kuathirika.

Mhe. Spika, kwa hivyo, tunaiomba serikali iko haja ya kuimarisha miundombinu itakayowawezesha watalii kupata huduma bora watakapokuja hapa nchini kwetu, ikiwemo kuimarisha viwanja vyetu vya ndege, barabara, kuongeza vivutio vya utalii, kuongeza maeneo ya kutembeza wageni, kuiweka miji yetu katika hali ya usafi na kuimarisha ulinzi kwa watalii.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu inategemea zaidi mapato yake kutokana utalii, lakini bado hatujawekeza ipasavyo katika kutoa taaluma ya kutosha, kwa ngazi zote kwenye chuo chetu cha utalii, kwani hadi leo chuo chetu cha hoteli na utalii pale Maruhubi, hakijaweza kutoa *degree* kwa wahitimu wetu, jambo ambalo linasababisha nafasi za juu katika ngazi ya ajira kuendelea kuchukuliwa na wageni na vijana wetu wanabakia kuwa waajiriwa kwenye ngazi za chini.

Mhe. Spika, ingawa katika mipango mipya tumepewa taarifa na Mhe. Waziri wa Mipango, kuwa hivi sasa kuna maandalizi ya chuo chetu hicho cha hoteli na utalii, kuwekwa chini ya *SUZA*, ili kujiandaa kutoa vyeti vyenye hadhi kubwa, lakini hofu yetu bado iko pale pale, hata chuo hiki kikipelekwa *SUZA*, je, kuna maandalizi gani ya kukipatia fedha, nyenzo, walimu walioboea katika masuala ya taaluma ya utalii, lakini hata ukiangalia *Scheme of Service* ya chuo, je, ni kweli itaweza kumvutia mwalimu aliyeboea kuja kufundisha katika chuo hicho cha utalii?

Mhe. Spika, Nadhani bado tuna safari ndefu ya kuimarisha utalii wetu, ili wananchi wetu waweze kufaidika na matunda ya utalii kwenye nchi yetu.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaitaka serikali kuongeza juhudi za kuutangaza utalii wetu, kwa kutenga pesa nyingi za kuutangaza utalii, kwani hadi hivi sasa juhudi kubwa za kuutangaza utalii hufanywa zaidi na wawekezaji wenyewe hasa wenye mahoteli, pamoja na *Tour Operator*. Kama ingelikua sio jitihada zao, basi utalii wetu ungelikua nyuma sana. Tunawapongeza wawekezaji wetu hawa na tunawaomba wasichoke kuutangaza utalii wetu. Pia, tunapongeza jitihada zinazofanywa na waandaaji wa matamasha mbali mbali hasa *ZIFF*, Sauti ya Busara, ambayo huitangaza Zanzibar duniani kupitia mitandao ya kijamii mbali mbali, ili kuwafanya wageni kuja kushiriki kwenye matamasha hayo.

Mhe. Spika, pamoja na hayo, iko haja ya kuvilinda na kuvienzi vivutio hivyo vya utalii, ili tuwe na vitu vya kuonyesha. Kamati yangu imesikitishwa sana na serikali kuliacha jengo la *Beit-El-Ajaib* kuporomoka, wakati mapato yanayopatikana katika jengo lile yangukuwa yanahifadhiwa vizuri na yanalihudumia jengo lile, kwani

yanatosha kabisa kulihudumia jengo lenyewe. Kamati yangu, inaitaka serikali kuanzisha mfuko maalum ili sehemu ya pesa zinazopatikana pale zibakie pale, ili kuliendeleza jango hilo, ile ni hazina kubwa kwa nchi yetu na tuitunze.

Mhe. Spika, lakini pia, tunaitaka serikali kudhibiti ujenzi unaoendelea Mji Mkongwe, kwani umenza kupoteza uasilia wa majengo yake na kujenga majengo ya kisasa, jambo ambalo linaweza kuiondoa Zanzibar kwenye miji yenye urithi wa Kimataifa.

Mhe. Spika, vile vile, kuimarisha usafi na ulinzi katika maeneo yote ya utalii ikiwemo Mji Mkongwe na kuwaondoa walaji unga ambao huwasumbua sana watalii katika maeneo hayo. Pia, kuitunza na kuiimarisha Bustani ya Mji Mkongwe, ambayo ni bustani pekee kwa Zanzibar yenye kuvutia na kulitunza jengo lililokuwa la kulelea watoto pale Forodhani, tukiweza kuyafanya hayo, basi utalii wetu kweli utaweza kuimarika.

Mhe. Spika, pamoja na serikali kuelezea kuwa uchumi wetu unatarajia kuimarika katika mwaka ujao kwa kuimarisha mazingira mazuri ya biashara, lakini suala hili inabidi serikali kulitekeleza kwa vitendo na sio kwa maneno mazuri tu kwenye vitabu, kwa kuacha urasimu kwa wawekezaji hasa wazalendo, kwa kuwaondolea vikwazo baadhi ya wazalendo hasa wanapoamua kueleza katika uwekezaji mkubwa, kwani wapo wazalendo walioamua kueleza uwekezaji mkubwa, lakini kuna baadhi ya watendaji serikalini wamewawekea vikwazo kwa makusudi ili kuwakwamisha.

Mhe. Spika, kwa mfano kuna mzalendo Mzanzibari ambae ameanzisha ujenzi wa Chelezo kule Mangapwani, ameshafanya kazi kubwa, ametumia pesa zake nyingi, pamoja ya kuwa ameshapata hata cheti cha mazingira, kinachothibitisha kuwa mradi huo haunaathari ya mazingira, lakini kuna watumishi wachache tu wa serikali, kwa dhamana walizopewa na serikali, wameamua kwa makusudi kuukwamisha mradi huo, hivi sasa kwa zaidi ya miaka mitatu kwa tamaa zao.

Mhe. Spika, serikali yetu inawatafuta wawekezaji kutoka nje kuja kueleza hapa kwetu, wakati huo huo inawazuia wazalendo kuwekeza ndani ya nchi yao. Hili halikubaliki hata kidogo, kwa kweli hali hii inasikitisha sana kwani mradi huu wa Chelezo ungeluweza kuzalisha ajira zaidi ya vijana mia mbili kwa wakati mmoja, lakini mradi huo unaendelea kukwamishwa. Sasa sielewi kwamba tunakwenda au tunarudi nyuma.

Mhe. Spika, kwa nchi yeyote iliyo makini, basi huwawezesha wananchi wake kuwatengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji, ili kuimarisha uchumi ndani ya nchi zao. Pia, isitoshe kuna wazalendo wengine ambao nao pia wanayo maeneo yao ya uwekezaji pembezoni mwa fukwe za bahari, lakini kwa makusudi kuna baadhi ya watendaji wa serikali kwa dhamana walizopewa na serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa tamaa zao na kwa kushirikiana na wawekezaji wa kigeni.

Mhe. Spika, kwa mfano Hoteli ya Cristal Hotel kule Paje ambayo kila mwaka tunairipotia dhulma wanayoifanya wameamua kumzuia mwananchi mzalendo asijenge kwenye eneo lake, wakati mgeni huyo mmiliki wa hoteli hiyo analitumia eneo hilo la mzalendo huyo, kwa kujipatia mapato kwa kujenga vibanda (Bangaloo) na kulaza wageni wake. Mawaziri nyote ambao mmepewa dhamana na Mhe. Rais, ili kuwatumikia wananchi mnalijua, lakini nyote mnapuuzwa, kwa kuwa nyinyi mambo yenu yamewanyookea, lakini ya wenzenu hamna habari nayo, sijui kuwa huo ndio uwajibikaji au vipi.

Mhe. Spika, hii ni dhulma kubwa haikubaliki na niaahidi kuondoa shilingi kwenye mishahara wa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ardhi kwa kushindwa kuwajibika kuzuia dhulma anayofanyiwa mzalendo huyo kule Paje, ambae pamoja na dhulma yote anayofanyiwa, lakini yeye anaendelea na jitihada zake na amekwisha kutuletea wahisani tofauti ili kutusaidia miradi mbali mbali ya kijamii kama vile ya maji kule Makunduchi pamoja na Uzi.

Mhe. Spika, vile vile, ameshaleta vifaa vya Hospitali Mnazi mmoja, kuboresha vituo vya afya na sasa hivi wana mpango wa kuboresha vituo vya afya vya vijijini, lakini vile vile, ujenzi wa madrasa, miskiti nakadhalika, sio hivyo tu bali pia watasaidia Sekta ya Elimu vijijini, sasa leo mwananchi kama huyu pamoja na kudhulumwa ndani ya nchi yake, lakini bado amebaki na uzalendo wake wa kuisaidia nchi yetu, lakini sio huyo tu, bali pia kuna wananchi wa Nungwi na Pwani Mchangani ambao tayari wameshapata wabia wa kueleza kwenye maeneo yao.

Mhe. Spika, lakini serikali hii tukufu ya Zanzibar inayoongozwa na D.k Ali Mohamed Shein kupitia waziri aliyepewa dhamana ya ardhi ameshindwa kuwapatia Hati miliki wananchi hao wanyonge alau na wao

wakaondokana na umasikini uliokithiri kupitia rasilimali yao hiyo waliyonayo. Sasa hapa ndio pale tunapojiuliza, je, hayo ndio mazingira mazuri ya biashara serikali inayotuahidi?

Mhe. Spika, hapa tunamuomba Mhe. Rais kuingilia kati masuala haya yote niliyoyataja hapo juu kwani inaonyesha mawaziri wake yamewashinda na sisi tutamsaidia kutatua matatizo hayo. Kwani maeneo hayo yana uwekezaji mkubwa, lakini wananchi wetu wanakwamishwa kwa makusudi.

Mhe.Spika, pia, kuna baadhi ya wawekezaji ambao wanayatumia maeneo ya wazalendo kueleza kwa makubaliano nao, lakini wameshindwa kuwalipa haki zao wananchi hao, kwa mfano mwekezaji kutoka Tanzania Bara mwenye Hoteli ya kitalii kule Michamvi Bw. Magembe ambaye Mheshimiwa Waziri anamjua ipasavyo, kwa zaidi ya miaka mitano, sasa yeye anazalisha pesa ndani ya eneo la watu, lakini hataki kuwalipa wananchi wale haki zao na taarifa hizi Waziri wa Fedha anazo, lakini amelipuuza.

Mhe.Spika, kwa hiyo, tunaitaka serikali yetu kusimamia haki za wananchi wetu kutoka kwa wawekezaji ambao wengi wao wamekua na kibri kwa kusema hawaogopi kwani serikali wameiweka mikononi mwao na kwa kuwa wanawadhulumu wazalendo ndani ya nchi yao na sisi sote tunawaangalia tu bila ya kuwachukulia hatua za kisheria, basi hiyo kauli yao inakua ni ya kweli.

Mhe.Spika, serikali inapozungumzia kuimarisha mazingira bora ya biashara hapa Zanzibar tunaomba isiwe kwa maneno, bali iwe kwa vitendo, inaonekana kuwa bado serikali iko mbali sana na wawekezaji wetu hasa kwenye Sekta ya Viwanda kwani kuna bidhaa nyingi ambazo huingizwa kutoka nje ya Zanzibar wakati bidhaa hizo nyingi pia huzalishwa hapa Zanzibar, hii inatokana kwa serikali kutokua na sera madhubuti ya kuvilinda viwanda vya ndani kama ilivyo kwa nchi nyengine ili kulinda ajira kwa Wazanzibari na kuvikuza viwanda hivyo na kuongeza pato la Taifa.

Mhe.Spika, kwa mfano leo Zanzibar kuna viwanda zaidi ya vinne vya maji, lakini bado kuna maji mengi huingizwa hapa nchini inaonyesha kuna ukwepaji wa kodi kwa bidhaa hizo zinapoingia Zanzibar tunaitaka serikali kulifanyia utafiti suala hilo na ripoti iletwe Barazani.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaitaka serikali kuyapima na kuyapatia Hati miliki maeneo huru ya kiuchumi yalioko huko Fumba na Micheweni na pia kuiwekea miundombinu ya kiuchumi ikiwemo barabara, maji umeme na pia kutangaza punguzo maalum la kodi kwenye maeneo hayo ili kuwavutia kuja kueleza hapa Zanzibar, leo zaidi ya miaka 30, serikali imeyatangaza maeneo huru ya kiuchumi, lakini hakuna miundombinu yeyote iliyowekwa, bali ni mwitu mtupu, je, ni mwekezaji gani atakaevutiwa kuja kueleza katika maeneo haya?

Mhe. Spika, tusidanganyane hapa katika dunia ya leo, nchi bila ya kuwa na viwanda vikubwa, vidogo na vya kati, basi tutaendelea kuwa omba omba siku zote. Kwa hivyo, basi hebu tumize vichwa vyetu kwa sote ili kuona ni namna gani tutafanya ili kuvutia wawekezaji wa viwanda kuja Zanzibar kueleza katika Sekta ya Viwanda. Kutengeza bidhaa na kuuza nje na kuongeza ajira.

Mhe. Spika, mazingira mengine ya biashara hapa Zanzibar ni kuzipa kipaumbele Kampuni za ujenzi za hapa Zanzibar, kwani wao ndio walipa kodi wakubwa hapa nchini, lakini tatizo mawizara wanapotoa *Tenders* kwa miradi mikubwa ya ujenzi, basi kazi hizo hupewa makampuni ya nje na kuwaacha makampuni ya ndani kuangalia tu wakisota hawana kazi za kufanya na tumeshuhudia miradi mingi tu ya ujenzi imepewa makampuni ya nje ya Zanzibar hasa Wizara ya Elimu na kazi hizo zimekwama hadi leo zimeshindwa kukamilika kwa wakati na kuitia hasara serikali ambapo wanaoumia ni wananchi.

Mhe. Spika, kwa hiyo, tunaitaka serikali dhana hiyo ya kuimarisha mazingira bora ya biashara, basi kipaumbele kiwe kwa wazalendo kwanza na mfano mzuri ni nchi ya China na Marekani, *Tender* yeyote inayotolewa na serikali, basi kazi hiyo kipaumbele cha mwanzo, basi hupewa Kampuni ya kwao ili kuyainua Makampuni yao na kufaidi matunda ya kodi zao. Sasa sisi tunaogopa nini? Ni lazima na sisi tuanze leo.

Mhe. Spika, vile vile, tunaiomba serikali yetu kuhakikisha miradi mikubwa ya miundombinu inamalizika katika muda muafaka uliopangwa hasa mwaka huu wa 2014/15 ikiwemo barabara zinazojengwa na Kampuni ya Mecco kule kisiwani Pemba, kwani hivi sasa ni zaidi ya miaka mitano hazijakamilika kwa uzembe na tamaa za watu kuchukua chao mapema bila kujali kuwa wanaliangamiza Taifa.

Mhe. Spika, pia, uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar kila mwaka serikali imekuwa ikibadilisha kauli na kututia moyo kuwa utamalizika, lakini hatimae mwaka unamalizika tunaidhinisha pesa nyengine kodi ya wanyonge, lakini wachache hufaidika kwani wao hukusanya posho za vikao, safari za nje na kwenye *Tender* mwisho wa siku hakuna liwalo na nchi inaangamia. Kwa hiyo, tunaiagiza serikali kuikamilisha miradi hiyo kwani tumechoka na hadithi za *style* ya “*Design and Building*” na sasa tunataka uwanja wetu tuutumie, kwani tunategemea uwanja ule ukimalizika utaongeza ajira nyingi za Makampuni binafsi yatakayokuja kueleza na hata serikalini.

Mhe. Spika, pia, ajira zitaongezeka, sio hivyo tu bali mashirika makubwa mengi yatavutiwa kuanzisha safari za ndege kupitia Zanzibar, kwani huduma zote muhimu zitaweza kupatikana hapo, harakati zote hizo zitaongeza ajira kwa vijana wetu na kuongeza mapato ya serikali.

Mhe. Spika, Kamati yangu inapongeza jitihada za serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta binafsi kueleza hapa nchini ili kutoa ajira kwa vijana wetu, lakini bado hatujawawekea kinga ya uhakika wa maisha yao vijana hao kwa kulazimisha wawekezaji kuwapatia mikataba ya kudumu waajiriwa, ili kujihakikishia uhai wa maisha yao, lakini hali ilivyo sasa wafanyakazi wengi hasa kwenye mahoteli hawana mikataba ya ajira, jambo ambalo wanakua kama manamba tu ndani ya nchi yao.

Mhe. Spika, kwani inawalazimu kila mwaka ukimalizika msimu wa utalii, msimu mpya unapoanza tena inawabidi waombe kazi tena na wengi wao huachwa na kuajiriwa wengine. Kwa hiyo, hubaki kuhangaika tu huku na kule kutafuta ajira sehemu nyengine jambo ambalo hawana uhakika wa kupata ajira nyengine na mtindo huo ni wa kawaida hapa Zanzibar, Makampuni mengi huwa hawatoi mikataba ya kudumu ya ajira na hata wakitoa, basi haizidi mwaka mmoja.

Mhe. Spika, suala je, tutakua na mfumo wa waajiriwa vibarua hapa nchini kwetu hadi lini? Kwani ajira hizo huwa hazina kiinua mgongo? Kwani ni za mikataba mifupi? Hii ni hatari kwa maisha ya baadae ya watu wetu kwani wakifika umri mkubwa watakuja kuwa omba omba kwani hawakuwa na kinga ya ajira.

Mhe. Spika, Kamati yangu kwa hivi sasa inaona iko haja kubwa ya kuutilia nguvu ule mfuko wa kuongeza ujuzi “*Skill Development Levy*” ili fedha zile zipelekwe moja kwa moja kwenye vyuo vya amali na chuo cha Utalii, hata kwenye shule za ufundi kwa mfano JKU ili kuwapatia ujuzi vijana wetu kuweza kuwaandaa katika soko la ajira, aidha waweze kujijari wenyewe au kuweza kuingia kwenye soko la ajira pahala popote duniani, kwani tumeanza kuona wenzetu Kenya na Uganda tayari wanampango madhubuti kwa vijana wao wanaomaliza skuli kuwapatia taaluma na ujuzi na baadae kuwaunganisha na Makampuni yanayotoa ajira katika Falme za Kiarabu kwa utaratibu maalum na kuleta tija kwa nchi yao.

Mhe. Spika, sio hivyo tu bali serikali iandae mpango maalum wa kuwasomesha vijana wetu katika fani mbali mbali za mafuta na gesi, kwani eneo hili litakuja kuhitaji vijana wengi wenye ujuzi katika fani hiyo hasa ukizingatia mara tu baada ya kumaliza mchakato wa Katiba mpya, basi Zanzibar italazimika kuanza kutafuta wachimbaji wa mafuta na gesi kuja kuanza kazi hiyo hapa Zanzibar, sekta ambayo itakuwa ni kubwa, pana na inategemewa kuwa itakuwa ndio ufunguo wa mafanikio kwa uchumi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa hiyo, ni vyema basi serikali yetu kuweza kuwa na mipango thabiti kuhusu kuwaandaa kwa kuwasomesha ili vijana wetu kuja kupata ajira kwa vijana wetu katika sekta hii kubwa kwa Taifa letu.

Mhe. Spika, tunaomba sana kutokana na idadi ya vijana wengi kumaliza masomo yao katika viwango tofauti na kwa kuwa muajiri mkuu serikali haina nafasiya kuajiri wote basi ni vyema kuviimarisha vyuo vya ufundi ili kuwaandaa vijana aidha kujijari wenyewe au kuajiriwa wakiwa na taaluma tayari.

Mhe. Spika, sekta ya kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wa Taifa letu pamoja na taarifa iliyosomwa na Waziri wa Fedha kuwa mazao ya kilimo yameongezeka ikiwemo mpunga, lakini tunaitaka serikali kuyatambua maeneo yote ya kilimo hasa yanayolimwa mpunga na kuyalinda yasiyengwe majumba, kwani kila siku zikienda mabonde ya mpunga yanaendelea kuvamiwa kwa ajili ya kujenga nyumba za kuishi, jambo ambalo linarejesha nyuma jitihada za kujitegemea kwa mazao ya kilimo.

Mhe. Spika, kwa kua bado Taifa letu linategemea kilimo na ndio sekta kubwa inayotegemewa na wananchi kwa kuendeshea maisha yao, basi sasa wakati umefika kwa serikali kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuweza kuyalinda maeneo yote ya kilimo, kwani ardhi tuliyokua nayo ni ndogo na haiongezeki, lakini watumiaji wao ndio wanaoongezeka.

Mhe. Spika, pia, serikali tunaiomba kuongeza wigo kwa ruzuku ya mbolea na pembejeo kwa mazao yote ili kuwahamasisha wakulima kuongeza kilimo na kupunguza nakisi ya uagizaji vyakula kutoka nje ya Zanzibar. Pia, tunamtaka waziri akija atueleze ni mafanikio gani yamepatikana tangu kuanza kuitumia mbegu ile inayoweza kuota sehemu za juu zenye miinuko isiyotegemea mvua, yaani Nerika.

Mhe. Spika, vile vile, iko haja ya kuimarisha kilimo cha mboga mboga kwani hapa Zanzibar kuna soko kubwa kwenye mahoteli ya kitalii ambayo siku hadi siku yamekua yakiongezeka hapa nchini.

Mhe Spika, vile vile, tunaipongeza serikali yetu kwa kuendelea kuimarisha zao la karafuu kwa kuongeza bei kwani hivi sasa wananchi wanafaidika na bei hiyo kwa kuinua kipato chao na kujikomboa kwenye wimbi la umaskini.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo tunaitaka serikali kutoa elimu kwa wakulima wa karafuu hasa katika kisiwa cha Pemba kuweka pesa zao benki kwa usalama wao ili kupusha kupata hasara pale itakapotokea majanga yeyote, kwani kwa mwaka uliopita Pemba peke yake zilinunuliwa karafuu zaidi ya shilingi bilioni 63, lakini pesa hizo hazionekani kuwekwa benki wakati kwa upande wa Unguja zilinunuliwa karafuu kiasi cha shilingi bilioni saba, lakini asilimia kubwa zimewekwa benki ya Zanzibar na wauzaji wa arafuu.

Mhe. Spika, kwani umuhimu wa kuweka pesa benki ni mkubwa kwao kwani pesa hizo zinakua salama, lakini pia, zinamfanya aliyeweka pesa hizo kuweza kuaminika na benki na kuweza kuomba mkopo yeye mwenyewe aidha wakati wa msimu mpya wa kuchuma karafuu au kujenga nyumba au kuanzisha biashara nyengine, kwani bei za mazao duniani hupanda na kushuka kila mara.

Mhe. Spika, moja katika jambo ambalo huchangia sana umaskini hapa Zanzibar, ni upatikanaji wa makaazi bora jambo ambalo mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, Marehemu Mzee Karume alitujengea nyumba bora za kuishi wananchi wake na hadi leo tunajivunia maendeleo hayo, lakini kitu cha kushangaza Tume ya Mipango katika vipaumbele vya mwaka huu wa fedha haikutuelezea chochote kuhusu serikali yetu kuendeleza azma ya kuwapatia wananchi wetu makaazi bora.

Mhe.Spika, kwa hiyo, Kamati yangu inaishari serikali katika vipaumbele vya mwakani, basi suala la ujenzi wa nyumba za makaazi kwa wananchi wetu, basi liwemo katika vipaumbele, kwenye bajeti yetu, kwani ukiangalia Mataifa yote yaliyoendelea duniani, basi wamehamasisha Makampuni mbali mbali ya binafsi na pia serikali zenyewe wameanzisha Makampuni ya Ujenzi wa nyumba (*Real estate*) na aidha kuwauzia au kuwakodisha wananchi au Makampuni na kuweza kujenga miji yao katika ubora na mpangilio maalum na kuifanya miji yao kuvutia, naamini serikali yetu ni sikivu italishughulikia suala hilo na hili likitekelezwa litasaidia hata kupunguza udokozi serikalini.

Mhe. Spika, sekta ya uvuvi ni moja katika sekta muhimu ya kiuchumi, ambayo bado hatujaitumia vizuri sekta hii ingeweza kutoa ajira nyingi kwa wananchi wetu, tungeliweza kuanzisha uvuvi wa bahari kuu ili kuweza kuuza samaki nje na kuanzisha viwanda vya kusindika samaki hapa Zanzibar, ili kuongeza ajira na kodi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, lakini pia, Kamati yangu imeanza kuona dalili ya kuanza kudorora kwa ile hamasa ya kuimarisha wavuvi wadogo wadogo kupitia iliyokuwa miradi ya *Macemp* ambapo wavuvi walikuwa hupatiwa maboti, nyavu, *mafreezer* na zana nyengine za uvuvi, lakini tunaona ile kasi imeanza kupungua kulikoni?

Mhe. Spika, Kamati yangu imesikitishwa sana na taarifa kutoka Tume ya mipango iliyoelezea kuwa zile boti kubwa za uvuvi tulizotegemea zingeliweza kununuliwa katika bajeti iliyopita ili kuja kutoa mafunzo kwa vijana wetu kuweza kutumia uvuvi wa kisasa na wa maji makubwa hadi leo boti zile hazijanunuliwa, kutokana na umakini mdogo wa viongozi wa Wizara ya Uvuvi ambapo tuliwahi kuambiwa kuwa aliekuwa Waziri wa Uvuvi kipindi kilichopita alikwenda kuona aina ya boti hizo, lakini kukatokea sintafahamu hadi leo hazijanunuliwa wakati pesa zipo.

Mhe. Spika, kwa hiyo, Kamati yangu tunakutaka Waziri wa Fedha kusimamia ununuzi wa boti hizo ili kukamilisha lile lengo lililokusudiwa na serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa taaluma kwa vijana wetu katika sekta ya uvuvi.

Mhe. Spika, pamoja ya kuwa serikali imeimarisha sekta ya fedha hapa Zanzibar, lakini bado haijaweza kuchukua nafasi kubwa hasa kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati, kwani mabenki mengi yaliyopo hapa Zanzibar ni matawi tu. Kwa hiyo, maamuzi makubwa huwa hayafanywi hapa.

Mhe. Spika, pia, bado riba iko juu sana ambayo badala ya kumsaidia myonge, basi mikato hiyo ya riba huwaneemesha zaidi wamiliki wa mabenki na kuwaacha wananchi na madeni makubwa ya muda mrefu. Kwa hiyo, tunaomba serikali kuzungumza na mabenki kupunguza riba hasa kwa watumishi wa umma kwani mikopo yao iko salama sana kupitia ajira zao. Kwa hiyo, sio sahihi kulipishwa riba sawa na wale wasiokuwa na dhama na ya utumishi wao.

Mhe. Spika, pia, Wazanzibari wanakosa fursa za kushiriki katika minada ya soko la hisa jambo ambalo lingeliweza kuogezwa wigo wa biashara kupitia soko la hisa. Kwa hiyo, iko haja ya serikali kuhamasisha shughuli kama hiyo ya uuzaji wa hisa kufanyika na hapa Zanzibar kama inavyofanyika kule Tanzania Bara.

Mhe. Spika, kwa upande wa Tanzania Bara, serikali wametoa mtaji wa kuanzishwa Benki ya Uwekezaji (*Tanzania Bank Investment*), benki ambayo imeweza kuwasaidia sana wafanyabiashara wakubwa na wa kati kuimarisha biashara zao, iko haja na hapa kwetu kuwa na chombo kama hicho.

Mhe. Spika, pia, kwa upande wa Tanzania Bara, mabenki yamekua na utaratibu wa kutoa mafunzo ya wateja wake wajasiriamali wadogo wadogo ili kujifunza kuingia kwenye masoko ya biashara na kuimarisha biashara zao, tunayaomba na mabenki ya hapa kwetu kuanzisha mfumo huo ili kuwajenga wajasiriamali ili baadae waje kuwa wawekezaji wakubwa.

Mhe. Spika, pia, napenda kurejea kauli yangu ya kila mwaka kuitaka serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha benki ya kinamama ambayo itakuwa ndio kichocheo kwa kinamama kujiimarisha kiuchumi kwani ukimuwezesha mama katika uwekezaji, basi umeisaidia familia.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna kinamama wengi wajane ambao wanalea watoto wao katika mazingira magumu sana, kwani wanashindwa hata kumudu kuwanunulia sare za skuli na mahitaji mengine watoto hao, mlo wa siku hadi kufikia kuwapa biashara watoto wao ili wakauze ili wapate mahitaji ya lazima ikiwemo chakula, wengine hufikia pahala watoto hao wanakwenda maskuli bila ya hata kupata chai na wakati mwingine hata wakirudi nyumbani pia hukosa chakula cha mchana.

Mhe. Spika, hii sio hali nzuri kwani hao watoto wetu ndio Taifa letu na viongozi wetu wa leo na kesho, lakini tukiweza kuwawezesha kinamama, basi hakika hakuna mtoto atakaenda skuli na njaa. Kwa hiyo, tunaitaka serikali kutoa mtaji ili kuwawezesha kinamama kufaidika na huduma za mikopo na uwezejishaji kwenye benki hizo. Nadhani serikali ingelitoa asilimia hamsini ya kuanzisha mtaji wa benki hiyo na asilimia zilizobaki zingelitangazwa hisa ili watu wajitokeze kuweza kununua hisa hizo. Ninaamini wapo Wazanzibari wengi wa ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar ikiwemo Uingereza, Marekani, Asia na Falme za Kiarabu waneliweza kununua hisa hizo.

Mhe. Spika, naamini hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wengi wetu tutakua tayari kununua hisa hizo ili na sisi kushiriki katika kukeza na kuwawezesha kinamama zetu hawa wazuri wa kizanzibari. Kwani hii pia ni sehemu ya uwekezaji?

Mhe. Spika, katika kuimarisha sekta ya fedha tunaipongeza serikali yetu kwa kufungua milango kwa wananchi kushiriki katika uwekezaji kwenye sekta mbali mbali za fedha mijini na vijijini kupitia mitandao ya simu za mkononi ikiwemo Tigo Pesa, Voda Pesa, Easy Pesa, Airtel Money na kadhalika.

Mhe. Spika, sekta hii imekua kwa kasi sana na imeweza kutoa ajira nyingi kwa vijana wengi mijini na vijijini, lakini jitihada zaidi za elimu zitolewe hasa kwa wananchi vijijini kuweka pesa zao benki, kwani ukiacha kuwa pesa zao zitakua salama, lakini pia, kuweza kuzitumia vizuri huduma za kibenki ambazo zitamjengea msingi mzuri wakati atakapohitaji mkopo kupitia benki hizo.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa kupunguza umaskini Zanzibar, yaani Mkuza 2 Serikali kupitia *klasta* ya kuimarisha huduma za jamii. Tunaishukuru serikali yetu kwa kuimarisha huduma za afya hasa kufanikiwa kutokomeza maradhi ya malaria, lakini tusijibweteke na hilo, basi serikali kuendelea kutafuta fedha ili kuendeleza upigaji wa dawa majumbani na kwenye madimbwi ya maji, lakini pia, kulitafutia mukelezaji eneo la mbele ya Bwawani Hoteli pale, ni sehemu kubwa ya uzalishaji wa mbu mjini Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile, tunaitaka serikali yetu kukiimarisha chuo cha afya cha Mbweni kwa kukipatia vifaa vya kisasa chuo hicho ili kuwaandaa vijana wetu kuja kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia, tunaipongeza serikali yetu kwa kuboresha maslahi ya madaktari wetu ili kurudi Zanzibar kuja kufanyakazi mara tu baada ya kumaliza masomo yao, pamoja na hayo tunautaka uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha madaktari wanakuwepo muda wote Hospitalini hapo kwani Hospitali inakosa pesa nyingi za huduma za Bima ya Afya kwani wagonjwa wakija huwa hawawakuti madaktari au kukosa dawa wanazohitaji leo ni aibu kubwa Hospitali ya Binafsi ya Al-Rahma eti.

Mhe. Spika, leo ndio inayoongoza kwa kuingiza mapato makubwa kupitia Bima ya Afya, kwa mwaka unaomalizika waliweza kulipwa na mfuko wa Bima ya Afya zaidi ya 1.2 bilioni wakati Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ambayo ndio ya rufaa ilipata pesa chache sana kiasi cha shilingi 250,000,000/=, walizolipwa na mfuko huo wa Bima ya Afya.

Mhe. Spika, hii ni kutokana kukosekana na kwa huduma wakati wote, wakati madaktari wengi wanaofanyakazi katika Hospitali ya Al-Rahma, ndio hao hao wanaofanya kazi wanaotoka Mnazi Mmoja, lakini isitoshe hata hao wagonjwa wanaoshindikana kwenye Hospitali binafsi, basi hupelekwa huko huko Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa matibabu zaidi.

Mhe. Spika, Kamati yangu haijaridhika hata kidogo na vipaumbele vya wizara ya afya katika bajeti hii kwani suala la ununuzi wa mashine ya *DNA* kwao haikua kipaumbele, tena cha kushangaza wizara imeshindwa hata kuheshimu maazimio yaliyopitishwa na Baraza lako tukufu la Wawakilishi kwenye kikao kilichopita kuunga mkono hoja binafsi inayohusu udhalilishaji wa watoto iliyoletwa na Mheshimiwa makini ambae pia, ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Mhe. Mgeni Hassan Juma ambaye pia, Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia wizara hiyo ya afya kwa kuitaka serikali kununua mashine hiyo ya *DNA* ili kuweza kupata ushahidi wa vinasaba, yaani *DNA* kwa watoto wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Mhe. Spika, kwa hiyo, Kamati yangu haikubaliani na hilo na inaitaka serikali kupitia Tume ya Mipango kurekebisha vipaumbele vya Wizara ya Afya na kuweka ununuzi wa Mashine ya *DNA* na kupunguza pesa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kununulia mashine hiyo ya *DNA*.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi tumeshachoka na vitendo vya udhalilishaji wanavyofanyiwa watoto wetu bila ya serikali kuchukua hatua za kisheria, eti kwa sababu hakuna ushahidi wa vinasaba, yaani *DNA*. Tunasema serikali ipunguze fedha kwenye mfuko mkuu wa serikali ili kununulia mashine hiyo ya *DNA* ili kuwaonyesha wananchi na ulimwengu kuwa na nyinyi mnachukizwa na udhalilishaji wa watoto wetu, suala hili ni muhimu hasa katika nchi inayoheshimu utawala bora na pia inayojali watoto wao jambo ambalo ndio Taifa la kesho.

Mhe. Spika, hatuwezi kuwa na Taifa la baadae lenye idadi kubwa ya vijana walioathiriwa kisaikologia kwa kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji walipokuwa watoto wadogo, jambo ambalo linaweza hata kuwaharibia maisha yao ya hapo baadae. Naamini Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu tutaungana sote kwa pamoja kuhakikisha tunapiga vita udhalilishwaji wa watoto katika bajeti hii.

Mhe. Spika, sekta ya maji pamoja na jitihada za serikali kusambaza maji mijini na vijijini, lakini mkazo mkubwa kwa sasa uwekwe mjini, kwani zaidi ya asilimia ya 45 ya wakaazi wote wa Zanzibar wako hapa mjini. Kwa hiyo, bado tunatumia pesa nyingi kununulia huduma za maji na pia muda mwingi kinamama kuutumia kutafuta maji na wakati mwingi wanakuwa hawana uhakika wa kupata maji ya uhakika.

Mhe. Spika, serikali kila siku imekuwa ikituambia tatizo la maji mjini litamalizika mwaka huu wa fedha, lakini hatuoni matokeo yake, sasa tunaitaka serikali kulimaliza tatizo la maji hapa mjini, kwani mji bila ya maji, basi ni uchafu na maradhi, lakini pia, tatizo la maji limekuwa likiwazidishia wananchi wetu umasikini wa kipato, kwani hutumia pesa nyingi kununulia maji na kinamama hupoteza muda wao mwingi kwenda kutafuta maji ya matumizi ya nyumbani.

Mhe. Spika, kwa upande wa elimu tunashukuru jitihada za serikali kuendelea kutusaidia majimboni pale tunapojenga madarasa kwani wizara huja kutuunga mkono kwa kuyamaliza madarasa hayo. Pia, tunapongeza jitihada za serikali kwa kujenga Skuli za Sekondari kila wilaya ambapo na mimi jimbo langu la Kwamtipura tumeweza kujengewa skuli hiyo, lakini cha kusikitika kwa jina iliyopewa skuli hiyo, eti kuiita jina la *“Faraja Sekondary School”*.

Mhe. Spika, kwa kweli hatukuridhika skuli ile kuitwa jina lile kwani zile jitihada za kumshawishi aliyekuwa Waziri wa Elimu wakati huo tulipomba kujengewa skuli hiyo, tuliomba kwa jina la Kwamtipura na ndio asili yake. Pia, kuweka Historia isipotee, lakini cha kusikitisha leo, eti inaitwa Faraja, sijui jina lile limetoka wapi?

Mhe. Spika, tunaitaka skuli yetu irejeshewe jina lake la asili la kuitwa Skuli ya Sekondari ya Kwamtipura, pamoja na hayo bado serikali yetu iangalie maslahi ya kwa Walimu Wakuu hasa wa *primary*, walimu wetu kwani wana posho shilingi elfu 20 kwa mwezi haistahiki kumlipa mwalimu hasa kwa kazi kubwa ya kusomesha watoto wetu na pia kuwalea watoto wetu. Tunaomba kwenye skuli zetu vitiwe vifaa vya maabara ili kuwaandaa watoto wetu katika karne hii ya Sayansi na Teknologia.

Mhe. Spika, katika klasta hii ya pili, kuimarisha miundombinu ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini, klasta hii bado imekabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo kuchelewa kwa miradi mikubwa ya miundombinu kwa mfano mradi mkubwa wa kuboresha miji yetu, yaani *ZUSP*. Mradi huu tangu umeasisiwa, sasa ni zaidi ya miaka minne bado unasuasua, haujaanza kazi ambapo tulitegemea ukimalizika mradi huu unaohusu ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji machafu kuelekea baharini, ambapo jimbo langu la Kwamtipura lingeliweza kufaidika na mradi huo ambapo mtaro unaotoka Darajabovu kupitia Shaurimoyo hadi Saateni ungeliveza kujengwa.

Mhe. Spika, lakini cha kusikitisha kila siku mradi huu unajengwa kwa maneno tu, wananchi sasa hawataki maneno, bali wanataka vitendo.

Mhe. Spika, miradi kama hii kila siku zikienda, basi gharama za vifaa vya ujenzi huwa zinaongezeka na baadae mzigo wote huo wa gharama linakua deni la Taifa, mzigo wote huu unawaelekea wananchi wetu. Kwa hiyo, wakati ukifika tunamuomba Waziri wa Fedha kuja kutoa maelezo ni hatua gani hadi sasa mradi huu umeshafikia. Kwani wananchi wengi hasa wa ng'ambo, huathirika sana na kuingiliwa na maji ya mvua kwenye majumba yao wakati wa mvua kubwa unaosababishwa na ujenzi holela na pia mji yetu kutokua na miundombinu ya kutolea maji machafu wakati wa mvua.

Mhe. Spika, huwezi kuzungumzia suala ya maendeleo bila ya kuhusisha na masuala ya mzingira, kwani kila mradi wa maendeleo kwa kiasi fulani ni lazima athari za uharibifu wa mazingira zitajitokeza. Kwa hiyo, ni lazima kila mradi utakaofikiwa kufanywa hapa Zanzibar, basi lazima litengwe fungu maalum la kuhifadhi mazingira ili kudhibiti uharibifu wowote wa mazingira utakaokuja kujitokeza hapo baadae na ingawa miradi yote mikubwa ya serikali linakuwemo fungu la kuhifadhi mazingira.

Mhe. Spika, lakini fedha zake zinakuwa hazipatikani na mara nyingi miradi hiyo baada ya kumalizika huacha athari kubwa ya mazingira jambo ambalo huliacha Taifa kwenye uharibifu mkubwa wa mazingira hasa kwenye miradi ya ujenzi wa barabara wajenzi huacha mashimo makubwa baada ya mradi kumalizika. Kwa hiyo, tunaomba serikali kuhakikisha miradi yote mikubwa kabla ya kuanza kwanza kufanyiwa tathmini ya mazingira na kusimamiwa ipasavyo wakati wa utekelezaji wake na kulipiwa fidia ya mazingira baada ya kumalizika miradi.

Mhe. Spika, nadhani hivi sasa marekebisho ya sheria ya mazingira iko tayari, basi tunaomba serikali sheria hiyo iletwe Barazani ili tuipitishie ili kuweza kusimamia majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, halikadhalika ujenzi holela usiofuata sheria unaoendelea kujengwa karibu na fukwe za bahari unaendelea kuharibu mazingira kwa kiasi kikubwa na athari yake huonekana kwenye maeneo mengine, kwani

hupelekea bahari kumega baadhi ya maeneo ya nchi kavu na kusababisha athari kubwa kwa watu wengine, kwani tumeshuhudia maeneo mengi kwa hivi sasa kuliwa na bahari na yanaingia maji chumvi wakati katika miaka ya nyuma maeneo hayo yalikuwa wananchi wakilima, aidha mpunga au mazao mengine, jambo ambalo hupelekea umasikini mkubwa kwa watu wetu waliokuwa wakitegemea mazao ya kilimo katika maeneo yale.

Mhe. Spika, kwa hiyo, ili kuzuia hali hii isiendele, basi ni vyema Idara ya Mazingira tukaweza kuipa meno zaidi ya kisheria ili iweze kutoa adhabu kali kwa mtu au taasisi yeyote itakayokiuka sheria au masharti ya uhifadhi wa mazingira.

Mhe. Spika, vile vile, ukataji wa miti ovyo bila ya kupata vibali sehemu husika, hivi sasa limekua ni jambo la kawaida katika jamii yetu na hakuna mtu anaechukua jukumu la kuisadia serikali kukemea jambo hilo. Hivi sasa vianzio vingi vya maji vimeanza kukauka kutokana kukatwa miti ovyo, lakini pia, kupelekea ongezeko la joto hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, lakini hata kuathiri wakulima kwa kukatiwa miti yao bila ya ridhaa yao, hii ni hatari kubwa kwa Taifa letu kama hatua madhubuti hazikuchukuliwa ili kuzuia hali hii isiendele, basi visiwa vyetu hivi vitaweza kupata matatizo makubwa ya kukosa miti ya kutosha na kusababisha ongezeko la joto nchini na ukosefu wa vianzio vya maji.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka niungane na Mhe Waziri wa Fedha kwa kuungana na wananchi wenzetu wa Afrika Kusini kumkumbuka kipenzi cha wengi ndugu yetu, mzee wetu Marehemu Nelson Mandela aliekuwa Rais wa mwanzo mweusi baada kumaliza utawala wa kidhalimu wa Wazungu Makaburu wa kule Afrika Kusini aliyefariki dunia tarehe 05 Disemba, 2013. Kwa kweli ametuachia pengo kubwa katika Bara zima la Afrika na Dunia, hatuwezi kumsahau kwa jinsi alivyojitolea sehemu kubwa ya maisha yake kupambana na ubaguzi wa rangi, jinsia, ukabila, udini na kuwa kielelezo kikubwa duniani kwa kuwa mpigania haki za wanyonge kwa muda wote wa maisha yake.

Mhe. Spika, lakini sio hivyo tu, bali alikua ni mtu wa kusamehe wote waliomkosea na kujaribu kujenga umoja pale alipohisi kuna dalili za mgawanyiko, yeye aliweza kutumia uwezo wake wote ili kuleta umoja na aliuonyesha ulimwengu kuwa yeye sie mtu wa kulipa visasi, kwani alipoachiwa tu kutoka gerezeni anakuwa Rais wa kwanza mweusi kule Afrika Kusini.

Mhe. Spika, basi jambo la mwanzo alitangaza kuwasamehe wale wote waliomkosea na pia kuunda Tume ya kusamehe na maridhiano ili kuondoa madukuduku na chuki miongoni mwa jamii ya Afrika Kusini iliyokuwa na matabaka makubwa mawili ya watawala weupe na watawaliwa weusi, hadi leo yeye ameondoka na kuliacha Taifa la Afrika Kusini likiwa huru lenye umoja, mshikamano, upendo na amani.

Mhe. Spika, kwa hiyo, basi tunawaomba viongozi wetu hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla hasa wa kisiasa, kukaa pamoja kama kuna makoseo yeyote, basi kuombana radhi na kusameheana na kutuongoza vyema Wazanzibari na Watanzania kwa jumla ili kwenda kuimaliza vyema mchakato wa Katiba ngwe iliyobaki, kwani wananchi wetu ni wanyonge, wanatuangalia sisi viongozi wao tutawavusha vipi kwenye hatua iliyobakia ya mchakato huo.

Mhe. Spika, naomba sana wananchi wetu ni wanyonge na maskini za Mungu mifarakano yetu ndio mauti yao na umoja wetu ndio neema na faraja na mafanikio yao, basi kwa sote tumlani shetani na turudi kwa Mola wetu ili tuendeleze umoja wetu tuelewane na tushirikiane, ili tuwaletee neema masikini za Mungu wananchi wetu. *Yaarabi* Mwenyezi Mungu Mtukufu tujaalie nchi yetu iwe na amani, upendo, mshikamano na maelewano ili kuwaletea wananchi wetu maendeleo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Wenyevit, naomba sote Wazanzibari kwa pamoja tuungane na wazazi na wananchi wote wa Nigeria kwa mtihani mkubwa wa watoto wao kutekwa na Kundi la Boko Haram. Tumuombe Mwenyezi Mungu kuwalinda watoto wetu hao wasidhuriwe na watekanyara hao na Mwenyezi Mungu awajaalie waachiwe huru wote wakiwa salama, wazima na wenye afya njema ili kurudi nyumbani kwao kuungana na familia zao.

Mhe. Spika, kwani watoto hao walikua wakitekeleza wajibu wao wa kutafuta elimu kama Mwenyezi Mungu alivyotuagiza kutafuta elimu popote duniani na tunawaomba wazee wa watoto hao Mwenyezi Mungu awape subra.

Mhe. Spika, baada ya hayo ninaamini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepata nafasi kubwa ya kuzisoma hotuba zote mbili za Mawaziri wa Mipango ya Maendeleo na Waziri wa Fedha kwa Makadirio na Mapendekezo na Matumizi ya Serikali yetu ya SMZ, wataichangia bajeti hii kwa umakini mkubwa, wataiboresha, wataikosoa kwa busara pale itakapobidi na pia wataishauri vizuri serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar, ili kuibua vianzio vipya vya mapato na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wetu wa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba hii *paragraph* ya mwisho niache kwa sababu nataka moja kwa moja niingie katika kitabu cha pili cha Mhe. Waziri na pia nitaomba uniruhusu kunywa maji.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yako ya Wenyeviti, naomba niwashukuru makatibu wetu wa Kamati, Bi Nasra Salmin Awaadh na Khamis Hamad Haji kwa kunisaidia kuandika hotuba hii na kuifanyia masahihisho pale nilipokosea na hatimae kuichapa na kuweza leo kuiwasilisha hapa Barazani kwa kweli ilikuwa sio kazi rahisi ni kazi kubwa imenichukua karibu siku tatu nilizikimbia familia zangu ili nipate utulivu kuweza kuwasilisha hapa Barazani.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi la Zanzibar kwa mara nyengine tena nnakushukuru kwa kunivumilia na kunisikiliza, kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati zako za Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura nawashukuruni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa baada ya maboresho ya bajeti hii, naomba tuiptishe kwa pamoja ili tumpae nafasi Mhe Waziri wa Fedha akatutafutie pesa ili kuwalata maendeleo wananchi wetu. Ahsante sana.

**RIPOTI YA KAMATI YA WENYEVITI WA KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MPANGO
WA MAENDELEO NA BAJETI
YA SERIKALI KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe Spika, kwa mara nyengine tena napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii ya kuichambua hotuba ya bajeti ya serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha wa Zanzibar.

Mhe Spika, kwa kuokoa muda naomba kuwapongeza kwa mara nyengine tena viongozi wote niliwapongeza hapo mwanzo kwenye hotuba yangu iliyochambua Mipango ya Maendeleo iliyowasilishwa na Waziri wa Mipango.

Mhe Spika, Kamati yangu baada ya kuipitia hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali ya mapato na matumizi ya mwaka unaokuja 2014/15, imeona kuwa kuna maendeleo ya kiasi yaliyopatikana kwa nchi yetu ingawa bado kipato cha mwananchi wetu bado hakitoshelezi mahitaji yao ya lazima ya kila siku, hasa watumishi wa Serikali kutokana na kiwango kidogo cha Mshahara wanachokipata.

Mhe Spika, Mhe Waziri wa Fedha ametueleza kuwa kwa mwaka ujao mfumko wa bei utaongezeka kwa tarakimu moja kulinganisha na mwaka uliopita, hali hii kidogo inatia moyo, kwa kweli katika kipindi kirefu huko nyuma tulishuhudia bei za vyakula na mafuta zikipanda kila siku kukicha, lakini kwa mwaka uliopita tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa jitihada za serikali yetu kuweza kudhibiti hali hiyo. Kwa hiyo, tunaomba serikali kuendelea na jitihada hiyo ya kudhibiti mfumko wa bei ili kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wetu.

Mhe Spika, lakini pia, ni busara kuhakikisha bidhaa za kutosha zinaendelea kuwepo muda wote hapa nchini, lakini hasa kwa bidhaa za chakula ambazo ndio muhimu zaidi kuwepo kwa muda wote. Suala hili la kuwepo kwa vyakula vya kutosha limekuwa zaidi kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje jambo ambalo sio la kutegemea sana. Kwa hiyo, iko haja ya kuhakikisha tunaongeza uzalishaji wa vyakula nchini hasa kukuza kilimo cha mpunga, ndizi, viazi, majimbi, mahindi na mboga mboga zinazoota hapa Zanzibar, tukiweza kulimudu hili, basi pamoja na kipato kidogo wanachokipata kinaweza kuwasaidia kuwapunguzia makali ya maisha.

Mhe. Spika, tumeona kwenye hotuba aliyotuwasilishia Waziri wa Fedha imeelezea kuwa kiwango cha mishahara kwa mwaka huu hakitaongezwa, isipokua tu itazingatia kurekebisha maslahi ya wale watumishi ambao maslahi yao hayakuweza kuzingatiwa. Pia, wale ambao hadi leo hawajapatiwa nyongeza zao za mwaka uliopita. Maagizo ya

Kamati ni kwamba wale ambao hawajafanyiwa marekebisho ya mishahara yao, basi wafanyiwe na walipwe malimbikizo yao, kwani ilikuwa ni haki yao ya mwaka uliopita, vyenginevyo watakuwa tumewadhulumu haki zao. Naamini serikali itatekeleza ushauri huo wa Kamati.

Mhe. Spika, katika suala la mishahara ya watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tunaiomba serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Umma kuweka maposho maalum kwenye mishahara ya watu wenye ulemavu, kwani wao ukiacha matumizi ya lazima ya kila siku, basi wao wanahitaji matumizi ya ziada ya kila siku, pengine kununulia madawa au *lotion*, lakini vile vile, kuwalipa wasaidizi wao. Pia, udhaifu wa maumbile yao kuweza kufanya kazi nyengine za ziada za kuwaongezea kipato ili kujaza lile pengo lililobaki ili kumudu mahitaji yao.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Mhe. Waziri wa Fedha ametueleza kuwa mapato ya ndani yameongezeka kwa mwaka uliopita na matarajio makubwa ya kuongezeka kwa mapato hayo, lakini bado kuna mapato mengi ambayo moja kwa moja yanapotea hayaingii serikalini na badala yake, aidha, kwa udokozi au baadhi ya wakubwa waliomo serikalini kwa kutumia mamlaka yao waliopewa na Mhe. Rais hutumia mamlaka hayo kuingiza mengi ya mapato hayo mifukoni mwao na kidogo yaliyobaki huingizwa serikalini.

Mhe. Spika, kwa kuwa wanahisi hakuna mtu anayeweza kuwajibisha kutokana na aidha vigogo wanaowategemea serikalini, hadi hii leo wanaendelea kujinufaisha wao na familia zao. Nadhani huu ni ukiukwaji mkubwa wa maadili ya uongozi na utawala bora. Sasa wakati umefika kuhakikisha wadhalimu hao wanawajibika kwa maslahi ya umma.

Mhe. Spika, katika kudhibiti na kuongeza mapato ya serikali, basi tunaitaka serikali ihakikishe kuwa maeneo yote yanayotakiwa kutozwa kodi yanafanyiwa hivyo, ili kuimarisha mapato yetu, kwa mfano maeneo ya fukwe za bahari zilizojengwa jeti na hoteli, kuwasilishwa kwa Sheria ya Mtathmini (*Valuer*) wa nyumba ili kuhakikisha wanafanyiwa tathmini majeti yale na kuweza kuyapatia mapato serikali.

Mhe. Spika, aidha, Kamati yangu inaitaka serikali iimarisha vianzio vya mapato vilivyopo, kwa mfano kuwashajihisha wasanii kusajili sanaa zao ili kuwaongezea kipato wasanii wetu na pia serikali kupata kodi yake pamoja na maendeleo ya Taifa letu. Nadhani serikali ikijitahidi kusimamia katika eneo hili, basi itaongeza ajira kwa vijana wetu hasa wasanii.

Mhe. Spika, kwa mfano katika nchi za nje kama Marekani na nchi nyengine za Ulaya wasanii wamekua na heshima kubwa kwa Taifa lao, kwani wamewezeshwa na wanao kipato kikubwa na wamekuwa maarufu sana dunia nzima na baadhi yao wamekuwa mstari wa mbele kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, walemavu na hata kusaidia waathirika wa vita katika maeneo mbali mbali duniani. Sasa eneo hili ni muhimu sana tulipangie mikakati maalum ili liweze kuleta tija kwa Taifa letu.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mapato yetu na kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa na Wazanzibari waliopo nje (*DIASPORA*), kuwa zinaratibiwa vizuri ili kuweza kuwanufaisha wao na familia zao na pia kuleta tija kwa nchi yao, kwani ziko nchi za wenzetu mfano, Kenya, India na Srilanka, wamewatumia vyema *DIASPORA* wao kuwasimamia na kuchangia uchumi wa nchi yao.

Mhe. Spika, lakini na wao pia kuweza kujivunia matunda yao pale wanaporudi kutembelea nyumbani kutembelea nchi yao kwa kuona matunda ya michango yao, kwa mfano nchi ya Srilanka wameweza kutumia kodi inayotokana na pesa zinazotumwa na *DIASPORA* ya kodi yao na wameweza kujenga skuli mbali mbali ambazo zimeweza kuwasaidia wananchi wao maskini katika nchi yao.

Mhe. Spika, vile vile, Kamati yangu inaitaka serikali kuimarisha huduma za Hospitali zetu za mijini na vijijini, ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. *Paragraph* hii Mhe. Spika, nitaomba niiruke kwa sababu pia nilijaribu kuisoma katika Ripoti ya Mpango wa Maendeleo, lakini pia, naomba iingie katika *Hansard*.

Mhe. Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ambayo ndio kimbilio letu Wazanzibari sote ili Hospitali hii iweze kukidhi haja iliyokusudiwa kutoa huduma zilizokusudiwa, hii ni kutokana na kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja inapokea wagonjwa kidogo wanaotumia Bima ya Afya ukilinganisha na Hospitali ya Al-Rahma, wakati watendaji wanaotoa huduma katika Hospitali ya Al-Rahma miongoni mwao wanatoka Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, vile vile, endapo mgonjwa atakuwa katika hali mbaya wakati yupo katika Hospitali za watu binafsi, basi hupelekwa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, sasa leo inashangaza sana kusikia kuwa Hospitali yetu kuu ya Rufaa ya Mnazi Moja kuwa kwa mwaka unaomalizika iliweza kupata malipo ya milioni 250, kwa ajili ya malipo ya huduma waliyoitoa kwa kutoa huduma ya Bima ya Afya, wakati Hospitali binafsi ya Al-Rahma ambayo haina huduma za rufaa iliwezaje kupata zaidi ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya huduma za Bima ya Afya walizozitoa?

Mhe. Spika, hili ni jambo la ajabu na linaonyesha kuwa ni kiasi gani Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ilivyokuwa iko katika kiwango cha chini cha utoaji huduma kulinganisha na Hospitali binafsi. Kwa hiyo, Hospitali yetu hiyo imekosa mapato mengi kwa mwaka huu inabidi waongeze bidii katika huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Kamati yangu imebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali haziheshimu Sheria ya Fedha, Namba 12 ya mwaka 2005 pamoja na Sheria ya Manunuzi Namba 9 ya mwaka 2005, hususan kifungu cha 22(2)(d) cha Sheria ya Manunuzi kinachozungumzia, sababu za kutokuitisha zabuni endapo gharama ya zabuni hiyo ni kubwa kuliko bajeti ya makisio iliyopo, kwenda kinyume na kifungu hiki kunapelekea Taasisi nyingi za serikali kuwa na madeni yasioweza kulipika.

Mhe. Spika, miongoni mwa taasisi hizo ni Vikosi vya SMZ, kwa mfano kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2011/2012, Kikosi cha Valantia peke yake kinadaiwa jumla ya shilingi 252,625,000.00, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinadaiwa shilingi 120,631,000.00, lakini Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kinadaiwa shilingi 149,115,200.00, wakati madeni hayo yote wamekopwa kutoka kwa watu au Makampuni binafsi ili kuweza kukidhi mahitaji ya vikosi vyetu, kwa matumizi yao ya lazima na ya kila siku, vyenginevyo wangelishindwa kumudu kutekeleza majukumu yao ya kila siku ikiwemo usafiri na chakula pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, kwa hiyo, tunaitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha deni hilo linalipwa mara moja vyenginevyo vikosi vitaendelea kutumia *OC* tutakazozipitisha kwenye bajeti ya mwaka huu ili kuweza kulipia madeni hayo, jambo ambalo litaendelea kuanzisha deni jengine kila mwaka na matatizo yatakuwa yanaendelea badala ya kumalizika.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaitaka Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) ianzishe huduma ya kadi ya *VISA* na *Master Card* ili kuwa na wigo mpana wa kutoa huduma zake, jambo ambalo litapelekea kuipatia mapato zaidi na pia kuongeza faida kwa benki yetu, jambo ambalo litaweza pia kuiwezesha *PBZ* kulipa gawio kubwa serikalini na kuongeza mapato ya serikali, kwani wakianzisha huduma hii wataweza kuwavutia wateja wengi hasa wale wafanyabiashara wakubwa na ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia watu huwa hawatembea na mkoba wa pesa, bali hutembea na *VISA Card* au *Master Card* kwa ajili ya matumizi yao ya kibiashara au yale ya kawaida.

Mhe. Spika, Kamati yangu imebaini kuwa taasisi zinazokusanya mapato huwasilisha fedha zote katika Mfuko Mkuu wa Hazina, jambo hili hupelekea taasisi hizi kushindwa kutekeleza vyema majukumu yao kutokana na uhaba wa fedha wanaopatiwa, kwa mfano Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale huingiza fedha kupitia vianzio vyake mbali mbali ambapo kwa mujibu wa kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo cha mwaka 2012/2013 katika ukurasa wa 91, alieleza kuwa hadi kufikia Aprili, 2012 Idara hii iliweza kukusanya zaidi ya jumla ya shilingi 142,362,852.00 sawa na asilimia 84% na katika hotuba yake ya mwaka wa fedha 2013/2013.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 61, vile vile, alieleza kuwa kuanzia Julai hadi Juni, 2013 ilikusanya karibu shilingi 116,554,201.00 sawa na asilimia 56%. pamoja na makusanyo haya mazuri, idara hii baadhi ya vianzio vyake vya mapato ikiwemo Beit – el - Ajaib hayaridhishi hadi watendaji wa Ofisi hiyo kuhamishiwa sehemu nyengine kutokana na ubovu wa jengo hilo kwa ajili ya kulinda usalama wao. Kwa kuwa taasisi hizi hukusanya mapato na kwa kuwa serikali haina uwezo wa kutekeleza baadhi ya majukumu ya taasisi hizi.

Mhe. Spika, Kamati hii inashauri kuwa ni vyema taasisi kama hizi zikapatiwa asilimia fulani ya makusanyo yake ili ziweze kutekeleza changamoto zinazozikabili. Hiyo ni taasisi moja tu, lakini ziko nyingi mfano wa hizo na tunaomba taasisi kama hizo basi aidha zipangiwe utaratibu wa kupatia asilimia fulani, yaani *Retention* ili ziweze kujiimarisha na kujijengea uwezo wa kukusanya zaidi ili kuongeza mapato ya serikali.

Mhe.Spika, Kamati yangu inaitaka serikali ifuatilie kwa karibu ukusanyaji wa mapato kwa taasisi inazozipa Ruzuku kwa madhumuni ya kujipunguzia mzigo wa baadae na kwa zile taasisi ambazo zina uwezo wa kujitegemea au kujijendesha wenyewe, lakini pia, kuweza kuyafanya tathmini ya taasisi hizo kuweza kutumia ruzuku hizo ili kuweza kujijenga na kujitegemea na kutoa gawio kwa serikali hapo baadae, lakini pia, kuyafunga Mashirika yote yaliyoshindwa kujijendesha kwa faida na kuongeza mzigo serikalini.

Mhe.Spika, kwani kwa utaratibu wa sasa kila taasisi itapimwa kwa malengo yake na utekelezaji wa malengo yake kama hakuna tija, basi ni kuondoa mzigo huo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Wenyeviti una dakika 15 kumaliza hotuba hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi): Ahsante sana Mhe. Spika, tunaishukuru serikali yetu kwa kuendelea kutupatia pesa za Mfuko wa Jimbo, kwani pesa hizo huweza kutusaidia kutatua matatizo madogo madogo yanayowakabili wananchi wetu majimboni, ingawa pesa hizo mara nyingi huwa ni kidogo hazitoshi kumaliza matatizo kwenye majimbo yetu.

Mhe. Spika, lakini kutokana na uhaba wa mapato ya serikali yetu, tunaamini kila mapato yetu yatakapoongezeka, basi na pesa hizo zitaongezwa, lakini pia, Kamati yangu imebaini matatizo kidogo kwenye pesa hizo kutokana na kukosekana kwa marejesho ya matumizi ya pesa hizo, lakini bado kazi kubwa inafanywa majimboni kupitia pesa hizo.

Mhe. Spika, pamoja na hayo, Kamati yangu inawataka Waheshimiwa sote ambao hadi leo hatujarejesha matumizi ya pesa hizo, basi kuhakikisha kwamba kabla ya kumalizika bajeti hii kuhakikisha tunarejesha marejesho hayo yanapelekwa serikalini ili kupatiwa pesa nyengine. Pia, Kamati yangu inaitaka serikali kufanya tathmini ili kuona ni kwa kiasi gani pesa hizo zinatua matatizo kwenye majimbo yetu.

Mhe. Spika, pamoja na yote, Kamati yangu inaishukuru Tume ya Mipango inayoongozwa na mama yetu mchumi maarufu hapa Zanzibar Bi Amina kwa kukubali kulipeleka ombi letu la Wenyeviti kuliongeza fungu la Mfuko wa Jimbo kutoka shilingi milioni 15 hadi 20 kwa mwaka ujao wa fedha, jambo ambalo litaleta faraja kubwa kwa wananchi wetu majimboni na kuweza kutatua matatizo yanayowakabili.

Mhe Spika, pamoja na waziri kuliirifu Baraza lako tukufu kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani umeimarika katika mwaka huu wa fedha, lakini bado kuna mapato mengi ambayo yanavuja kwa njia moja au nyengine kwa baadhi ya watendaji kutia mifukoni mwao na wengine kupitia dhamana zao walizopewa na Mhe Rais, basi hutumia nafasi zao huchukua mapato makubwa kwa kujinufaisha wao na familia zao na kile kinachobaki kidogo ndio huingizwa kwenye mapato ya serikali bila ya kujali kwamba hiyo ni dhulma na kuliangamiza Taifa.

Mhe Spika, na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunajitahidi sana kuionesha serikali yetu, ni maeneo gani mapato yanavuja, lakini kwa bahati mbaya sana serikali imekua mbogo haijali na wao ndio huwa watetezi wakubwa kwa hao wanaofanya ubadhirifu huo.

Mhe Spika, hata hivyo, Kamati yangu inaiomba serikali kufanya utafiti kwa Taasisi zake za ukusanyaji wa mapato, kwa mfano Bodi ya Mapato Tanzania (TRA) hususan kwa upande wa Idara ya Forodha imeshindwa kufikia malengo yake kutokana na uingizaji mdogo wa mizigo (*import*). Hivyo, ni vyema ikajulikana ni sababu gani na ni bidhaa gani ambazo zimeingia kwa asilimia ndogo na kujua kilichosababishwa na uingiaji huo mdogo.

Mhe Spika, kwa kuwa serikali yetu hutegemea mapato yake kupitia ushuru wa bidhaa zinazolingia nchini, basi ni vyema kuboresha mazingira mazuri ili kuwavutia wafanyabiashara kuleta bidhaa zao hapa Zanzibar na kuongeza mapato.

Mhe. Spika, Kamati yangu imeona kuna umuhimu mkubwa wa kuzishirikisha Taasisi zote za Umma wakati wa kuandaa mipango ya nchi ili kupata ufanisi uliokusudiwa. Hii ni kutokana na kuwa endapo serikali itaamua mambo bila ya kushirikisha baadhi ya taasisi hasa zinazokusanya kodi, jambo hili hupelekea hasara kwa baadhi ya taasisi, kwa mfano maamuzi ya misamaha ya kodi kwa bidhaa zinazolingia nchini hupelekea Idara ya Forodha kushindwa kukusanya vyema katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kwa hiyo, ni vyema kabla ya kufanya maamuzi, basi kuwasiliana na wahusika wanaokusanya kodi ili kushauriana mapema kabla ya kufanya maamuzi hayo.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi nyingi duniani zimepata maendeleo ya haraka kutokana na kuwekeza katika sekta ya viwanda, sekta ambayo inazalisha bidhaa nyingi na kuweza kuuza nje ya nchi na kuingiza pesa za kigeni, lakini pia, hutoa ajira nyingi kwa vijana wao na kuinua pato la Taifa, nchi zote kubwa duniani zimeendelea kutokana na viwanda, kwa mfano China hivi sasa kila siku zikienda basi bidhaa za viwandani zinaongezeka kutokana na kuwekeza katika sekta ya viwanda na bado wanaendelea kujenga viwanda vyengine.

Mhe. Spika, kwa hiyo, hivi sasa tuandae mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza kwenye sekta ya viwanda ili kuongeza mapato yao, lakini kujiandaa na uwekezaji huo, basi ni busara kwana serikali kukaa pamoja na wawekezaji wa viwanda waliopo hapa nchini kwa sasa, ili kujua matatizo yanayowakabili wawekezaji hao kwa lengo la kuimarisha sekta hiyo. Kwa upande wa viwanda ambavyo vinazalisha ni vyema viwanda hivi vikajiimarisha zaidi ili viweze kusafirisha bidhaa zake nje ya Zanzibar japo katika soko la Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, Kamati yangu inawashauri wenye viwanda waliyopo hapa Zanzibar, kuwa na ‘*Marketing Strategies*’ zinazokwenda na wakati ili kuweza kumudu ushindani wa kibiashara uliopo pamoja na kuwa na Maafisa wa Masoko wenye uwezo wa kutosha kwa nia ya kuishauri Makampuni hayo ipasavyo ili hatimaye kufikia malengo yaliyokusudiwa, kwani tumeshuhudia bidhaa nyingi zinaingizwa humu nchini wakati bidhaa hizo huzalishwa hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati yangu imegundua kuna baadhi ya Makampuni yametia mikataba ya uwekezaji serikali, lakini wameshindwa kuheshimu makubaliano hayo na kufanya wanavyotaka wao, serikali inawaangalia tu, kwa mfano Kiwanda cha Soda Maruhubi hivi sasa kinafanyakazi kinyume na makubaliano na serikali, lakini vile vile. mmiliki wa Kiwanda cha *Cotex* Maruhubi wameyazuia maeneo makubwa ya Chumbuni na Karakana bila kufanyia shughuli yeyote ya kiuchumi kama ilivyokusudiwa na kuitia hasara serikali.

Mhe. Spika, Kamati yetu inaitaka serikali kuiangalia upya mikataba yote iliyokubaliana na wawekezaji kwenye maeneo mbali mbali ya uzalishaji na kuifuta ile yote itakayoonekana kuitia hasara serikali na hasa yale maeneo yaliyookaa bure kwa miaka mingi bila ya kuwepo na uzalishaji wa aina yoyote na kutafuta waliokuwa tayari kukeza ili kuongeza ajira na kipato kwa nchi yetu na pia kuweka makubaliano hayo kwa njia ya maandishi ili kuwa na uhakika wa matumizi bora na yenye tija kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, kama nilivyoieleza katika taarifa yetu ya uchambuzi wa mipango ya maendeleo, kuwa serikali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali inunue *machine* ya *DNA*. Hili sina haja ya kulirejea kwa sababu tayari nimeshalitaja.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Mhe. Waziri ametuelezea kuwa bajeti ya mwaka ujao itaongezeka kutoka shilingi bilioni 658.5 hadi kufikia shilingi bilioni 707, hali hii bado sio nzuri sana kwani ongezeko hilo zaidi linaenda kwenye mishahara, lakini bado kwenye matumizi mengine ya serikali, yaani *OC* bado hali itakua sio nzuri, kwani mahitaji halisi ya watendaji serikalini kwa mwaka uliopita hali haikua nzuri na kwa mwaka ujao bado hali haijatengamaa kama mahitaji halisi.

Mhe. Spika, hii hupelekea kuwapa wakati mgumu watendaji wetu wa serikali kufanya kazi chini ya uwezo wao kutokana na kupata pesa chini ya mahitaji yao. Kwa hiyo, inatubidi sisi Waheshimiwa kuweza kuishauri vyema serikali yetu kubuni vianzio vipya vya mapato na sio kuendelea kuvikamua hivyo vilivyopo. Kwa hiyo, bado ninaendelea tena kuwashauri wenzangu kupunguza siasa na tujelekeze zaidi kwenye kuimarisha mapato yetu ili kuinua uchumi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka uliopita Baraza lako tuliidhinisha ongezeko la kodi kwenye Ada ya Bandari ili kukusanya Bilioni mbili, lakini pesa hizo hazikuenda kutumika huko tulikokokusudia, tunaitaka serikali kuheshimu matumizi kama yalivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kununulia madawati.

Mhe. Spika, ingawa kwa mwaka huu hakuna ongezeko lolote la kodi, isipokuwa kwa wasafiri wa ndani watakao safari kupitia viwanja vya ndege na kuimarisha ukusanyaji kwa yale maeneo yaliyokuwa hayalipiwi kodi, lakini maeneo hayo bado ni machache na mapato yatakayopatikana hayatoshelezi mahitaji muhimu. Kwa hiyo, kwa mara nyengine tena naomba tuishauri vizuri serikali ili kupata vianzio vipya vyenye mapato makubwa.

Mhe. Spika, Kamati yangu pia inatoa shukurani zetu za dharti kwa kuifuta ada ya kulipia mitihani ya Kidato cha Sita, jambo ambalo litawasaidia sana wananchi wetu wanyonge kupungukiwa na mzigo wa ada hiyo na tunawataka vijana wetu waitumie vizuri msamaha huu waliopewa na serikali kwa kuongeza bidii katika masomo yao.

Mhe Spika, kamati inaungana na mkakati wa kuwaorodhesha na kuwakusanya walipakodi wote kwa kuimarisha hatua za kiutawala yaani *Block Management System* kwa utaratibu huu utaweza kuongeza wigo wa mapato ambayo hapo nyuma hayakuwa yakikusanywa, hasa kwenye nyumba bubu za wageni n.k.

Mhe. Spika: Dakika tano bado Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi): Dakika tano, ahsante Mhe. Spika, naamini nitamaliza. Mhe. Spika, lakini pia kuanzisha mkakati mpya wa kutumia Machine za kisasa za kutolea risiti kama walivyofanya wenzetu Tanzania Bara ambao wamefanikiwa kuongeza mapato yao serikalini, lakini ushauri wangu nadhani machine hizo zingelionesha bei halisi ya bidhaa ya kununuliwa bidhaa pamoja na kodi inayolipwa kama wanavyofanya wenzetu Marekani na hata kwa baadhi ya Mahoteli makubwa mfano kule nchini Uganda.

Mhe Spika, kamati yangu inaiomba Serikali yetu kuiharakisha na kuileta Barazani sheria ya *Local Government* kwani sheria hii itaongeza ufanisi kwa kuzipa mamlaka zaidi Serikali za Mitaa ili kuweza kubuni mipango na kuingia mikataba na taasisi mbali mbali za ndani na nje ili kuharakisha maendeleo kwenye sehemu zao bila ya kuisubiri Serikali kuu, hatua hii italeta mabadiliko makubwa kwenye halmashauri zetu na kuongeza mapato kwa nchi yetu na pia kupunguza kwa kiasi kikubwa matatizo katika maeneo yetu mbali mbali vijijini. Hatua hii pia halmashauri na mabaraza ya miji kuweza kuomba pesa moja kwa moja kutoka mfuko wa Barabara kwa kuboresha njia za ndani kwenye maeneo yetu mbali mbali kwa kuingia mikataba na makampuni binafsi ya ujenzi wa barabara.

Mhe Spika, kamati yangu kwa niaba ya wananchi wote wa Zanzibar tunaipongeza Serikali yetu kwa kupunguza ada ya mirathi kutoka asilimia 5 hadi 0.25, jambo hili litawasaidia sana wananchi kuweza kufanyiwa tathmini ya mali zao jambo ambalo hapo mwanzo lilikuwa likiwakimbiza wananchi wetu kwenda kufanyiwa tathmini hiyo kwa kukimbia ada kubwa iliyokuwa ikitozwa na idara hiyo. Kwa hiyo, tunaamini hivi sasa watu wengi watakwenda kuomba kufanyiwa tathmini za mali zao ili kuwawezesha kuingia kwenye mikataba au mikopo kupitia Mabenki, lakini vile vile kurasimisha mali zao kwa njia ya biashara.

Mhe Spika, pamoja ya kwamba Baraza lako tuliridhia mwaka uliopita kuwatoza kodi wajasiriamali wadogo wadogo mauzo yao yasiozidi milioni 10 kwa mwaka, nadhani Serikali kwanza ingelianza na hawa vigogo yaani wafanyabiashara wakubwa kwani huko ndiko mapato mengi yanakopotea.

Mhe Spika, tunaipongeza Serikali yetu kwa mwaka huu kuanza kutekeleza kilio chetu cha siku nyingi cha kufuatilia malipo kutoka kwenye makampuni ya simu kwani wao hutukata pesa nyingi kupitia matumizi makubwa ya simu tunayoyafanya kila siku. Jambo ambalo pia litaongeza mapato ya Serikali.

Mhe Spika, ingawa Mhe Waziri ameitaja kwa kifupi sekta ya umeme lakini eneo hili kwa sasa linawaumiza sana wananchi wetu kutokana na bei kubwa ya umeme ambayo inaendelea kuongezeka kila siku. Kwa hiyo pamoja na Serikali kutuelezea kuwa wanafanya utafiti wa kianzio kipya cha umeme wa upepo, lakini pia tujiandae na mipango bora na matayarisho ya Sera ya Gesi na Mafuta ambayo tunategemea si muda mrefu mara tu baada kumaliza mchakato wa katiba, nchi yetu itaweza kutafuta na kuzalisha Gesi kwa wingi ambayo yenyewe ni kianzio kikubwa cha kuzalisha umeme ambapo tunategemea nishati hiyo itapunguza sana bei ya umeme hapa Zanzibar na umeme mwengine kuweza kuuza nje ya Zanzibar. Kwa hiyo, tunasema nguo ya Ijumaa siku hizi hufuliwa Jumatano kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Spika, pia kwa kumalizia tunaipongeza Serikali yetu kwa kusikia kilio chetu cha kudhibiti upandaji wa bei ya mafuta ya Petroli na Diesel kila kukicha hapa nchini kwani kupanda kwa bidhaa hii pia husababisha bei za vitu vingine kupanda.

Mhe Spika, baada ya hayo naamini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mmepata nafasi kubwa za kuzisoma hotuba hizi mbili za Mawaziri wa Mipango wa maendeleo na pia Waziri wa Fedha kwa Makadirio na Mapendekezo Mapato na Matumizi ya Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar, wataichangia Bajeti hii kwa umakini mkubwa, wataiboresha, wataikosoa kwa busara na pale itakapobidi wataikosoa.

Pia wataishauri vizuri serikali yetu kuibua vianzio vipya vya mapato na kuleta maendeleo endelevu kwa nchi yetu na kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yako ya Wenyeviti naomba kuwashukuru Makatibu wetu wa Kamati Bi. Nasra Salmin Awadh na Ndugu Khamis Hamad Haji kwa kunisaidia kuandika hotuba hii na kuifanyia masahihisho pale nilipokosea hatimae kuichapa na kuweza leo kuwasilisha leo hapa Barazani. Kwa kweli ilikuwa sio kazi rahisi ni kazi kubwa imenichukuwa karibu siku tatu nilikimbia familia zangu ili nipate utulivu wa kuweza kuwasilisha vizuri hapa Barazani.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi la Zanzibar kwa mara nyengine tena nashukuru kwa kuweza kunivumulia na kunisikiliza. Kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura nawashukuruni sana kwa kuweza kunisikiliza.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti umetumia vyema muda wa kuwasilisha hotuba au ripoti ya Wenyeviti kwa hotuba zote mbili.

Sasa naomba nimkaribishe mchangiaji wa kwanza baada ya Mwenyekiti. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali ili nae achange.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kuneemesha meena kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo kwa kutupa afya na pumzi kwa kufika mbele yako na tukawa katika hali ya usalama kabisa, *alhamdulillah*.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii vile vile kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Uzini kuipongeza Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa bajeti nzuri iliyoleta matumaini kwa Zanzibar na vile vile ninaamini Waziri anaehusika na bajeti hii ambaye aliyotuletea, naamini mimi pamoja na wananchi wangu pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri na kwa imani kubwa kabisa waliokuwa wameifanya wakatuletea bajeti hii.

Vile vile, nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Fedha chini ya Taasisi zake zote ya *ZRB*, *TRA* na vyombo vyote vya ukusanyaji wa mapato katika sehemu mbali mbali kwa kazi nzuri na kwa sababu ya kuonesha jinsi gani wenzetu hawa kwa utaalumu wao na mashirikiano yao wameweza kufanya ubunifu wa kuweza kufanya pesa na kuvuka malengo kama mfano wa *ZRB* na sehemu nyengine katika kusaidia bajeti yetu hii. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nampongeza kwa dhati Waziri wa Fedha pamoja na wasaidizi wake wote.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha atupe ufafanuzi, nimepata kigugumizi kidogo Mhe. Spika. Kigugumizi kilichonikuta hiki cha Gazeti la Serikali la *Daily News* ilikuwa linatwambia pamoja na sisi Wawakilishi tulikuwa tumepewa elimu ya kuelezwa Waziri wa Muungano anasema Zanzibar tuliwapa bilioni 27.19 siku ya Jumanne Mei 13 kwa maana ya mwezi huu mwaka 2014.

Katika hizo bilioni 27 alitwambia kwamba ni msaada wa Muungano wa upande wa Zanzibar. Sasa kwa bahati nzuri Mbunge wa CCM ndani ya Jamhuri ya Muungano kutoka Zanzibar alisema kwa kuwa hizi pesa zilitajwa alitaka na sisi tuelimishwe. Maana yake mimi Mhe. Spika, nimefika darasa la 12. Kwa hivyo, alitaka tuelimishwe tuambiwe kwamba hizi pesa zilivyotolewa ili tufahamishwe na Wazanzibari wafahamishwe.

Mhe. Spika, fedha zilizotajwa humu ndani sizo pesa za msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu hapa pamezungumzwa *Phase I* bilioni 15, hizi ni pesa zetu wenyewe. Kwa bahati tu kwamba wenzetu wanapokea kwa niaba yetu na katika Bajeti ya Waziri wa Fedha *page 47* imeeleza humu. Sasa nilitaka kutoa tu ufafanuzi Mhe. Spika, si kweli kwamba Muungano umetupa msaada sisi Zanzibar bilioni 27. Ukweli ni kwamba bilioni 17.6 ni pesa zetu kwa ajili ya wafanyakazi wa Jamhuri wa Muungano wanaofanya kazi Zanzibar.

Kwa hivyo, kwa maana hizi pesa wametupokelea tu na kwa bahati nzuri Mhe. Spika, hotuba yangu ya mwaka jana ya Wizara ya Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee hizi pesa walizifanyia kazi walizuia mwanzo pesa zetu, hawakupaswa kuzuia hata siku moja, walizuia wakafanyia kazi zao ilibidi sisi tukapige kelele. Kuliundwa Kamati mwaka jana ya Waziri Mkuu na upande wa huku wa Zanzibar ili kupata hizi pesa zetu. Kwa hivyo, hizi pesa zetu sio kama tumepewa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hili mimi niliomba nisaidie na nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja hapa ku- *wind up* basi atufafanulie kwamba hiyo *phase I* ni pesa zetu au ni pesa ambazo tumepewa na Jamhuri ya Muungano. Naomba Mhe. Waziri wa Fedha akija atufafanulie.

La pili, kuna mchango huu wa wabunge tunaambiwa kwamba na Waziri wa Muungano kwamba kuna Wabunge wa Zanzibar kumeletwa pesa 1.2 bilioni hawa ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, hizi pesa si za msaada wala haikuja kwenye SMZ ni pesa za Muungano Wabunge wa Jamhuri ya Muungano Bara na Zanzibar. Kwa upande wa Zanzibar wako Wabunge wa Zanzibar ndio maana zikaletwa *share* zao huku.

Kwa hivyo, ninachoomba Mhe. Spika, ningeliomba Mhe. Waziri wa Fedha aje atwambie hapa hizi pesa zimeingia au zimepita tu hapa kuwapa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini zaidi kilichokuwa kimenisikitisha zaidi Mhe. Waziri wa Muungano pamoja na huyu Mbunge wa CCM kwa upande wa Zanzibar, anasema Serikali ya Muungano imeisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika miaka 50 ya sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu milioni 600, nzuri *alhamdulillah* lakini iliyosaidia ni Jamhuri ya Muungano.

Sasa atwambie Mhe. Waziri wa Muungano, Serikali ya Tanganyika ilikuwa na sherehe zake miaka 50 je, Serikali ya Muungano iliipa milioni mia ngapi Serikali ya Tanganyika au Serikali ya Tanzania Bara, kwa sababu kama ni Muungano wangetwambia na upande wa Tanzania Bara kama tulivyo sisi wamewapa ngapi? Mhe. Waziri wa Fedha kuna mambo mengi haya nimesema haya kwa sababu tumeambiwa na Mbunge huyu tuje tuelimishwe.

Sasa mimi kwa kuwa ufahamu wangu ni mdogo, kuwa mshamba si kuzaliwa kuwa mshamba ni kutokufahamu mambo. Kwa hivyo, mimi nilitaka ufafanuzi kwa upande wangu. Kwa hivyo, Mhe. Spika...

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe Serikali ya Tanganyika haipo.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Serikali ya Tanzania Bara.

Mhe. Spika: Serikali ya Tanzania Bara haipo.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Serikali ya Muungano. Sasa basi tungeambiwa kuwa hii Serikali ya Muungano tulikuwa na sherehe zimetoka ngapi na kama Serikali ya Muungano imetusaidia nini? Lakini Mhe. Spika, katika bajeti hii tuliyosoma mbele ya Waziri wa Fedha katuletea ningeliomba Mhe. Waziri wa Fedha atwambie Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetuchangia nini katika bajeti yetu sisi ya Zanzibar hii hapa, mimi humu sikuiyona kwa ufahamu wangu mdogo.

Mhe. Waziri wa Fedha aje atwambie kwamba humu kuna mchango wa Serikali ya Muungano kama Muungano lakini kama misaada ile ni *share* zetu ambazo hazipaswi kusemwa kwa sababu hizo ni *share* ambazo tumekubaliana.

Jengine Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri wa Fedha kwamba tunaelekea katika mwezi wa Ramadhani na kama tunaelekea katika mwezi wa Ramadhani nina hakika huko mbele kwa huruma za Rais wetu, mpendwa wetu, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hivyo ndivyo ninavyoamini kwamba huko mbele kutakuja msamaha kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba kuhusu chakula.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri wa Fedha panapotoka msamaha wa chakula Serikali itangaze rasmi kuwajulisha wananchi kwamba tunasamehe tende kwa mwezi huu, mchele, lengo la serikali ni kuwaondolea ukali wa maisha wananchi wa Zanzibar hasa kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Ningeliomba vile vile Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na sehemu nyengine wakae maana yake Mhe.Spika, sisi akina Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali kila tukipata msamaha tunaona hatutosheki tunataka kujiongezea faida tu. Kwa hivyo, ningeliomba kuweko na utaratibu maalum kwamba huu msamaha unaotoka ulengwe na wananchi wote ili wafaidike kuona kama kweli Serikali yao ni nzuri, inawapenda na inawajali wananchi Wazanzibari.

Kwa hivyo, kama kuna hilo litatokea basi Mhe. Waziri wa Fedha akae na wadau kuona jinsi gani chakula hiki kitakachokuja kitafikia walengwa bila kuweka mwezi wa Ramadhani ikimalizika halafu kije kuuzwa mara mbili. Kwa hiyo ninaona niizungumzie.

Mhe. Spika, lakini vilevile kwamba kazi tuliyokuwa nayo sisi Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri wa Fedha katika miradi mingi ambayo hii tuliyokuwa tunaitaka na tunaizungumza ni uzuri Mhe. Waziri wa Fedha akawa makini sana kwa miradi ile ya wananchi inayowagusa wakati anapotoa kusimamia kwamba miradi, ile inayotolewa pesa iwe inakwenda kwa walengwa au inakwenda katika miradi ambayo inawagusa wananchi katika kutelekeza ahadi ambazo ilikuwa imeshazungumzwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Hili limeshazungumzwa kwenye Bajeti, kwa hivyo ni uzuri vitu kama hivi vikasimamiwa kwa pamoja ili tukaona kwamba yale yote ambayo yamezungumzwa katika bajeti iliyopita yanatekelezwa katika njia inayofahamika.

Mhe. Spika, la mwisho katika kusisitiza hayo nimalizie kusema naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imani yangu na imani ya wenzangu baada ya kupata nafasi hii ya kuzungumza pamoja na bajeti hii na majibu ambayo ninaamini Waziri wa Fedha ni mtu ambaye namuheshimu sana na najua si mtu wa kutafuna tafuna maneno, pamoja na wasaidizi wake nafikiri masuala haya atakuja kwa uwazi kuyazungumza, ili atusaidie. Pia ningeliomba wenzetu hata kama gazeti hili la Serikali kwa kweli mimi lisingekuwa na jambo kama gazeti hili lisingeandikwa.

Nilipongeze gazeti la Serikali la Zanzibar leo, Gazeti la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hapa kuna picha ya Waziri, Katibu Mkuu haya yote hayakueleza humu yaliokuwemo. Kwa hivyo, mimi ninachoomba tu Mhe. Spika, atwambie na kama kuna uwezekano basi atwambie hiyo Kamati ya pamoja ya *account* ya Muungano atwambie imekusanya ngapi, Zanzibar tunadaiwa ngapi?

Mhe. Spika, baada ya majibu haya mimi Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Uzini pamoja na wananchi wangu naiunga mkono Wizara ya Fedha Bajeti yake baada ya majibu mazuri na naamini ndivyo yalivyo. Naunga mkono kwa asilimia mia na moja, ahsanteni. (*Makofi*)

Mhe.Spika: Tunakushukuru Mhe.Mohamedraza Hasanali Mohamedali. Wahesimiwa Wajumbe napenda nikumbushe tu kwamba, tunajadili hotuba zote mbili. Hotuba ya Hali ya Uchumi, na Mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini wakati huo huo Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Naomba sasa nimkaribishe Mheshimiwa Ali Salum Haji na baadae Mheshimiwa Ashura Sharif Ali. Mheshimiwa Ashura chukua nafasi.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezimungu Mtukufu aliyetujaalia uhai, na uzima akatuwezesha leo hii kukutana hapa tukiwa wazima, kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe Mheshimiwa Spika, kunipatia nami nafasi hii, ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika mengi katika mada iliyoko mezani wakati huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa aniwapongeze Mawaziri wote kwa Hotuba zao na kwa uwasillishaji wao. Na niwapongeze watendaji na watu wa Tume ya Mipango. Baada ya kuyasema hayo ya utangulizi wangu huo nianze na utangulizi ufuatao:-

Mheshimiwa Mzee Aboud Jumbe miaka ya 70 alileta khanga za aina tatu, na zote alizipatia majina. Yakwanza alisema “*mcheza kwao hutunzwa*”. Ya pili akasema “*kiumbe mzito*”; na ya tatu akasema “*maneno yawe mafupi vitendo viwe virefu*”.

Baada ya utangulizi wangu huo, sasa nataka niingie katika Bajeti hii. Mheshimiwa Spika, Wazanzibari wote kwa muda mrefu walikuwa masikio wazi, kutaka kuisikiliza serikali yao, imewapangia mipango gani ya maendeleo na wajenge matumaini gani katika kipindi cha mwaka 2014/2015 kiutendaji na utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo ya jamii ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, mimi kimtazamo wangu, niliangualia hii Bajeti, na hatimae kuweza kufanya dondoo mbali mbali, nikilinganisha Bajeti zetu mbali mbali. Vianzio vyetu vya mapato, nikaona uhalisia wa fedha ambazo zinapatikana na mipango yetu ambayo tunaipanga, haiendani kabisa na haya malengo tuliyojiwekea. Tunaizungumzia Bajeti ya Serikali maana yake shughuli ambazo tumezipanga ziweze kutekelezeka.

Mhe. Waziri wa Fedha ameniambia hapa kwamba ameongeza bajeti hii ya makisio yake lakini uhalisia anasema hivi. Uhalisia anasema kwamba ana mataarajio ya kukusanya jumla ya Tanzania shilingi 707.8 bilioni ambazo kuna ongezeko la silimia 7.5 ambapo kwa mwaka wa fedha uliomalizika alikusanya shilingi 658.5 milioni. Lakini uhakika wake wa fedha ambazo alizipata unaendelea chini.

Anasema alipata makusanyo ya shilingi 552.9 milioni. Huu ndio uhalisia. Mhe. Waziri wa Fedha, niseme kwamba niwapongeze kabisa watu wa Tume ya Mipango, Mipango wanayoipanga ni mizuri, kama inatekelezeka ni madhubuti na niimara. Na inapotekelezwa kweli, basi tunaweza tukafikiwa malengo. Lakini kimsingi ukiangualia hiki ambacho tumekishikilia mkononi kwa wakati huu, haya malengo tuliyojiwekea katika kipindi hiki cha mbele cha mwaka 2013/14, hayatekelezeki ndio ukweli.

Ninayasema haya kwa sababu nimeziangualia Bajeti za wizara mbali mbali wameshindwa kuingiza Kasma katika mafungu mbali mbali. Lakini kuna miraadi ya Serikali ambayo ilitaka itekelezwe. Mimi nimeona katika kitabu hiki cha kwanza kuna miradi mbali mbali humu, ambayo Serikali imeiwekea hivyo, lakini mpaka bajeti hii inasomwa inaambiwa haijapatiwa hata shilingi kumi. Mfano, kuna utekelezaji wa kifedha hapa. Kuna mradi huu wa kiwanja cha Ndege Pemba. Mpaka inafika leo hakukuingizwa hata shilingi. Kuna Mpigaduri, mpaka kufikia leo hakukuingizwa shilingi. Mlundikano wa miradi mingi, bila ya kuwa na fedha hususan, hatutaweza kuyafikia malengo. Na bajeti imesema wazi wazi, kwamba kinachoweza kupatikana ni mishahara tu, na hata hizo *OC* zenyewe hazikidhi haja.

Umefika wakati Serikali izungumzwe ukweli. Huwezi kushona nguo ambayo ukubwa wake anaweza kuvaa Mheshimiwa Mwinyihaji, ukamshonea Mheshimiwa Hija, haimtoshi kitambaa, ndio ukweli.

Haiwezekani kabisa, imefika wakati Serikali ijipange, ijiwekee vipaumbele ijigawie katika mpango madhubuti, Serikali itafute miradi mingapi, kama ni mitano basi iwe mitano kwa mwaka mmoja lakini miradi hiyo iweze kukamilika kwa wakati, kwa huu mwaka wa fedha ambao tumejipangia. Lakini tuna utitiri wa miradi ambayo ukiangualia haina kasma humu ndani. Unaambiwa mwaka huu hatukuingiziwa fedha, ukimuuliza mtendaji anasema sikuizingiziwa fedha. Sasa mimi najiuliza ikiwa utekelezaji wa serikali uko hali hii, jamani hiyo jamii yenyewe ya Wazanzibari katika haki zao za msingi kabisa, msingi wa haki ya binaadamu mmoja, ambao na sisi ni wadau, ni haki ya mtu kupata kula ya mara tatu. Watu wetu wanamiliki hili, kwa bajeti yetu hii ya Mheshimiwa Waziri?

Mimi nakataa hili, nasema kwamba Mheshimiwa Omar Yussuf tubadilike, twende na ukweli, fedha ambayo tunaikusanya ndio tuiandalie matumizi yake ya uhalisia. Tusiongeze tu, maana sasa tumekuwa na maneno tukifika hapa. Mwaka huu tumeambiwa kwamba kuna 707.8 mwakani ikija bajeti maana yake tutakuta iko 800.8. Lakini uhalisia wa fedha tunazokusanya ndizo ambazo zitatuzesha sisi kuweza kutekeleza mipango ambayo tumejipangia. Mimi niulize, nimeona kwamba kuna vipaumbele hapa vimewekwa. Vipaumbele vinasema kwamba kuimarisha miundominu ya kiuchumi na kijamii lakini pia kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo elimu bora na huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, nataka nigande hapa, kama lengo letu ndio hilo kweli, na ndivyo tulivyo, na nimeona kwamba tunasema kwamba uwiyo uliopo kwa wanafunzi wetu, Zanzibar ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 28 huu ni

uongo. Huu ni uongo, tunadanganyana. Haiwezekani, twendeni mashuleni tukaangalie, mwalimu mmoja ana wanafunzi wangapi.

Mwaka jana mlikuwa mkalisema hili, mwalimu mmoja kwa wanafunzi 26, mwaka huu mnasema 28, jamani tunakwenda wapi, tunamdanganya nani. Huyu anaedanganywa nani? Tunadanganya nafsi zetu, hatuwadanganyi watu. Ni vyema tukafanya kitu ambacho kimo ndani ya uwezo wetu. Kusema kweli si dhambi, tuseme uchumi wetu hauruhusu, tusipange mipango kadhaa ambayo hairuhusu. Tusipange mipango kadhaa ambayo haitekelezeki.

Amuweni Serikali, kufanya miradi mitano tu katika mwaka wa fedha. Lakini tunahakisha Sherehe za Mapinduzi zikifanyika miradi imekamili. Leo tuna utitiri wa miradi zikifika sherehe miaka sita, mradi unakwenda unaambiwa ukiingiziwa fedha basi ule mradi vipi, umekuwa tayari, ungeweza kufunguliwa katika sherehe hizi. Jamani hiyo ni bajeti, hiyo nido mipango. Kwa nini tusijiwekee mipango ya muda mfupi tukajiwekea mipango ya kati, na mipango ya baadae ya muda mrefu.

Sisi tunaingia kwenye mikumbo tu na shughuli hasa hususan za kisiasa zimekwaza sana hapa kwetu. Hata ukisema ukweli, ukizungumza juu ya ukweli kuhusu maendeleo ya Taifa inasimamishwa siasa. Hatufiki. Tujitathmini, hizi fedha atunazozipata ndio sahihi, na miradi hii tele tunayoitia ndio kweli. Mradi wa taka salama, sijui mradi wa nini, lakini hiyo yote haitengewi fedha. Fedha unaambiwa haikupatikana ukimuuliza mtendaji, mimi sikupata, sikuingiziwa fedha. Mradi haukuwa Mheshimiwa haikupatikana fedha.

Wahisani nao wameanza kuchoka, maana zamani tulipoanza bajeti ya 2011/12 niliona wahisani walikua wana nafasi pana na kweli walikuwa wakizitoa hizo fedha. Lakini inaonesha wazi kwa wakati huu kwamba wahisani nao wanatuwacha mkono. Mhe. Spika, umefika wakati Serikali ya kutathmini hasa vianzio vyake vya mapato. Lazima tujitathmini, tuvielewe vianzio vyetu vya mapato tena viwe endelevu. Tusibahatishe.

La pili hebu tusimamieni haya matumizi ya hizo fedha, maana hizo fedha zinazopatikana na miradi inayofanywa hazifanyiwi ukaguzi yakinifu. Hiyo mipesa inaingia mifukoni mwa watu, hakuna *value for money* mtu anakwenda zake haulizwi, kazi imekwisha. Baraza lako hili Mhe. Spika, umeliundia kamati Teule ngapi, Serikali imekataa ku-react juu ya hilo, imenyamaza kimya inaficha ufasidi, inaficha mambo ya uovu na uadui. Hizo ni fedha za wavuja jasho, zinahitajika zitumike kwa maslahi yao, leo kinywa Serikali imenyamaza haisemi chochote kuhusiana na jambo hili. Ni jambo la kusikitisha sana.

Serikali umefika wakati ufasidi na wizi tuukomeshe. Nacho hicho ni kikwazo cha kufanya mapato yetu yasipande juu, tukaweza kufikia malengo yetu tuliyojipangia. Mwaka jana nilisema mwaka jana, wazanzibari tumekuwa na matatizo ya kujuwana. Huyu ni mtoto wa mjomba huyu niwashangazi, maana wizi tumeuhalalisha, maana mtoto wa mjomba akiiba Mungu kasema halali. Jamani, tumuogope Mwenyezimungu. Udugu huu katupa kwa mapenzi si kwa wizi. Tunaogopana hatuwezi kusema, ndio ukweli. Hatuwezi kusema na wala kuwajibika, tumetengeneza Tume ya Rushwa lakini hiyo Tume imetengenezwa tu ni pambo, ni sampuli ipo, haijafanya kazi, ndio ukweli.

Kama serikali ina Tume kadhaa tulizotumia kutengeneza makamati hapa hapa Teule, lakini hakuna kinachofanyika, kimya, kama vile watu wanausingizi.

Nije sasa katika kuiangalia afya. Hii huduma ya Afya imefifia au tuna majengo tu. Ni kweli kwamba Waziri wa Afya alijibu hapa kwamba tuna majengo yakutosha na vituo vya Afya vya kutosha ni kweli, lakini je, hizo huduma zinapatikana humo. Suala la wakati huu kwa Serikali ni kuangalia huduma si kuangalia majengo.

Narudia tena kusema kwamba, mumesema humu katika kitabu chenu hiki, mnasema ya kwamba mtawaboreshea wakulima pembejeo nafuu. Nakwambieni si kweli, mimi nimekwenda Mtwango juzi, baada ya kusomwa bajeti. Serikali ndio nyinyi mliotiliana mkataba na wananchi wale wanalima Mtwango, mkawaambia mtawapa pembejeo mkawapa, hazikutimia na hivyo mkasema mtaununua mpunga wao hamkuununua, unaroa, mvua, nguvu za wanyonge zinapotea. Mumewaboreshea nini, kawalipeni pesa zao, sio muboreshe kulima, walipeni kwanza zile pesa ambazo mpunga wao upo pale kanunueni na fedha wanazowadai muwalipe Serikali.

Nimekwenda na mkitaka ushahidi twendeni mkaone hilo. Mpunga wa wanyonge, masikini wamejituma, wamehangaika mumefunga nao mikataba, hamuwalipi pesa zao na mpunga hamuununui. Na tena nikwambieni

unaroa sana, hilo banda ni bovu mno. Naomba sana serikali, mnaingia kwenye sekta za Uwekezaji bila ya kuangalia eneo hilo mnalowapa wawekezaji ndio husika kwa uwekezaji huo? Hamuyaangalii hayo, madam mnataka mna-*react* moja kwa moja mnakwenda tu.

Mumechukua eneo ambalo lina mishokishoki, michungwa, mifenesi, mumeng'oa mnataka kujenga kiwanja cha Gofu, hatari sana katika taifa kufanya hivyo. Hatuna maeneo mbadala. Jamani hatuna *research* katika mipango yetu. Huu ndio utamaduni wetu, tunawapendelea kheri Wazanzibari, tuambiane ukweli. Kama hatukubadilika tukaweza kusimamia mipango ikawa endelevu, ambayo uchumi wetu tukausimamia hatuna safari, tusijidanganye. Nasema tena tusidanganyane. Sote niwatu wazima, tunajuwa kwamba penye fedha ndio kwenye maneno.

Serikali haiwezi *ku-react* kwa mwizi, mbadhirifu, mla rushwa, tunatizamana, tunachekana, tunatumia muda mrefu zaidi wa maneno, vitendo vyetu vimekuwa vifupi. Namalizia mada yangu ya kwanza ya Kanga za Mhe. Aboud Jumbe.

Maneno yetu yamekuwa ni marefu maana kila baada ya mwaka tumekuwa tunakuja kupiga kelele hapa. Maneno mengi vitendo vimekuwa vidogo mno, hakuna pesa katika wizara jamani ndio ukweli, muna masufuri matupu. Tunatarajia kufanya nini mwaka huu wa fedha hakuna, maana yake tusitarajie kitu, hao walimu tunaotaka kuboresha elimu maana yake kama hukuntunza mwalimu, ukampa stahiki zake, na yeye hatoweza kuzalisha hicho unachokihitaji wewe, ndio ukweli huo.

Naiomba sana serikali, tubadilikeni jamani kwa maslahi ya watu. Mungu atatuuliza juu ya haya aliyotupa hapa sisi. Haya hayaji tu, wako wengi wana akili na uwezo kuliko lakini Mungu kataka sisi tuwoko huku kusimamie hiyo mipango ya watu. Tumuombe Mwenyezimungu atuwezeshe hili lakini Mwenyezimungu hatamsamehe mtu anayefanya kwa makusudi juu ya jambo hili.

Mhe. Spika, nije kwa upendo kabisa, kwa sauti ya unyenyekevu kabisa, ile ya mwanzo ni sauti yangu ya kawaida ninapokuwa nazungumza sauti ya kibunge. Lakini niombe serikali, ifikirie sana kabisa juu ya kuweka miradi inayotekelezeka isiwe miradi mingi lakini utekelezaji wake ukaenda kwenye miaka kumi, haipendezi. Maana hata huyo unayemuweka unamkuta yule Katibu Mkuu anayesimamia kahamishiwa Wizara nyengine, akija huyu hajui aanze wapi. Mradi haujakamilika, wala haujafika mwisho. Hili halipendezi. Ni vizuri kabisa tukajiweka vizuri, lakini pia tukasimamia njia za uchumi, tusiogope. Wazanzibari ni matajiri, na rasilimali ya mafuta na gesi tunayo.

Zamani ilikuwa aibu, ukisema unashikwa mdomo, kwa nini useme, maana yake, tunayo. Naona Mhe. Spika unataka kuniambia nisimame, lakini niseme kwamba nakushukuru sana kunipatia fursa hii nami ya kutoa mchango wangu mdogo, lakini sitaunga mkono hii mpaka nipate maelezo ya kina juu ya mipango ya Serikali, safari hii na miradi yake kuhusu shughuli za maendeleo ya Taifa hili. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Sasa nimkaribishe Mhe. Ali Salum Haji na baadae Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhiti kupata fursa hii kuwa mchangiaji katika asubuhi hii ya leo. Kabla sijaanza lolote nianze kwa kumshukuru Mwenyezimungu kwa kunijaalia afya njema. Lakini pili nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa namna anavyosimamia Serikali yake pamoja na wasaidizi wake wote wawili.

Tatu Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa namna anavyosimamia Wizara yake kwa umakini kabisa na umahiri katika Serikali hii.

Mhe. Spika, nitajaribu kwenda mbio mbio katika kukidhi muda wako naomba niingie kwenye kitabu cha Bajeti ukurasa wa 14 na 15 makusanyo ya kodi *TRA* na *ZRB*.

Mhe. Spika, tumeona jinsi ya mafanikio ya makusanyo namna yalivyoongezeka. Hii ni hali ya kupigiwa mfano na kuipongeza Serikali kwa namna inavyosimamia mapato yake.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo watu wanasema "Mgema akisifiwa tembo hulitia maji". Mimi pamoja na sifa zote hizi basi nimuombe Mhe. Waziri pamoja na mafanikio mazuri waliyoyapata katika kuongeza mapato haya bado

kuna matatizo madogo madogo katika taasisi zetu hizi. Nimuombe azidishe jitihada katika kuyasimamia mapato haya ili yaongezeke maradufu. Lakini pia aongeze jitihada katika kuwabaini wale ambao wanakwepa kodi kwa namna moja au nyengine ili kuweza kuzuia mianya iliyokuwa si mizuri.

Jengine ninalotaka kulizungumzia Mhe. Spika, katika ukurasa wa 19 Mhe. Waziri ameelezea namna Wizara ilivyojaribu kuziba mianya ya upotevu wa fedha na namna walivyoweza kufuta mapato haya. Lakini Mhe. Spika, nasema kwamba udhibiti wa mianya una namna nyingi, unaweza ukadhibiti katika namna ya makusanyo pamoja na matumizi. Lakini kuna tatizo ambalo bado linaonekana limekuwa sugu katika Wizara yetu ambalo linapelekea kupoteza fedha nyingi katika Serikali pasipo na sababu za msingi.

Mimi nilikuwa nataka nitaje kama maeneo mawili matatu ambayo Mhe. Waziri ajaribu kuyaangalia na kuyafanyia kazi ili kuweza kuepusha matumizi mabaya ya Serikali ya pesa za walipa kodi.

Sehemu moja Mhe. Spika, ambayo nataka Mhe. Waziri aiangalie na kuifanyia kazi ni sehemu hususan ya manunuzi ya vitu vya thamani vya ofisi. Mhe. Spika, tunakuwa tunapanga bajeti na tunawawekea Mawizara fedha za vitu vya thamani, lakini vitu vinavyonunuliwa vinakuwa havina viwango na fedha ambazo zinatumika na matokeo yake vinakuwa havina muda mrefu wa kuishi baadae kila mwaka Wizara inakuwa inahitaji manunuzi ya thamani na tunapelekea kutumia fedha pasipo katika mazingira mazuri.

Katika eneo jengine Mhe. Spika, kumekuwa na kawaida ya kuacha kutumia nyumba za Serikali na kukodi nyumba za watu binafsi. Hili ni tatizo Mhe. Spika, kwamba tuna nyumba zetu za Serikali, Serikali imetumia gharama kubwa sana kujenga nyumba zile, lakini tunaziacha nyumba za Serikali ambazo zinahitaji ukarabati mdogo na matokeo yake tunakwenda kukodi nyumba za watu binafsi kwa fedha nyingi na tunapoteza fedha za walipo kodi pasipo na sababu za msingi. Hili Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aliangalie na ajue namna ya kulifanyia kazi kwa wale ambao wanaacha kutumia nyumba za Serikali na kutumia nyumba za watu binafsi kwa kodi na gharama yake kubwa.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nataka Mhe. Waziri anisaidie katika masuala ya warsha na semina mbali mbali. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameelezea katika kitabu chake hiki kwamba amejaribu kuangalia kuona namna gani wataandaa warsha na semina katika kipindi hiki cha Bajeti. Yaani tutaacha kutumia hoteli za kigeni na kutumia kumbi zetu za Mawizara ili kuepuka gharama za utumiaji wa fedha kiholela katika Serikali yetu.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri, unaweza ukatumia kumbi hiyo unayotaka wewe ya binafsi lakini kuna jambo ambalo limejitokeza. Hili Mhe. Spika, nataka nimpe mfano Mhe. Waziri lakini naisubiri taasisi husika katika Bajeti ya Kisekta hapa Mhe. Waziri atakuja kutuelezea vya kutosha. Kuna Wizara Mhe. Spika, imeandaa semina hewa, wakaandaa watu wa semina hewa, *documents* hewa, matokeo yake wameitia hasara Serikali pasipo na sababu za msingi. Hii nataka wawe na tahadhari lakini Wizara inayohusika itakapofika Waziri atakuja kunieleza sababu za msingi na kwa nini hatua hazijachukuliwa kwa wahusika mpaka sasa hivi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuzungumzia ni suala zima la ukurasa wa 21 katika ada ya bandari. Suala ni zuri na nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna alivyotuletea katika bajeti iliyopita namna ya kuongeza kodi kutoka shilingi 1,000 hadi shilingi 2,000 kwa wasafiri wa Zanzibar na Tanzania Bara. Ilikuwa ni jambo zuri na tumeona namna alivyoweza kukusanya mapato karibuni bilioni 1.95 zimekusanywa katika sekta hii. Lakini bado mimi nimuombe Mhe. Waziri hebu anieleze ni sababu gani ambazo zimepelekea kukusanya kodi katika upande wa usafiri wa Zanzibar kwenda Dar es Salaam, lakini tukaacha Zanzibar kwenda Pemba wakati pesa hizi zinahusika katika masuala mazima ya kuisaidia jamii. Kwa sababu wanaotembea ni wafanyabiashara na watu wa kawaida, lakini pale tunapokusanya tunazipeleka katika jamii ili ziwaisaidie na hususan katika masuala ya afya, maji na elimu. Na nashukuru kwamba hili zaidi tumeliweka katika suala hili.

Kwa hiyo atwambie sababu za msingi na kwamba hatuoni haja bado umefika wakati kwamba baada ya kukusanya pesa hizi kwa upande mmoja kwa kuiga, mfano huu basi kipindi hiki kwa nini tusiipitishie na upande wa pili ili tukapata hizi pesa nyingi zikaweza kusaidia wananchi wetu kuondokana na umaskini katika hali waliyokuwanayo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niendeleo katika ukurasa wa 26 vipaumbele ambavyo Mhe. Waziri amevitaja. Mimi nataka niende katika sekta ya elimu, afya na maji. Ni jambo la muhimu kuyapa kipaumbele masuala haya, ni

jambo zuri, lakini bado pamoja na kupewa kipaumbele, kwa sababu kipaumbele hiki sijui kama kuna miaka hakijawekwa, kila mwaka elimu, afya na maji kwa sababu ndio vitu vya muhimu. Lakini pamoja na kupewa kipaumbele bado kuna matatizo makubwa katika sekta hii, tunatumia fedha nyingi, Serikali inajikita kukopa fedha katika hizo taasisi, lakini fedha zinazokwenda kutumika ni tofauti na Serikali inavyojipanga na zile Wizara za kisekta namna zinavyotumia fedha zile.

Mhe. Spika, kuna mifano mingi sina haja kwa sababu ya muda kuelezea yote. Lakini kwa mfano tu Serikali ilitenga fedha katika masuala ya skuli za sekondari na wengi wamenufaika Mpendae, Kwamtipura na wengine huko. Lakini baadhi ya maskuli yamejengwa chini ya kiwango na ni hatari kwamba muda mdogo skuli zimeanza kutoka *tiles* na nyengine zinavuja, hivyo inakuwa Serikali yale malengo tuliyojiwekea hatufikii pahala muafaka, kwa sababu tunatengeneza baadae katika kipindi cha mwaka mmoja inabidi zitafutwe gharama nyengine katika kufanya matengenezo.

Sasa ni dhamira nzuri na hilo hata katika masuala ya maji ndio hayo hayo rafiki yangu hapa Mhe. Hamza Hassan Juma amesema sana katika sekta ya maji, alifika mwisho kuleta majeshi ndio wapewe ile taasisi. Ukiangalia miradi mingi imekwenda katika mamlaka ya maji, gharama kubwa za ndani, za nje, za wafadhili tunaweza katika suala la maji. Lakini ukiangalia faida katika kuwekeza haionekani. Kuna mradi ule wa Mkoa Mjini Magharibi wa Japan gharama zilizotumika hazina idadi, lakini ukenda ukiangalia *benefit enough* hamna kitu Mhe. Spika.

Sasa Mhe. Spika, mimi nafikiri kuna haja ya kuangalia pale tunapoweka pesa katika kuondosha matatizo basi pia tuandae na mikakati ya kuhakikisha kwamba ile miradi inakwenda katika ufanisi na inakuwa ni miradi yenye ubora kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo dada yangu aliyekaa chini alijaribu kulizungumzia kwa kina na mimi nilikuwa nimeshaliweka hapa ni suala zima la ukurasa wa 34 pembejeo za kilimo. Mhe. Spika, kuna masikitiko makubwa sana bado tunarudi pale pale kwamba Serikali inakuwa inapanga mipango mizuri lakini wanaopewa dhamana ya kusimamia ile mipango inakuwa haiko katika hali nzuri.

Mhe. Spika, tunafahamu kuwa bajeti zilizopita zilikuwa zinaonesha namna ya pembejeo, mbolea zinavyokuwa hazina ubora, badala ya kukuza mimea zinaathiri mimea, mipunga hapa iliwahi kuungua. Lakini kuna kilio tangu majuzi ambacho tunakisikia katika maeneo mbali mbali, mwenzangu amesema yeye kaenda Ndiyani sijui, lakini mimi nilisikia mara mbili katika vyombo vya habari kwamba wananchi wanalalamika katika suala zima la pembejeo hususan mbegu. Wananchi wale wanasikitika kwamba hawajalipwa na nikamsikia Katibu Mkuu mwenyewe anazungumza kwamba wasiwe na wasi wasi wawe na subira kwa sababu Wizara ya Fedha inakuwa inawaingizia pesa kidogo kidogo kwa mafungu.

Sasa Mhe. Spika, hii ni hatari, wewe unapoizungumzia Wizara ya Fedha inaingiza pesa kwa mafungu ndio sababu hujawalipa watu, lakini watu walikuwa wanalala na njaa, watu wamelima kwa mantiki ya kuhitaji kwamba wanasubiri wapate chochote angalau waweze kujisaidia na maisha yao. Sasa wewe ukisema unasubiri Wizara ya Fedha kidogo kidogo iingize mafungu, na yule mwananchi wa chini maskini wa Ndiyani, Jendele na maeneo mengine yenye mabonde kama Mwera unafikiri unaweza kumueleza kwamba na yeye asubiri, labda asile kidogo kidogo mpaka pesa ziingizwe hii ni hatari.

Mimi nafikiri kuna haja ya kujipanga katika hili tuone kwamba tunajipanga vipi baina ya mtoaji na mpokeaji, ili kwa yule ambae anahitaji kuzipata zile pesa basi azipate kwa wakati ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu na kadhia ya kuwa na umaskini wa kuendelea.

Mhe. Spika, jengine ni ukurasa wa 40 tumeona kwamba Mhe. Waziri amejipanga katika suala zima la kuanzisha utaratibu wa kukusanya kodi kwa kutumia hizi mashine za *electronic*. Ni jambo zuri ambalo litaepusha ile migongano midogo midogo, litaepusha zile dhana ambazo tulikuwa tunazo za kutokuwaamini baadhi ya watendaji kwamba wanatumia njia za kukusanya kodi kwa kujinufaisha wao wenyewe. Lakini nilikuwa naomba nitoe indhari kwamba mashine hizi kwa wenzetu wa Tanzania Bara zilileta kadhia kubwa sana katika pande mbili; moja katika suala zima la kuona namna gani wanaweza kutumia katika ukusanyaji wa kodi. Walikuwa wanaamini kwamba wao mashine zinawabana na ikafika pahala baadhi ya wafanyabiashara kufunga maduka.

Jengine ilikuwa katika suala zima la gharama za mashine yenyewe kwa yule mtu ambae alipewa tenda kuingiza zile mashine kulikuwa kuna matatizo na watu walipiga makelele sana kwamba mashine zile zinazuzwa rahisi, lakini zinapoingia nchini zinakuwa na gharama kubwa mfanyabiashara anashindwa kuzinunua na kuweza kutekeleza haya mahitaji.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri ajipange vizuri katika namna zote, katika suala zima la uandaaji wa tenda wakati wa kuingiza mashine katika nchi yetu, lakini na suala zima la elimu kwa watumiaji wa mashine ikiwemo wafanyabiashara wote.

Mhe. Spika, jengine ni suala la misamaha ya kodi. Mhe. Spika, naishukuru Wizara na Serikali kwa ujumla ina nia njema kwa wananchi wake na inakuwa inajipanga kuona namna gani inawasaidia wananchi wake. Mhe. Spika, kuna utaratibu huu wa kutoa misamaha katika bidhaa muhimu kama mchele, sukari na unga wa ngano kwa wafanyabiashara wetu ili wananchi wanyonge, wa kipato cha chini waweze kunufaika na huu msamaha katika kupata bidhaa kwa bei ya chini. Lakini bado inaonekana kuna matatizo na ulaghai kwa wafanyabiashara, kwamba wafanyabiashara wetu hii fursa wanayoipata ya msahama wa kodi hawaitumii ipasavyo, wao wanapata misamaha lakini ukenda ukiangalia bei za bidhaa wanashindwa kuziua katika bei ya chini.

Mimi nahisi kwa Mhe. Waziri kuna haja ya kuwa na chombo mahsusi ambacho kitakuwa kina-*monitor* wale wafanyabiashara ambao wanakwepa misamaha ya kodi kwa ile misamaha kwa kile ambacho wanakipata, msamaha na namna gani wao baada ya kupata misamaha wanaweza wakawasaidia wananchi wetu kwa kuuza bidhaa zile katika hali ya chini. Vyenginevyo itakuwa ndio yale yale tunawapa watu misamaha lakini bidhaa wanauza kwa bei ya juu miaka miwili matajiri maghorofa kila pahala, biashara zenyewe hazijulikani.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumzie na nafikiri itakuwa ni suala langu la mwisho katika uchangiaji wangu, kuna hili suala la bajeti ya kawaida katika kuangalia kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba safari hii wameangalia zaidi katika bajeti ya kawaida na wameacha kuangalia zaidi bajeti ya maendeleo kutokana na hali halisi. Na hawakuongeza mishahara kwa sababu ya kutaka kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kipindi kilichopita. Ni jambo zuri Mhe. Spika, na hili lilikuwa lina lengo maalum, lengo lake ilikuwa ni kuboresha zaidi fedha kwa wataalam wetu ili kuweza kuwabana.

Kwa sababu katika kipindi cha nyuma tulikuwa tuna kawaida tumezoea wataalam wengi walikuwa wanashindwa kukaa nchini kufanya kazi, kwa sababu ya maslahi madogo ya fedha ndio ukakuta madaktari wanakimbia maeneo ya Uganda na Zimbabwe. Walimu wengi walikuwa wanakimbilia Tanzania Bara.

Sasa niishukuru Serikali kwa kuliona hili na kuamua kuwajengea uwezo mzuri hawa wataalam ili waweze kuwa na imani ya kubakia kufanya kazi katika nchi yao.

Pamoja na kuwaandalia maandalizi mazuri wataalam bado kuna matatizo katika wafanyakazi wengi wa kada ya chini na hususan wale wazoefu, kwamba kuna watu kwa muda mrefu pamoja na Serikali kuwa inafanya marekebisho haya bado wao wana matatizo ya marekebisho katika mishahara yao. Nimuombe Mhe. Waziri basi afanye jitihada ya kurekebisha yale mapungufu ambayo yamejitokeza kwa baadhi ya wafanyakazi katika kipindi cha bajeti ya mwaka jana mpaka mwaka huu. Mpaka leo hawajaweza kufanyiwa marekebisho ya mishahara yao na wamekuwa wakisitika hapa na pale.

Sasa namuomba sana Mhe. Waziri zile kasoro ambazo zimejitokeza kwa baadhi ya wafanyakazi kutokurekebishiwa mishahara yao basi wayafanye jitihada ili kuweza kuondosha usumbufu huo.

Mhe. Spika, baada ya hayo nikushukuru kwa dhati kabisa na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani nasema naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri mia kwa mia na naitakia kila la kheri. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii ili kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hizi mbili za Mpango wa Maendeleo pamoja na hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, tukianza kuzungumzia bajeti lazima kwanza tuzungumzie hizi nambari ambazo Waheshimiwa Mawaziri hawa wametuletea. Na nambari hizi ndio ambamo muna matumaini ya wananchi. Maana ukianza kuleta

nambari zinazoonesha uchumi unakua, makusanyo yanaongezeka hii ni dalili ya kuwapatia wananchi matumaini, kwa hiyo na mimi nataka nianze na hizi nambari.

Mhe. Spika, nimekiangalia kitabu cha Mpango wa Maendeleo kuhusu ukuaji wa pato la taifa na tukaambiwa pale kama pato la taifa sasa hivi ni shilingi 1,442.8 bilioni na huo ni ukuaji wa asilimia 7.4. Sasa hilo ukitizama linatia moyo kidogo lakini ukija ukigeuka kwenye pato la mwananchi kwa mwaka ni sawa sawa na dola za Kimarekani 665. Sasa kiwango hiki hakipishani sana na kile cha mwaka uliopita.

Kwanza Mhe. Spika, mimi naona hiki kiwango ni kidogo sana, ni kidogo ukilinganisha na maisha wanayoishi Wazanzibari hapa yenye wastani wa shilingi milioni moja sijui na nukta ngapi kwa mwaka ambazo haziwezi kumsaidia Mzanzibari hata kwa nusu mwaka sikwambii mwaka mzima. Kwa hiyo hali yetu ni mbaya.

Kwa upande mwingine hiyo kiuhalisia Mhe. Spika, kwa sababu hiyo ni *average* ya pato la kila Mzanzibari, lakini ukija kwenye ukweli hasa hili si pato la kila Mzanzibari, ni sawa sawa na kupiga mfano na watu 10, lakini watu 10 hawa watu watano wana milioni zao 10 kwa mfano, hawa watano hawana hata shilingi. Lakini sasa ukifanya *average* ya watu 10 basi wale watu watano wenye milioni zao 10 utazigawa mpaka kwa hawa watano wengine ambao hawana kitu.

Sasa unapata kigezo kwamba kila mtu kati ya wale 10 ana milioni mbili kwa mfano lakini kumbe si kweli walio na milioni zao 10 ni wale watu watano tu na hawa huku hawana kitu. Sasa ndio mfano huu ni watu wachache waliomiliki hizi nambari za mapato ya nchi.

Ni vyema niainishe zaidi kwamba mapato haya Mhe. Spika, wanapata wanasiasa, wanapata na Maafisa wa Serikali Waandamizi ndio wanaomiliki hizi nambari. Lakini ukitoka hapo ukija chini huku hakuna kitu. Sasa ukifanya *average* ya mapato ya watu hawa wachache ambao hata ukiangalia asilimia yao haifiki asilimia 20 ya Wazanzibari wote, halafu ukagawa pato la watu asilimia 20 kwa watu asilimia 100, kwa kweli Wazanzibari hujawatendea haki.

Sasa nakusudia kusema hizi dola za Kimarekani 665 ambazo tunaambiwa anapata kila Mzanzibari, mimi nadhani si kweli, ni utaratibu tu ambao Mhe. Waziri anautumia kwa kuja kuonesha kwamba kwa pato hili la nchi, basi kila Mzanzibari anafaa kupata asilimia hii, lakini uhalisia hasa si kweli.

Nilikuwa nafikiri ili kuwa muwazi zaidi Mhe. Waziri bora katika miaka inayokuja hebu awagawe watu kwa *category*, aangalie watu hawa mapato yao ni kiasi fulani atupe *average* yao. Halafu aje kwa asilimia ya watu wa chini atwambie ukweli mapato yao ni kiasi gani na *average* yao ni kiasi fulani. Mhe. Spika, kufanya hivyo hii itashuka mpaka dola 200, sasa hii nasema kiuhalisia. Lakini nilitangulia kusema kwamba pato hilo hata apate kweli Mzanzibari haliridhishi. Haliridhishi Mhe. Spika, hebu tulinganisha visiwa vyetu vya Zanzibar ambavyo kwa mfano Zanzibar ina *square kilometre* 2,600 takriban. Wenzetu wa Mauritius wana *square kilometers* 1800. Vyote viwili ni visiwa katika bahari ya Hindi. Vyote viwili ni visiwa ambavyo takriban vilipata uhuru wao katika muongo mmoja. Wakati vinapata uhuru visiwa hivi, uchumi wa Zanzibar ulikuwa ukiongozwa na karafuu na uchumi wa Mauritius ulikuwa ukiongozwa na miwa.

Hivi sasa Wazanzibari tupo takriban *population* yetu ni 1,300,000 na Wa-Mauritius takriban nao wapo katika kiwango hicho hicho. Lakini sisi tumeongezeka kwa eneo. Kwa hivyo tunapaswa sisi uchumi wetu kuwa zaidi kuliko wao. Lakini hebu tuangalie pato la Mzanzibari anayeambiwa sasa hivi ana dola mia sita na sitini na saba kwa mwaka, wakati mwananchi kutoka Mauritius ana dola elfu kumi na mbili kwa mwaka.

Mhe. Spika, tulikosa nini mpaka tukadumaa katika kiwango hicho wenzetu wakenda mbele katika kiwango hicho. Tafsiri yangu Mhe. Spika, hizi sera zetu na ilani za Chama cha Mapinduzi zimepitwa na wakati hazitotufikisha tunakokwenda. Ndio tafsiri yangu mimi.

Kwa hivyo kuna haja sasa ya kupanga ilani nyengine Mhe. Spika, na hiyo ilani iseme wazi kwamba hatufuati ilani ya chama chochote, tupange ilani ya nchi, tupange sera ya nchi. Chama chochote kinachokuja serikalini kifuate sera hizo. Labda hiyo itatusaidia na kitakaposhindwa mwaka unaofuata wa uchaguzi hiyo chama kiambiwe kaa pembeni hufai kutoongoza sisi Wazanzibari. Mhe. Spika, lakini tukiendelea kung'ang'ania tu tutafika pahali kwa kweli akidi au asilimia ya watu ombaomba Zanzibar itakuwa kubwa sana.

Mhe. Spika, sasa niendeleo kukosoa hii sera pia ya mfumo wa muungano wa serikali mbili. Ninaendelea kuukosoa kwa sababu ya athari zake kiuchumi kwa Zanzibar. Mhe. Spika, toka kuingia kwa mfumo huu, kuna tatizo kubwa sana la Zanzibar kupoteza *sovereignty* yake. Kwa sababu hatuna *sovereignty* ile misaada kutoka nje ya nchi ambayo inatusaidia sana sisi Wazanzibari au Watanzania au zinawasaidia sana nchi zinazoendelea, sisi kama Wazanzibari tunazikosa.

Mhe. Spika, nitatoa mfano mmoja mdogo, tena mdogo sana maana yake katika mingi. Tuna hiki chama chetu cha mpira hapa cha *ZFA*, Chama hiki kilipeleka maombi ya kujiunga na *FIFA* lakini *FIFA* wakajibu kwa sababu Zanzibar sio *independant country*, sisi hatukuruhusu kujiunga. Kwa hivyo muktaka nendeni Tanzania kwenye *TFF*.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Juma Shamuhuna juhudi zake zote zikakwama. Matokeo nini? Matokeo yake kila mwaka *ZFA* inakosa karibu dola laki tatu za kuendeleza michezo hapa nchini. Wenzetu *TFF* hivi sasa wanajenga jengo la ghorofa 18 kupitia misaada hii. Sisi tunaendelea kudumaa.

Mhe. Spika, kwa hivyo kwa mfano huo na mifano mengine mingi ambayo tunaikuta hata katika sekta za serikali hapa. Waziri fulani anakwenda kuomba msaada kivyake vyake, anaambiwa *okay*, sisi tupo tayari kukupa msaada lakini hebu aje Waziri wa Jamhuri ya Muungano hapa atie saini yake. Waziri wa Muungano anaambiwa anakataa. Matokeo yake msaada ule hapa sisi hauji lakini kwa wenzetu unakwenda. Kwa hivyo bado ninasema, sera hii ya serikali mbili, mimi ninadhani wenzangu waniwie radhi sana, lakini inaendelea kutudumaza katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, niendeleo kutoa mfano; kwa mfano mwaka huu hotuba ya Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano imetaja mapato yatokanayo na misaada na mikopo nafuu kutoka nje ya nchi. Ni bilioni elfu moja mia moja na sitini na tatu. Ukiangalia kama tulivyokubaliana kati ya fedha hizo Wazanzibari tuna asilimia yetu ya 4.5. Mhe. Spika, tungeipata hiyo, tungelazimika kupata bilioni hamsini na mbili nukta tatu tano. Lakini matokeo yake tumegaiwa milioni 32.62 ambayo hiyo ni sawa sawa na asilimia 2.8 pekee. Kwa mwaka huu tu wametunyima wenzetu karibu bilioni 25.14.

Mhe. Spika, hizo ni pesa nyingi sana ambao wenzetu wamezipata kwa mwaka huu. Ukizikusanya hizo kwa muda wa miaka kumi, watakuwa wametunyima bilioni 251. Mhe. Spika, pesa ambazo kwa mazingira yetu ya Zanzibar tungezipata hizo basi zingetusaidia sana kuimarisha huduma zetu za jamii. Kwa mfano, afya isingekuwa tena tatizo kwenda pale Hospitali ya Mnazi Mmoja ukaambiwa hakuna dawa. Isingekuwa tatizo kwa vijana wetu sasa hivi kukosa hata madeski ya kukaa kule maskulini. Tusingekuwa na tatizo sasa hivi la maji kwa mfano. Tungepata pesa humo za kuwawezesha wakulima wetu katika kujiimarisha kilimo.

Mhe. Spika, lakini yote hayo tunayokosa kwa sababu ya mfumo huu mbaya wa muungano. Kwa hivyo ninaendelea kuwanasihii wenzangu, tukubali kubadilisha huu mfumo ili na sisi tujifungue na pingu za miguu tupate kwenda mbele. Vyenginevyo tuing'ang'ania tutaendelea kudumaa siku hadi siku na wenzetu watatupita katika kiwango kisichotabirika.

Mhe. Spika, nikiacha hilo sasa nizungumzie kidogo kuhusu uvujaji wa mapato. Ili tuendeleo tunahitaji kukusanya mapato itakiwavyo. Tunahitaji kupata ufanisi mkubwa katika kukusanya mapato. Kwenye vitabu vya bajeti haya makisio tunayoambiwa, ukija mwisho wa mwaka basi ni maeneo machache sana ambayo tunayafikia kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, lakini mara nyingi kunakuwa na upungufu mkubwa katika makusanyo.

Mhe. Spika, sasa tulichokigundua kuna uvujaji wa mapato na mara nyengine unachangiwa na viwango vikubwa vya kodi. Kwa sababu mfanyabiashara unapomuekea kiwango kikubwa cha kodi, yule ni binadamu akiona pato lake linapungua anatafuta mbinu ya kukwepa kodi. Sasa ili akwepe kodi analazimika kula na watu. Kwa hivyo usije leo ukashangaa mfanyabiashara anakubaliana na afisa wa *TRA* au anakubaliana na afisa wa *ZRB* ili wafiche ukweli katika bidhaa alizozileta. Kwa mfano kama kontena linagharimu milioni thalathini, wamuandikie kwenye zile *documents* kwamba kontena lake linapaswa kulipwa milioni kumi na tano na hizi kumi na tano hizi, wanazigawa. Mhe. Spika, kwa hivyo kwa njia hii kodi yetu inapungua sana na ni kwa sababu ya viwango vikubwa vya kodi. Hivyo nilikuwa ninaishauri serikali suala hili iliangalie tena.

Halafu kuna mapato yanakosekana sana...

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika 5 za kumaliza hotuba yako.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: ...kupitia watalii. Mhe. Spika, watalii wanaoingia hapa nchini ni wengi mno. Lakini pamoja na wingi wa taasisi zinazoshughulikia watalii, ukitaka kupata idadi ya watalii wanaoingia kwa siku au kwa mwezi, hata siku moja huwezi kuipata. Katika sekta ambayo inajitahidi sana katika kukuza uchumi wetu ni sekta hii ya utalii lakini kuna mapapa wamekaa humo, wanakunja pesa za wananchi kupitia utalii wakitafuna. Mhe. Spika, sasa nilikuwa ninaomba sana kupitia Mhe. Waziri aliangalie suala hilo kwa macho makubwa zaidi.

Mhe. Spika, halafu ukiangalia huu utalii ulikusudiwa kuwasaidia sana wananchi. Sio tu kwa kulipa kodi ya serikali lakini wale wananchi wenyewe walipaswa kufaidika kwa ajira. Wamo wanaoajiriwa lakini ajira nyingi nyengine zinakwenda nje ya nchi. Lakini ukiacha hivyo kuna *concept* ya utalii kwa wote, maana yake nini? Maana yake utalii uwe unatengeneza angalau soko la bidhaa zetu za kilimo, soko letu la bidhaa zetu za baharini. Lakini kutokana na kudumaa kwa wananchi wetu na kutokana na kwamba sera hizi na ilani hizi haziwasaaidii sana wananchi wetu. Wananchi bidhaa zao wanazozalisha zinakuwa haziuziki katika mahoteli ya kitalii, na badala yake watalii au mahoteli ya kitalii yote yaliopo katika nchi yanalizimika kuagiza mpaka tungule, mbatata, makebeji kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Spika, matokeo yake sisi badala ya utalii huo kusaidia kukuza soko la ndani ya nchi, lakini unasaidia kukuza soko la jirani zetu la Tanzania Bara kule, sio sisi. Sasa hii nayo ni kasoro kubwa. Ninadhani kuna haja ya ilani hizi kuziweka sawa ili wananchi wetu waweze kuzalisha bidhaa zilizo na ubora utakaosaidia kukubalika katika mahoteli. Mhe. Spika, kwa kumaliza ninataka niseme kwamba siridhishwi hata kidogo na bajeti ya maendeleo. Kwa sababu bajeti ya maendeleo ukiangalia, makusanyo ndani ya nchi yetu ni bilioni 365. Lakini zinazokwenda kwenye maendeleo ni bilioni 65 pekee. Bajeti yote ya maendeleo inachangiwa na pesa kutoka nje ya nchi, pesa ambazo hazina uhakika. Ukiambiwa mutapatiwa bilioni 300, basi mwishoni mwa mwaka Waziri anaripoti asilimia 65, 60 ya mapato ya nje.

Mhe. Spika, kwa hivyo kama hatujajirekebisha tukaweza kutumia mapato ya ndani zaidi kwa maendeleo, tukaendelea kutegemea mapato ya nje basi nchi yetu itaendelea kukusanya pesa kwa ajili ya mishahara na *other charges* tu lakini pesa za maendeleo au mipango ya maendeleo siku zote itakuwa ikifeli.

Mhe. Spika, na ndio maana ndani ya miaka hii minne, serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein haijabuni hata mpango mwengine mpya wa maendeleo, inaendelea kusota na mipango mikongwe ambayo haijatiimbia mpaka leo. Hii kwanza ni aibu! Miaka minne munashindwa kuibua mipango mengine mipya ya maendeleo!

Mhe. Spika, la mwisho kabisa mimi nimepata tatizo kidogo au niseme kuna utata kwa baadhi hii ya maendeleo. Tumekosa uwazi na kwa sababu tumekosa uwazi, sisi tunaanza kuangalia kama kuna *indicators* za ufisadi katika miradi hii na ninaomba niitaje:-

1. Mradi wa *Terminal II* wa *airport*, uwazi wake ni tatizo.
2. Barabara zile za Pemba mpaka leo zinasuasua, kuna nini hebu mutwambie.
3. Kuna mradi wa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri, mpaka leo hakuna uwazi katika hili.
4. Kuna mradi wa maendeleo ya eneo la Bwawani pale. Tumetajiwa tu lakini hatuoni kinachoendelea.
5. Kuna mradi wa mkonga wa mawasiliano, mpaka ukiuliza *analysis* ya matumizi ya pesa zile huwezi kuambiwa. Hebu tuambie huko wizarani kuna nini mheshimiwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninadhani Mhe. Waziri atakuja kunijibu mpaka niridhike ili nisije nikainua mkono kupinga bajeti hii.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Sasa nimkaribishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuniruhusu kuchangia. Lakini kabla ya kuanza kuchangia nina ushahidi wa picha kama tatu hizi, naomba moja nimkabidhi Mhe. Waziri wa Fedha na moja nilete kwako. Wahusika naomba wakukabidhi hizi.

Moja mpe Mhe. Waziri wa Fedha na moja mpe Mhe. Spika.

Wajumbe: Picha za nini sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, na mimi nianze katika kuchangia kwangu kwenye kitabu cha Wizara ya Fedha ili kuimarisha miundombinu katika kero zilizopewa kipaumbele kwa kuimarisha miundombinu ya kiuchumi. Mhe. Waziri wa Fedha mwaka jana hapa alikuja kuchangisha katika hotuba yake shilingi thalathini ya lita ya mafuta kwa lengo la kuimarisha barabara.

Mhe. Spika, hizo picha nilizoleta ndio hali ya barabara zetu zilivyo na mzigo unazidi kuendelea hivi sasa zikiwa mjini na nyengine hata katikati ya barabara unaweza kupanda mgomba. Hizo picha ni za Darajani eneo la Mji Mkongwe hilo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, huku serikali ni kujiongezea mzigo juu ya mzigo. Hivyo, Mhe. Spika, barabara hii ukachukue dongo la uwandani la kupandia muhogo ukatie katikati ya barabara. Mimi Mhe. Waziri kwanza utakapokuja kwanza unieleze tokea ulipopitisha hii bajeti ya shilingi thalathini na tano kwa lita ya mafuta ya petroli na dizeli, hizo pesa zimekwenda wapi na zimefanyiwa nini?

Mhe. Spika, leo hii udogo wa kupandia muhogo unakwenda kuitia katikati ya barabara, ikaja mvua utakaa kweli. Tunatengeneza au tunabomoa, ndio miundombinu ya kweli hii inayohitajika. Ni kitu cha kusikitisha sana ikawa dereva au mwananchi anachangia barabara ile, matokeo yake huyaoni. Sawa sawa na kwenda sinema baada mchezo hauoneshwi, sijui pesa yako umdai nani?

Mhe. Spika, tuangalie barabara ya kwenda Jambiani kuna wawekezaji wangapi wenye mahoteli. Wale wengine ninafikiri hata hawajaomba misamaha ya kutoa kwenye mahoteli. Barabara ile nimekuwa nikipiga kelele muda mrefu. Kuna mahoteli karibu kumi mpaka kumi na tano. Ninafikiri mimi hata hawajaomba msamaha katika uwekezaji wao. Barabara kama ile wawekezaji wa nje, kutengenezewa barabara kutiliwa fusi ni kitu cha aibu. Kwa hivyo, hapa utakapokuja Mhe. Waziri unieleze shilingi ngapi ulizokusanya tokea kuanzisha bajeti ile mwaka jana hadi hapa tulipofikia, hadi leo kufikia barabara kutiwa vumbi utafikiri kunataka kupandwa muhogo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ni je upande wa pili, kuimarisha huduma za kijamii zikiwemo elimu bora na huduma za afya.

Mhe. Spika, hapa kidogo ni pahali ambapo pananisikitisha sana tena sana. Wizara ya Fedha haijawa tayari kwa kweli kuimarisha kitengo hiki cha afya pamoja na jitihada alizozichukua Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwenye wizara, lakini bado hali ya Hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja imekuwa tete. Wataalamu wetu wengi wataendelea kukimbia na kutoroka kwa hali hii. Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza hapa kwamba Hospitali madaktari hawakai na hawakai kweli.

Mhe. Spika, kwenda kumtafuta daktari wa mifupa anakusubiri pale, daktari ni mmoja tu wa mifupa ninayemjua mimi ambaye ni Dkt. Shaib. Sasa hii bajeti imezingatia kweli Wizara ya Afya hii. Leo pale nenda saa saba kaangalie panapochomwa taka pale, baada ya ule ugonjwa uliokuwemo mule ndani na maradhi mengine tunayazidisha sisi wenyewe kwa makusudi. Mashine ya *incinerator* haipo, taka zile zikawashwa mule ndani moja kwa moja mpaka kwenye vyumba vya wagonjwa, chumba chenye kimoja wagonjwa watatu, wawili kwenye kitanda, tunaongeza mzigo mwengine. Bado Waziri wa Fedha pamoja na kusema kwako kwa miundombinu kuwa umepeleka katika Wizara ya Afya au kipaumbele kipo katika Wizara ya Afya, lakini bado imekuwa ni kizungumkuti. Bado wataalamu wetu watazidi kutoroka katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na mafao madogo wanayoyapata.

Mhe. Spika, halafu nikafikiria zaidi Mhe. Waziri utasema hapa kuwa miradi mingi, mimi niitaje miwili tu ambayo ya muda mrefu na mpaka sasa hivi hakuna hatua iliyochukuliwa na kuhusu bandari ya Mpigaduri siju tumefikia wapi?

Habari ya kujenga Hospitali kubwa ya Binguni nayo sijui imefikia wapi? Ndio vipaumbele hivi, umetaja Wizara ya Afya hakuna kinachoendelea mpaka muda huu tunavyokwenda.

Halafu ukija katika sekta ya uvuvi, hata Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein alipounda katika uteuzi wake Wizara ya Uvuvi kaiweka mbali kutokana na umuhimu wake, haikuguswa humu habari ya uvuvi, ni kitu cha kusikitisha sana. Mhe. Spika, suala la *TRA* wafanyabiashara wa Zanzibar kusumbuliwa Bara ni suala limekuwa la muda mrefu. Tanzania ni nchi moja, tunatumia mfumo mmoja wa kodi na tuna mamlaka sawa ya kusimamia kodi, yaani *TRA*, tuna viwango vimoja vya kodi mpaka leo wafanyabiashara wetu mizigo yao miezi sita mpaka mwaka hakuna kinachopatikana kule ndani.

Leo tuangalie neema aliyotujaalia Mwenyezi Mungu, Waziri wetu wa Fedha katokea Zanzibar, waziri wetu wewe mwenyewe hapa ni Mzanzibari. hebu fikieni pahali mzikaguwe hizi kero ni za muda mrefu, wewe unategemea Mhe. Waziri wa Fedha yatakuwa mapato kweli kwa hali kama hii, hayawezi kukuwa.

Mhe. Spika, ni kitu cha kusikitisha sana.

Mhe. Spika, nije kwenye Mfuko wa Jimbo. Kwanza nikupongeze Mhe. Waziri kwa dhati, mtoto akizaliwa haendi mbio, hutambaa, akisota akipata mguu. Ulianza na milioni 10, ukaja milioni 15, mpaka sasa hivi milioni 20, hiki ni kitu cha kutia moyo na nikupongeze kwa dhati kabisa.

Mhe. Spika, lakini nikuambie jengine Mhe. Waziri, kuna mengine utataka *return* huwezi kupata. Mwanafunzi ukamsaidia pesa hizi atakupa *return* itatoka wapi? Mwanafunzi unamsaidia akanunuwe viatu, akanunuwe raba, akanunue buku, atakupa *return* kutoka wapi? Ni kitu cha kusikitisha, kwa hizi nyengine usitegemee kuwa *return* zitarudi.

Formula ya 4. 5 ya mgao wetu kutoka kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara au Serikali ya Muungano, hii *formula* ni ya muda mrefu na hii ikae ikizingatiwa nayo, lazima hii kodi iongezeke sasa kutoka 4. 5. *Population* ya Zanzibar inazidi kukuwa, hatuwezi kubaki hapa hapa 4. 5 na mgao huu.

Mhe. Spika, kwa hayo, machache naomba nifikie hapo tu (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Hassan Hamad Omar na baadae tumsikilize Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa na hali ya uzima na afya inayoniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu hili, ili kutoa mijadala ya michango yetu.

Mhe. Spika, mimi nianze na kitabu hiki cha Mhe. Waziri wa Fedha, katika ukurasa wa 26 kifungu nambari IV ya kirumi, ambacho kinasomeka kama ifuatavyo, naomba kunukuu kwa idhini yako;

Kifungu cha IV "*Kuimarisha mazingira ya biashara kwa kuondoa vikwazo visivyo vya lazima na urasimu*".

Hili ni jambo jema Mhe. Spika, na kama tunaweza kulifanyia kazi, basi wafanyabiashara wetu wanaweza kuendelea.

Mhe. Spika, tukiangalia sera ya biashara tunashukuru imepitishwa na Baraza, lakini inatakiwa iende na changamoto wanazokabiliana nazo wafanyabiashara katika shughuli zao za kila siku. Kwa hivyo, ninashauri hii iendane na changamoto ziliopo hivi sasa na utekelezaji wake uwe wa haraka ili kuwapunguzia usumbufu wafanyabiashara kufanyakazi zao kiufanisi zaidi.

Mhe. Spika, imesomeka kama nilivyonukuu hapa, lakini ukiangalia wafanyabiashara wetu, kunakuwa na urasimu mkubwa ambao hauleti tija. Sasa mheshimiwa ili kuyaondoa haya, ni kufuata utekelezaji ambao ni mzuri.

Kwa mfano, tukizungumzia suala la urasimu katika biashara ya Zanzibar hakuna *One Stop Centre*, kunakuwa na usumbufu mkubwa kwa mzunguko uliokuwa hauleti tija kabisa.

Mhe. Spika, mtu akitaka kufanyabiashara afanye usajili kwa msajili wa biashara mambo Msiige, akitoka hapo apitie *TRA* Mayugwani, akitoka hapo apitie *ZRB* Mazizini. Pia haitoshi, apitie Manispaa Malindi. Pia kwa wafanyabiashara wa chakula wapitie Bodi ya Chakula. Kwa hivyo, inakuwa ni mzunguko mrefu hatuna *One Stop Centre* ya kuweza kufanya mambo yetu tukayamaliza hapo hapo, ukitoka ofisi hii, ukaingie ofisi hii inakuwa ni usumbufu wa kutosha na muda unapotea.

Kama kwamba haitoshi malipo mengi au kodi nyingi za wafanyabiashara wetu hawa. Kiuhalisia Zanzibar, wafanyabiashara wanakabiliwa na kodi nyingi ambazo hazina ulazima.

Kwa mfano, unaweza ukafungua biashara ukalipia leseni kwa shilingi 300,000, hapo hapo Manispaa ulipie tena shilingi 300,000 na bado kwa wale wanaofanya biashara za vyakula inabidi walipie na bodi ya vyakula na madawa. Inakuwa mfanyabiashara huyo mtaji wake unaishia katika malipo.

Kwa hivyo, kama kweli tumekusudia kupunguza urasimu huu, basi ni lazima tuwatazame wafanyabiashara wetu, ili wapate nguvu ya kufanya hiyo biashara na ndio tutafikia shughuli ya maendeleo. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe hayo matumaini au mchanganuo wa kutosha, itakuwa vipi katika kelele tunazopiga ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nikiacha kitabu hiki, niende katika kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Mhe. Spika, katika kitabu hiki ukurasa wa 11 naomba ninukuu kama kilivyoeleza, namba I na II za kirumi.

Namba I

"Kuimarika kwa sekta ya kilimo, misitu na uvuvi ambao umekuwa kutoka asilimia 2.0, mwaka 2012 hadi asilimia 3.6 mwaka 2013".

Namba II

"Kuimarika kwa baadhi ya sekta ya viwanda kulikochangia na ongezeko la ukuwaji wa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani, kutoka asilimia 0 mpaka nukta moja kwa mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 mwaka 2013". Sawa hili ni jambo zuri sana.

Mhe. Spika, ukiangalia katika shughuli za kilimo ni uti wa mgongo kabisa katika nchi yetu. Mapinduzi ya mwaka 1964, tarehe 12 Januari ilikuwa ni kuwakomboa wakulima na wavuvi ambao ni watu wa nchi hii, na ukiangalia nchi yetu ni ya visiwa, lakini ukiangalia kama kilimo kimepewa kipaumbele mwaka jana, mara hii hatukuona hata kutajwa kwake. Uvuvi ni hali kadhalika ulitajwa kuelekea uvuvi wa bahari kuu mara hii hatuoni kutajwa je, tutafika huko tunakokusudia. Ni kuwa tukishakutaja kitu hatuna utekelezaji wa kutosha. Kwa mantiki hiyo ni lazima tujitahidi mambo tunayojipangia tuweze kutekeleza, kama hatukutekeleza yatabakia ndani ya vitabu tu.

Mhe. Spika, tunaionba serikali yetu ya Mpinduzi ya Zanzibar katika kuwaendeleza wakulima na mtu anapoitwa mkulima ni yule anayelima akapata chakula chake cha kujitosheleza, bahati mbaya yake kinachobakia akauza. Lakini leo mtu anakwenda kulima hapati chochote cha kuweza kujitosheleza yeye mwenyewe, hii ni kutokana na kutomuezesha, tunawavunja moyo wakulima wetu. Lakini tukiangalia kwenye vitabu orodha yake utasema sasa hivi nchi itaingia rutuba kubwa sana, tofauti na tunavyoandika kwenye vitabu na vitendo tunavyovifanya huku.

Mhe. Spika, tunaishauri serikali kama ni kweli inataka kufikia haya maendeleo ya kweli katika ukulima, basi ni lazima wakulima wetu tuwawezesha kwa zile ahadi tunazowapa, bila kuwatekeleza tunawavunja moyo.

Mhe. Spika, tukiangalia katika mambo ya uvuvi haya, tumesema kuna uvuvi wa kuelekea bahari kuu, lakini hivyo hivyo kabla ya kufika bahari kuu tuwaimarishe wavuvi wadogo wadogo, hatuoni kuimarika kwa wavuvi wadogo wadogo ni mambo tu kwenye vitabu. Mambo haya mpaka lini kuwadanganya wananchi. Hebu tunamuomba Mhe. Waziri kwa kupitia hapo tunaomba atupe ufafanuzi wa kutosha. Ni kitu gani unachowaendeleza wavuvi hawa

wadogo wadogo mpaka leo hii, tunawatia tamaa halafu tunawaachia njiani. Hii hatuwasaidii kitu ni kuwavunja moyo tu.

Mhe. Spika, mimi nakumbuka siku za nyuma katika kuwaendeleza wavuvi, kulikuwa kuna maduka ya *fisheries* ambayo yalikuwa yakiuzwa nyavu, mishipi, ndowana na kila kitu cha uvuvi kikipatikana pale hata mikopo ikipatikana. Lakini sasa kuna jambo gani linalowaendeleza wavuvi, naomba tusiwadanganye wananchi, kama hatuna cha kuwaambia basi tunyamazeni kimya.

Vile vile lilizungumziwa uzalishaji katika mambo ya viwanda. Lakini mimi katika mambo ya viwanda napata mashaka makubwa sana uzalishaji wake ni upi? Mhe. Spika, katika kumbukumbu hapa Zanzibar kulikuwa na viwanda mbali mbali. Kwa mfano kulikuwa kuna Kiwanda cha Maziwa kilikuwepo Zanzibar, kulikuwa na Kiwanda cha Viatu na ngozi, kulikuwa na Kiwanda cha Masufuria, kulikuwa na Kiwanda cha Sigara, kulikuwa na Kiwanda cha Makonyo, kulikuwa na Kiwanda cha Mafuta ya Nazi na viwanda vinginevyo. Viwanda vyote hivi nilivyovitaja vimeshakufa, hebu tuelezeni hivyo viwanda vinavyosaidia kukuza uchumi huo ni vipi. Namuomba waziri atakapokuja hapa atueleze kwa kina kama tunazalisha viwanda hivi, lakini ukiangalia hali halisia ni kuwa viwanda hatuna.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango katika ukurasa huu wa 16 na kifungu cha 3 kimeeleza kupanuka kwa sekta ndogo za hoteli na migahawa. Mimi nasema ni kweli mahoteli yetu yamepanuka na migahawa, kwani sasa hivi kila upitapo katika kona za miji na vijiji unakuta hoteli na migahawa. Hili nasema ni kweli na halifichiki, hatuna mashaka nayo. Lakini katika migahawa hiyo ni lazima tuiendeleze katika mazingira yaliyosafi ili kuwa kivutio, lakini kwa hili mimi naliunga mkono kuwa lipo, ni maendeleo tunashukuru.

Mhe. Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 12 katika kifungu cha V cha kirumi, naomba ninukuu hapa kimeandikwa;

"Kuendelea kwa hali ya amani na utuvuli nchini".

Mimi nasema kuhubiri jambo hili ni jema sana. Lakini niseme sio kutamka ndani ya vitabu tu, tunapohubiri ndani ya vitabu au tukisimama juu ya majukwaa tukahubiri kauli hizi ni njema, wananchi wetu tunawapa mshikamano wa kushikamana katika kujenga amani. Mimi nasema amani iliopo nchini ni amani ya ukomavu wa wananchi wa Zanzibar na Tanzania nzima kwa ujumla na hii ni hidaya ambayo Mwenyezi Mungu ametuletea, lakini tukiangalia kauli za viongozi wetu zinatua mkozi kweli kweli.

Kwa mfano, Mhe. Spika, mimi niseme kwa uchungu kabisa tunazungumzia amani, lakini kiongozi wa juu anaweza kusimama akatoa kebehi na akadharau, unapomkebehi mtu ni uvunjifu wa amani. Mimi nataka ukae na mwenzako umkebehi na umdharau hatma yake itafikia vipi.

Mhe. Waziri aliyezungumza katika kitabu hiki Mhe. Mwinyihaji Makame mimi ni mzee wangu namuheshimu sana na nitaendelea kumuheshimu, lakini wakati mwengine anapotukebehi kwa mambo kama hayo, basi tunakosa busara sana. Kwani ukimuangalia ni mtu mzima na ukiangalia hekima zipo, lakini anapofika katika viriri anababaika na nini sijui.

Nchi yetu sasa hivi iko katika mchakato wa kupata katiba mpya na mchakato wa katiba mpya ni jambo ambalo linataka utulivu na amani kama nilivyolizungumzia. Lakini Mhe. Mwinyihaji Makame alipokuwa akichangia kule ametukebehi sana hasa wapinzani, wanaotaka Zanzibar huru, pamoja na mamlaka kamili.

Leo huyu anathubutu kutuambia kama hata neno mkataba hatuwezi kutamka, tunatamka nkataba ni jambo la kujejea. Tunaomba kama Mwenyezi Mungu alimjaalia akakosea kwa ulimi tu kuteleza basi arudi, mambo kama yale asifanye ni kebehi kubwa kwa kiongozi mkubwa kama huyo. Mimi namuomba Mwenyezi Mungu amrudishe alikotoka, lakini ile ni kejeli kabisa aliyotukejeli hasa Wapemba.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe una dakika tano na urudi kwenye hoja ilioko mezani.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante. Kwanza tunawaomba viongozi nyinyi mnaposimama ndio wa kutueleza musipotee njia mkafuata vijana wanaoingia sasa, namna kama ile unaturudisha nyuma. Leo tunataka amani na

utulivu, unahubiri kitu kama kile, utaupata wapi utulivu. Nawaombeni sana viongozi nyinyi ndio wa kutuongoza, mkisimama kwenye viriri msipagawe kama vijana.

Mhe. Spika, mimi nasema naishia hapo na Inshaallah mawaziri wote tunataka majibu mazuri ili kutuunganisha sio kutugawa. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na kama muda utakuwepo tumsikilize Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza mimi naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mchana huu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha. Pia Mhe. Spika, nikushukuru tena kwa kuchaguliwa katika Bunge Maalum kuwa Mwenyekiti wa muda na kuendesha vizuri kabisa na kwa sifa nyingi, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais Dk. Ali Mohamed Shein, kwa juhudi zake kubwa alizochukua kwa kuimarisha miundombinu na sekta zote za jamii katika nchi yetu ya Zanzibar, namshukuru sana.

Pia Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa juhudi zake kubwa kabisa pamoja na watendaji wake wote wanaosaidiana naye kazi katika wizara hii kubwa na mama katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Vile vile Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa juhudi zake kubwa kabisa kuisoma ripoti yake ile na kwa maelezo mazuri kabisa na yenye nia njema katika nchi yetu hii ili kuboresha sekta mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi nianze katika ukurasa namba 42 hotuba hii ya Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 42 kuhusu ushuru wa stempu. Mhe. Spika, kama unavyojua nchi yetu bila ya kutoza kodi hatuwezi kuendesha nchi yetu, kwani kodi ndio inayoendesha kila kitu. Mwalimu Nyerere alisema nchi iliyokuwa haitozi kodi basi hiyo nchi itakuwa *corruption* kabisa Mhe. Spika. Kwa hivyo, mimi nampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi zake kubwa mbali mbali za kutoza kodi.

Nianze na kodi hii ya ushuru wa stempu wa *Airport*. Mhe. Spika, kama unavyojua ushuru huu wa stempu zetu za *Airport* hauko sawa kiasi hicho, kwani ukitizama kodi hizo mpaka leo mgeni analipa dola 40, lakini dola 40 hizo unapewa kipande kidogo kama karatasi au risiti, hakipo katika utaratibu mzuri. Lakini tukitizama mfano mzuri kabisa Shirika la *Precision Air*, unakuta mpaka leo ukienda pale unalipa 11,000/= kidirishani pale ambapo mambo yameshapitwa na wakati miaka mingi nyuma. Sasa hivi kodi za uwanja inakuwa mara nyingi unalipia kwenye tiketi, lakini cha kusikitisha shirika hili haliwezi kutoa pesa na linadaiwa pesa nyingi sana. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri suala hili ulishughulikie kwa maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile kodi hii ya bandari ya shilingi 2,000. Mimi nawaomba hawa wasafiri na wafanya biashara mbali mbali wawe wanalipa kodi, sio wanakwenda Tanzania Bara tu, bali sehemu mbali mbali wao wanalipa kodi sio Tanzania bara tu bali sehemu mbali mbali wanazokwenda, walipishwe kodi hii ya 2000 kwa hivyo inasaidia sana kwa ajili ya nchi yetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nije kwenye ukurasa wa 40 Kodi ya Ongezeko la Thamani, la misamaha ya kodi ya hoteli VAT. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa nia yake nzuri na njema kabisa ya kuongeza mapato, lakini mimi niseme kidogo Mhe. Spika, suala hili kidogo linaleta kigugumizi hapa kwani misamaha hii inayotolewa iangaliwe vizuri.

Mhe. Spika, wazalendo wenye hoteli zetu hapa Zanzibar unakuta wanalipishwa kodi gharama zao ni kubwa. Kuna wafanyakazi, kuna umeme, kuna kodi ya Serikali, kuna uendeshaji wa hoteli ile lakini misamaha ile mara nyingi wanakuwa wanapata wale wawekezaji wakubwa wakubwa ambao wanatoka nje ya nchi.

Kwa hivyo naomba Mheshimiwa Waziri hili uliangalie sana, uwape kipaumbele sana wazalendo wa nchi hii waliokuwa na hoteli ambao wanaajiri wananchi wetu wengi na kipato chao cha chini, kwa hivyo hawa naomba waangaliwe suala la kodi vizuri ili waweze kujikwamua na maisha magumu na uendeshaji wao wa hoteli, kwani wazalendo wana kazi kubwa na pesa yao au mtaji wao ni mdogo Mheshimiwa Spika. Pia wawekezaji wakubwa waangaliwe misamaha yao isiwe mikubwa, kwa sababu wanakuja na fedha nyingi kuwekeza kwenye nchi yetu, sio wanakuja kutusaidia, wanakuja kuchuma pesa na kufaidika kwa maslahi yao zaidi. Kwa hivyo naomba hawa wakija Mheshimiwa Waziri awaangalie vizuri na kodi yao iwe nzuri na halali kabisa iweze kulipwa.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 11 wa kitabu hiki cha bajeti cha Makadirio na Mapato, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na nawapongeza sana ndugu zangu wa *ZRB* kwa kazi yao kubwa sana wanayoifanya kwa kukusanya kodi hii, kwani ukitizama kila mwaka wanajitahidi kuongeza kodi kupita mwaka jana na mwaka huu wamezidisha kipato cha kuweza kukusanya mapato yetu. Mwaka huu kwa kitabu kinavyosema wameweza kukusanya karibu bilioni 171.9 bilioni, kwa kweli hizi ni pesa nyingi sana wameweza kukusanya kwa wafanya biashara wetu mbali mbali wa hapa Zanzibar, lakini naamini wanaweza kuongeza mapato hayo, nawashukuru sana na kazi yao kubwa.

Pia niwashukuru hawa ndugu zetu wa *TRA* kwa kukusanya bilioni 147.9 kwa kweli nawapongeza sana kwa nia yao njema sio kwa nia mbaya. Mhe. Spika, mimi niseme suala moja hapa ambalo linanitia wasi wasi na gugumizi kubwa, hii kodi ya *TRA* ambayo wanalipishwa hapa ushuru wa bidhaa unakuta hapa mwananchi analipishwa kodi kama kawaida, lakini akichukua mzigo ule ule atoke hapa aende bandarini Mheshimiwa Waziri analipishwa tena na anasumbuliwa sana, mimi mwenyewe nimeshaona hali halisi ilivyo hata uchukue kitu chako binafsi wewe mwenyewe cha kutumia mfukoni utapekuliwa na utaambiwa ulipe.

Nashukuru sana kwa kusikia hata kwenye TV Bungeni lilizungumzwa suala hili na ushuru wa bidhaa hizi wananchi wanatoka Zanzibar waondoshewe kero hii. Kwa hivyo nakuomba uliangalie kwa wafanyabiashara wote wadogo wadogo, wanahangaika kutafuta rizki kule Dar es Salaam kwa kuuza vitu.

Naomba hawa waondoshewe hii kodi kabisa, wasisumbuliwe kwani kodi hii ya *TRA* wamekusanya hapa bilioni 147.9 zinatoka wapi hizi fedha, hizi bidhaa zinazolingia pale zinalipishwa kodi, sasa kama hawaridhiki na kodi hii Mheshimiwa Waziri waongeze kodi hii, mzigo ukienda kule Dar es Salaam wawaachie.

Mhe. Spika, saa nyengine Serikali ina nia njema kwa wananchi wake lakini watendaji pale bandarini wanafanya zile fedha zinakuwa zao kwenda mifukoni mwao, kwa hivyo naomba Serikali iangalie kwa uzuri na kwa kina kabisa kufuatilia hawa wafanyabiashara wetu wasisumbuliwe wakienda kule bara. Wananchi wetu wanyonge rizki zao zinatokea hapa kwenye biashara hii, na kule wakienda wanasumbuliwa lakini naamini kwa Serikali zetu mbili hazina nia hii ya kuwatoza wananchi wetu kodi na kuwasumbua. Lakini watendaji pale bandarini hawana nia njema na nchi zetu na Serikali zetu mbili hizi Mhe.Spika.

Nije kwenye hili deni letu la taifa ukurasa wa 50. Mhe. Spika, kufikia mwezi wa Machi, 2014 deni la Taifa limeongezeka hadi kufikia bilioni 294.9 sawa na asilimia 17. Mhe. Spika, hili deni ni kubwa sana na sisi kulilipa itakuwa ni vigumu itachukua muda sana kulilipa, lakini nashukuru sana Serikali yetu ya Muungano na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kutudhamini kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa jumla ya asilimia 88. Mhe. Spika, mimi nafarijika sana kuona kitu kama hicho hapa kwenye bajeti hii na wadhamini wakubwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwani hawa ndugu zetu wanatuamini, na wanajua umuhimi wa fedha hizi kwa ajili ya maendeleo.

Kwa hivyo nawashukuru sana ndugu zetu hao kwa kutusaidia kwa asilimia 88 kwenye deni hili la milioni 294.9, nawashukuru sana kwa juhudi zao kubwa na kwa muungano huu wa kindugu na wa kuaminiana kabisa.

Mhe. Spika, nije maeneo ya kipaumbele ukurasa wa 55 kama tunavyoona Mheshimiwa kwenye ukurasa wa mwanzo wa deni la taifa, tuna deni la milioni 294.9 kwa Serikali yetu, lakini na hivi vipaumbele Mheshimiwa Spika, kwa watendaji wetu wakati mwingine nasikitika sana mambo mengine yanafanyika kwa watendaji wetu wanatuharibia kwa makusudi, nia njema ya Rais wetu na Wizara zetu, lakini unakuta watendaji wetu saa nyengine wanatuharibia hawakai wakaangalia vipaumbele vifanywe kwa nia njema na kuleta maendeleo kwa jina la nchi yetu.

Mhe. Spika, huduma za afya ukiangalia katika kipaumbele hiki ukiangalia hapa kuna nia njema kabisa, lakini utakuta utendaji sio mzuri Mheshimiwa Spika, unakuta hali haipatikani ile sekta ikawa imekamilika kama Serikali ilivyokuwa inataka, na hapa tatizo kubwa lipo kwa watendaji wetu, nasema wafuatiliwe zaidi na kwa undani kabisa.

Tukija kwenye suala la maji safi na salama, kuna matatizo mengi sana katika nchi yetu ya Zanzibar maji safi na salama unakuta pesa hizi tunapata miradi, pesa za mikopo tunapata kwa wafadhili, lakini unakuta miradi haiendi inavyotakiwa vizuri. Tuseme mfano sasa hivi, ukitizama sehemu nyingi za miundombinu za mabomba ya maji ni mabovu, maji yanapotoka sehemu husika kufika sehemu husika yameshapotea mengi sana. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa Spika, tuangalie kwanza miundo mbinu hii tusiwe tunafanya miradi tu, lakini miundombinu mibovu, kwa hivyo naomba tuangalie sana mabomba haya ya maji yanayoleta sehemu husika za maji.

Mhe. Spika, sasa tuje kwenye hivi vipaumbele tunavyosema, nashukuru sana *Airport* yetu inajengwa vizuri, *apron* inakwenda vizuri *runway* na ukija kwenye *terminal* Mhe. Spika, hapa kidogo kuna matatizo, lakini hivi fedha kama alivyosema za mikopo naomba tuangalie makosa yanapotokezea basi tusirudie makosa hayo hayo kila siku, kwani hizi pesa ni mikopo ya wananchi na inatakiwa tulipe.

Kwa hivyo naomba tuangalie makosa kama ya *terminal* yale yasitokezee, mpaka leo *terminal* ile haijamalizika, wataalamu tunao tukae nao chini tupate kupata uhakika vizuri wa kufanya kazi zetu ili Serikali yetu kwa nia njema kabisa na wananchi wake wa Zanzibar wapate maendeleo. Kwa hivyo naamini Mhe. Spika, hapa tukifanya vizuri tunafanikiwa vizuri kabisa kwenye miradi yetu ambayo tunachukua fedha hizi za mikopo hizi.

Nije kwenye miundo mbinu ya barabara, nitoe mfano mdogo tu bara bara zetu zinakuwa zinatengenezwa lakini nikitoa mfano mdogo uhakika kabisa, juzi juzi katika jimbo langu la Bububu kulitiwa kifusi namshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuliona hilo tatizo kubwa, katia kifusi kwa milioni nyingi sana fedha za serikali, lakini nashangaa kifusi kile mpaka leo kinaharibika, mashimo yanaanza tena, kuwa gari hazipiti mvua za juzi mashimo, magari kupita yanakwama pale. Sasa hivi fedha naona zinapotea kwa muda wa mwaka mmoja kutiwe tena kifusi.

Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri uliangalie hili tumetia kifusi tumalize lami ili kuondosha hili tatizo nakuomba sana hizi fedha tusizipoteze kama zilizokuwa hazina mwenyewe, wakati hii ni mikopo na tunadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wenzetu, mwisho watachoka hawa wenzetu kutusaidia watakuwa wanatuona sisi sio watu wa kuona maendeleo mazuri katika nchi yetu.

Mhe. Waziri namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuwapa wazee wasiojiweza kipaumbele, naomba hili suala liendeleo, lakini cha ajabu hawa wazee sijui wanafaidika vipi katika kupaumbele naomba kidogo ukija uweke utaratibu mzuri hawa wae kuhakikisha wanafaidika katika hiki kipaumbele ulichoweka, na washukuru katika hali hii kwani maisha yao ni magumu sana.

Mhe. Spika, suala la watoto pia lina matatizo makubwa hasa ukija kwa wanafunzi wana tatizo la usafiri, wana tatizo la *uniform* wana tatizo la viatu na mabuku yote Mheshimiwa Waziri hawa watoto yanawakabili, lakini nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri mara hii kama mjumbe aliyetangulia alisema safari hii umetuongeza pesa za jimbo angalau milioni ishirini, mimi nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tuna matatizo mengi katika majimbo yetu. Kwa hivyo zitasaidia kutatua matatizo haya madogo madogo ya watoto wetu wa skuli. Kwa sababu hawa watoto wakisoma sisi tutafaidika kwa kuwa tutapata viongozi wazuri kesho. Tusidharau suala hilo Mheshimiwa Waziri kwani nimekuona kwa moyo wako mzuri kabisa na nia njema kabisa uliyokuwa nayo.

Pia Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa kuwasaidia kwani watu hawa ni muhimu na wana shida sana Mhe. Spika, na Mheshimiwa waziri kwa kuliona hili nakushukuru sana na Mungu atakusaidia na uzidi kuona kitu muhimu sana kuwasaidia watu hawa wenye ulemavu.

Mhe. Spika, nimalizie suali la mwisho kabisa, suala la ajira na umeliweka kwenye kipaumbele ajira kwa vijana, lakini nasikitika suali la ajira sasa hivi ni gumu. Vijana wetu hawana kazi wengi, sijui umepanga vipi kuwasaidia vijana katika ajira, lakini mimi niseme suala moja kwa Serikali yetu yenye nia njema kutoka kwa Rais wetu Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutafuta wawekezaji na kuwapa moyo wawekezaji hao.

Nitoe mfano kama muwekezaji huyu mmoja huyu Said Bakhressa mfanya biashara maarufu kabisa, mimi namshukuru sana sana na Serikali yetu ikiwa na mashirikiano mazuri na yeye kuwekeza katika viwanda kama hivi, kwa mfano kiwanda kimoja kilichopo Fumba cha maziwa tunaambiwa karibu kitaanza kazi zake. Juzi juzi nimesikia anataka kuajiri watu 250 kwa sehemu tofauti vijana wapate kufanya kazi hapa. Kwa kweli hii ni hatua kubwa sana kwa mfanyabiashara huyu kuweza kuweka kiwanda hapa, tupate wawekezaji kama hawa kama wanne au watano nafikiri ajira kidogo itakuwa ipo sawa katika nchi yetu.

Kwa hivyo mimi nampongeza sana mfanya biashara huyu Said Bakhressa na Serikali imuone kila inachoweza kumsaidia imsaidie kwani mfanya biashara huyu ni muhimu sana katika nchi yetu, kwani huyu akiwekeza atakuja na mwengine Mhe. Spika, watakuja kuwekeza ili kuona faida katika nchi yetu na kufikia malengo ambayo tunataka vijana wetu wote wapate kazi na wasikae tu mitaani wakawa hawana cha kufanya.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi naunga mkono hotuba hii ya Waziri asilimia mia kwa mia. (*Makodi*).

Mhe. Spika: Nilisema kama muda utakuwepo nimkaribishe Mheshimiwa Mwanajuma Faki Mdachi ambae naona simuoni. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa jioni tunategemea tuwasikilize kwanza Mheshimiwa Mwanajuma Faki Mdachi, halafu atafuata Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk, baadae Mheshimiwa Mwanaidi Kassim Mussa, Mheshimiwa Moh'd Mbwana Hamad, Mhe. Moh'd Haji Khalid, na hatimae tumsikilize Mheshimiwa Saleh Nassor Juma, niwaombe wote hawa wafike mapema ili tuweze kuendelea na mjadala wetu. Tusitishie mjadala wetu hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliakhirishwa mpaka Saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa majadiliano yanaendelea nafasi ya kwanza jioni hii ilikuwa ya Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi hayupo naomba basi nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, mimi nianze kuingia katika ukurasa wa tisa huu ambao unaeleza, Mhe. Waziri wa Fedha wa Zanzibar alitoa maelezo yake mazuri kwa furaha kabisa, alisema kuwa naomba ninukuu kidogo tu.

“Mhe. Spika, la tatu nina furaha ni la kuteuliwa Waziri mpya wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Waziri ambaye namfahamu sana kutokana na ufanyaji nae kazi huyu kijana na ni msomi na ni mchapa kazi”.

Hata hivyo hakusema kama ni mzanzibari hapa sijaona, lakini naomba sana furaha hii Mhe. Spika, hata mimi nilikuwa nataka nifurahi sana. Kwa sababu kila sehemu ambayo yenye neema katika Jamhuri ya Muungano kule inakuwa sisi wazanzibari tunategemea kupata faraja kubwa sana. Mheshimiwa nilikuwa na furaha hiyo tu, lakini undani sijaona kuwa furaha ile kuwa huyu mwenzetu ambaye katika mashirikiano nae na wewe unavyomjua utendaji wake wa kazi labda kuna mambo kakusaidia, naomba sana Mhe. Waziri njoo unieleze kuwa katika furaha yako hii kuna mambo ambayo amekufurahisha zaidi sio karibu tu kukaa nae na kuna mambo ambayo yamesaidia kwa kuchangia katika upande wa Zanzibar, naomba sana Mheshimiwa hili uje kunisaidia kunieleza.

Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri na hii ni mara nyingi sana anapotoa hotuba yake ya bajeti ninamshukuru sana kwa kusema kuwa uchumi wa Zanzibar umekuwa. Lakini wananchi hawafahamu Mhe. Spika, ukuaji huo wa uchumi ukoje na hili tatizo siku nyingi sana kuwa tunakuja kulizungumzia katika Baraza hapa, lakini wananchi hatuwaelimishi, wananchi hawapati taaluma, hasa katika vitongoji na shehia, sababu waheshimiwa hawafahamu jinsi gani kukua kwa uchumi wa nchi.

Wanakwambia wananchi kweli uchumi wa Zanzibar umekua lakini vitu vinapanda bei, anakusomea mwananchi huyo mishahara hakuna, sasa anajiuliza mwananchi, dawa hospitali hazioni, anajiuliza mwananchi, kodi zinapanda leo na kesho, anajiuliza kukua kwake uchumi Mheshimiwa tusione tabu ya kuwaelimisha wananchi wetu wakafahamu jinsi gani uchumi unavyokua Zanzibar. Wanakwambia uchumi unakua kwa juu tu, kumuona Waziri kapanda zuri, Katibu Mkuu kapanda gani zuri, Katibu Mkuu ana mishahara mingi, Waziri ana mishahara mikubwa labda hiyo ndio wanafahamu kuwa ndio kukua kwenyewe huko.

Sasa mimi ningeomba sana Mhe. Waziri hili suala tuweze kutoa semina kwa wananchi kabla hatujapitisha bajeti, tuwaelimishe wananchi wala tusipate tabu tuna shehia zetu na hili kama tutaweza kufanya Mheshimiwa wananchi, basi wasingepata tabu sana. Lakini tatizo letu tunadharau tu kuwaelimisha wananchi. Hata na mimi mtaalam ninapata shida kukua kwa nchi kwa sababu bado sijaona kuniwezesha huu ukuaji wa uchumi Zanzibar kwenye mapato, bado mimi sijaona kabisa.

Mhe. Waziri hebu nambie una kipato gani kikubwa ambacho kianzio kinachotoa tija kubwa sana hebu naomba njoo unieleze, katika hivyo vianzio vyako vyote ni kianzio gani hasa wewe Mheshimiwa wewe unategemea, hata ukasema leo ukenda kifua mbele ukasema kama uchumi wa Zanzibar umekua hebu nambie kama unacho hicho.

Mara nyingi sana ukusanyaji wako unafika mpaka bilioni nne na *something* juu. Lakini mara hii unaniambia mpaka una milioni mia saba na hizi sijui umezipata wapi, Mheshimiwa hebu njoo unambie. Mhe. Spika, naomba mimi anieleze amepata pata vipi hata akafika leo kunambia ana bajeti yake na ina-cost milioni 700, ninanukuu na vitu vyengine vidogo vidogo juu. Ninaomba sana hilo Mheshimiwa Waziri ili uje kunieleza hali halisi ilivyo.

Waheshimiwa kusema ukweli hali halisi ilivyo ni nchi ndogo sana hii Zanzibar lakini ni nchi ambayo mimi nilitegemea tusiwe hata katika *second world* tuwe katika hii *East African* yetu tu, tuwe angalau nchi aidha tumechelewa basi tuwe wa tatu katika utajiri, kutokana na hali halisi mandhari ya kisiwa chetu kilivyokuwa kizuri Mhe. Spika, kutokana na hali ya uchumi wetu ambao tuliokuwa tunao sijui tunauklia au tunaubeza, nashindwa kufahamu. Ninaomba sana Mheshimiwa tujenge sifa, tujenge taaluma iliyokuwa ya uhakika kabisa, mimi Mheshimiwa nina wasiwasi sana.

Mhe. Spika, sikufuru kwa Mwenyezi Mungu lakini ningesema suala kama kusema Dkt. Shein ananisikia basi katika nchi hii na mimi ningeweka historia wala si bwana uchumi, sina sifa ya uchumi, lakini nina akili ya uchumi. Kwa sababu kuna vitu ambavyo kama tutaweza hasa kikweli kweli, kisawa sawa Mhe. Spika, basi ninakuhakikishia Zanzibar mishahara wa mwanzo tungeweza kulipa shilingi 300,000/= na kuendelea mbele, tungeweza kabisa. Siutaki uwaziri wa Fedha lakini afanye masihara tu Mheshimiwa sasa hivi anipe Wizara iliyo ngumu halafu nimuonesha Mhe. Sheni si mchezo kwa sababu mawaziri wengine nitasema ni mzigo kwa sababu hawajaonesha mfano kuleta uchumi Zanzibar, kwa sababu kuna vitu bado tunavichezea chezea Mheshimiwa wangu Spika.

Mhe. Spika, nimeona hapa Mheshimiwa wangu anasema kuna mambo ambayo ameyapa kipa umbele, sasa tatizo letu kubwa hawa wataalam wanavyonishughulisha mimi akili yangu tunabuni miradi mingi ambayo ni muhimu sana kwenye ukurasa wa 26, mimi naomba kwa fikra zangu afya ni muhimu kwa binaadam Mhe. Waziri lakini afya Mheshimiwa bado hatujawa *serious*.

Mimi naomba sana Mheshimiwa hata zile pesa tunazokusanya hebu tuachieni tuwape wenyewe waendeshe, vipesa vidogo sana Wizara inataka nini pesa zile, zile pesa ni ndogo sana Mheshimiwa Waziri hata mfukoni hazijai vijipesa kidogo tu, Mhe. Spika, waachiwe wenyewe zile pesa za baiskeli, hata zile zende Hazina, mambo mengine jamani tuyafikirie, tuachieni wenyewe Wizara ya Afya wazitumie zile fedha.

Jana walipata ajali wananchi wangu kama watano, sita, saba nimekwenda dawa hamna haki ya Mtume ninakwambia Mhe. Spika. Jana usiku saa 5.00 nilikuwa hospitali, vijana wangu wanatoka kwenye mchezo wakapata ajali. Na dawa zenyewe utacheke, panadol nimekwenda kununua nje mimi, halafu leo unanambia Mheshimiwa uchumi umekuwa. Ninaomba sana Mheshimiwa tuzibe mapengo tuachie wenyewe watu wa Wizara ya Afya.

Ninataka mradi mwengine kuharakisha upatikanaji wa ajira bora kwa vijana. Mheshimiwa ajira bora kwa vijana hatujawa *serious*, hebu tutengenezeni, mimi ninashangaa sana Mhe. Waziri umefungua Chuo kule cha Chwaka, mimi ninakushukuru sana ninakwambia, lakini kakifunge kile Chuo. Kwa nini nikakwambia ukakifunge, kwa

sababu tayari umewasomesha watu lakini utakuta kuna watu wanatoka nje *course* zile ulosomesha pale wana uwezo wa kwenda kufanya hawapati kazi Mhe. Spika, hawapati kazi kabisa vijana wetu.

Leo *foreigner* analipwa *per day* tu shilingi 500,000/= na wengine wanakuja kufundishwa hapa hapa kazi. Tatizo lenyewe linalouma Mhe. Spika, wanakuja kufanyiwa *training* hapa hapa halafu anafanywa kama TX hatujawa *serious government* Zanzibar. Vijana wetu wanahangaika bure Mheshimiwa tunapiga kelele wanakula unga, wasile unga! Watakula unga, wasiwe wizi, watakuwa wizi, hatujawa *serious* katika kuwajengea hii ajira bora tunaisema tu kwenye vitabu Mhe. Spika.

Nimetoa mfano jana na Mheshimiwa wangu Mhe. Haji Omar Kheri, ninamshukuru sana kanionesha jitihada ya kutaka kufanya, jamani tumuige mwenzetu Jakaya Kikwete amesema watu mzigo kama ule wasiwepo hapa wafutiwe vibali. Mheshimiwa Waziri tuna hasara gani, unakosa mapato wewe hujui mapato gani unakosa, ndio nikakwambia mimi mtaalam musikilize kuna mambo ambayo ma-*foreigners* wengine hawalipi kodi, wewe hujui Waziri.

Halafu mimi ninashangaa sana nitafanya challenge siku moja aidha Waziri au Naibu Waziri mmoja tu aliyetembea katika sekta zake, kama yupo mimi nitamlipa shilingi elfu kumi. Hawaendi hawa katika sehemu zao kuangalia jinsi gani watu wanavyopata shida, hawaendi hata siku moja. Mapato yanavuja Mheshimiwa wewe hujui, mapato yanapotea ma-*foreigners* wapo kibao huko wanapata pato zuri sana.

Mheshimiwa tuje katika kiwanja chetu cha ndege, Mhe. Spika, tulitoa zabuni hapa tukasema kuwa twende katika *international air port* ili Zanzibar tuweze kupata mapato mengi, watalii waje lakini kumbe kazi yetu kupandisha kodi tu sio kutafuta vianzio, ndio nilichogundua hiki kitabu chako Mhe. Waziri. Imeletwa *tender* hapa lakini tenda hiyo Mhe. Spika, mpaka leo sijui imefikia wapi, imekufia wapi. Lakini kama Serikali imemuona kuna muekezaji anafaa kwa nini mnalaza damu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri aje anipe jibu hapa nani ambae aliyefaa ili tupate neema katika nchi hii. Tunakwenda na mambo ya sasa hivi ya kitaalam bwana, tuwapeni watu waliokuwa tayari wana uwezo, wana fedha zao na nchi yetu ndio maana nikakwambieni hamko *serious*. Kwa sababu njia ya kupata mapato ziko njia nyingi Mheshimiwa, tuna *delay* katika masuala ambayo ya kupatia mapato.

Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri hilo nalo najua utakuwa si mzigo wako lakini moja katika kianzio cha kupata mapato njoo unijibu ni moja katika kupata mapato. Kwa sababu leo ungepata mtu ambae mwenye uwezo ile *air port* sasa hivi kungejaa sana pale. Ninaomba sana hilo Mheshimiwa, hili nitakuja kulisema wakati wa Wizara yake husika Mheshimiwa.

Mheshimiwa tukienda katika masuala ya pembejeo, kwa kweli kuna wanancnhi ambao hasa wa Pangei na Kilombero wameikopesha serikali lakini mpaka leo hawajalipwa, uchumi umekuwa wapi Mhe. Spika. Ikiwa leo mtu mdogo kabisa ameikopesha Serikali kwa lengo na madhumuni ya kuweza watu waendeleo katika kukuza kilimo, mpaka leo tunawahangaisha *budget to budget, budget to budget* watu hawajalipwa, mimi sikubaliani nalo Mhe. Spika, sikubaliani kabisa kama uchumi wa Zanzibar umekuwa ninakataa, *unless* aje kunifahamisha jinsi gani uchumi huo umekua hata yule mtu wa Kilombero na Pangei amepata pesa zake katika kukopesha mbegu za pembejeo zakuweza kulima. Mheshimiwa hili suala ninasikitika sana.

Mhe. Spika, mimi ninasikitika sana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mheshimiwa ninasikitika sana leo kodi za wenye magari kupasisha, Mheshimiwa, mimi ninaona haya hata kusema kuziunga mkono kwa sababu Mhe. Spika, wenye magari ni maskini ya Mungu, gari una-*risk*, leo tunakwenda kumwambia atoe pesa ya kodi ya kupasisha wakati tuna njia nzuri tu ya kuweza kupata mapato makubwa. Mheshimiwa ninafikiria sasa hivi tutafute viwanda vikubwa vikubwa.

Mhe. Waziri nimekuamini sana sijui kwa nini unachelewa, kuna makampuni mpaka leo hii ninashukuru. Kuna Kampuni moja ya umeme sasa hivi *SACRONA* wakati wowote inaweza kuwa tayari na *inshaallah* ikaleta baraka

katika nchi hii ikaongeza nayo kupata kodi, haya ndio tunayoyataka bwana, tulete makampuni ambayo yatakayoweza kutia kodi kubwa, sio mwenye gari anakwenda kupasisha anatolewa leseni anatozwa pesa chungunzima. Gari yenyewe watu, wenyewe kidogo, watu wenyewe 40, leo tunamuwekea kodi huyu jamani aa Mheshimiwa naomba sana, fikiria sana Mheshimiwa.

Hawa wataalam wasikwambie na kesho ndio hawa hawa, na hawa hawa ndio wenye vigari vyenjewe hawa hawa. Lakini tunatunga sheria hawajui kama baadae ile sheria itatugeukia sisi wenyewe. Leo miaka mitano inakwisha tunakaa pembeni hapa, wewe una kigari chako ndio utaanza kulani sasa pale ndio utaona Mhe. Spika, joto la jiwe, umepitisha sheria ngumu halafu leo sheria ile inakukwaza wewe sasa. Mimi ninaomba sana Mheshimiwa tulifikirie jamani tusivitafute vyanzo vidogo vidogo tukawaumiza wananchi. Hili suala kwa kweli Mheshimiwa linaumiza sana.

Nimalizie Mheshimiwa kabla hujakuna kichwa, Mheshimiwa ninakubaliana na suala moja kutokana na hali halisi sasa hivi kuwa kama alivyoeleza Mheshimiwa wangu pale nilimuhurumia sana Mhe. Mohammed Aboud, Mhe. Waziri hizi fedha ambazo ningeomba sana Mhe. Waziri akaziangalia fedha za sherehe ambazo na yeye ofisi yake s inakuwa ndogo, lakini ofisi ile ikiingizwa *time* nyengine kwa shughuli nyengine tayari inaonekana kama na yeye amefaidika, wakati ile ni Wizara yake kubwa sana.

Sasa mimi ningefikiria na yeye akatafutiwa *means* fuko lile likawekwa katika njia nyengine au likapelekwa kule kule kwenye sherehe za mapambo ili na yeye akaweza kunufaika na hiyo AC kwa kuwasaidia wananchi, kwa sababu Wizara yake ni kubwa sana. Wizara yake ina wananchi karibu nao sana pamoja na waheshimiwa wenyewe kwenye mfuko wa jimbo uko pale pale Mheshimiwa. Sasa mimi ningeomba sana tuweze kumsaidia mwenzetu kwa kumtafutia *means* ya kuweza na nini na hizi fedha tuziondoshe katika mambo ya maendeleo tukazitafutie sehemu nyengine ya kuziweka fedha hizi ili zisiingie katika mambo ya maendeleo pesa za jimbo hizo.

Mheshimiwa nimalizie la mwisho, Mheshimiwa ninaomba Mheshimiwa Katibu wako, na Manaibu Katibu na Wakurugenzi wako, *serious* si kitu cha masihara, Mheshimiwa sasa hivi kwenye mahoteli kunapigwa bao pale, hebu fanya siku moja tu *operation*, anzia kusini ishia kaskazini, uone jinsi gani utavyokusanya mapato, halafu uone kifua mbele utapoweza kuwapandishia mishahara wananchi, naomba sana nenda.

Kuna watu ninavyokwambia hawalipi kodi na kuna watu wanachezea kodi, mimi nakubaliana na wewe kwa huo mfumo wa *international* hiyo mashine nikubaliane na wewe kabisa kuwa tayari hiyo iletwe ili ioneshe mapato yetu jinsi gani yanavyokwenda. Mhe. Waziri nimshukuru sana kwa hili na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akubariki na kila la kheri.

La kumaliza Mhe. Spika, kulikuwa na mradi mmoja wa Chelezo, mwaka jana niliusema na wewe ukasimama kifua mbele hapa Mhe. Waziri, yule ni mwananchi mzalendo, na hawa wazalendo tunapenda sana kuwakorofi sijui kwa nini. Wazalendo wenyewe wanataka kuweka chelezo ambacho kitaajiri wananchi si chini ya 300, kitatia kodi, naomba sana hili suala Mhe. Waziri alisimamie sasa hivi huyu mwananchi na yeye ajisikie huru katika nchi yake.

Mhe. Spika: Mheshimiwa ahsante sana muda wako umemalizika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nashukuru Mhe. Spika, ahsante sana naka kitako.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa jioni ikiwa ni mara ya kwanza katika Baraza hili kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora pamoja na ile ya Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nachukua nafasi hii ya kuchangia kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame. Nitaanza na ukurasa wa pili *paragraph* ya pili.

Mhe. Spika, ukurasa wa pili *paragraph* ya pili inasema kwamba, "Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kukutana tena hii leo katika Kikao cha Kujadili Hali ya Uchumi mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015. Tunaomba Mwenyezi Mungu akijaalie kikao hiki kuendesha kazi zake kwa amani, usalama, utulivu na upendo kati yetu".

Mheshimiwa maneno haya ni maneno mazuri, ni maneno makubwa, ni maneno ya msingi, kwa sababu tunaomba dua hii kwa Mwenyezi Mungu ili atupe hekima. Hekima ni kitu kikubwa sana, na nataka nizungumze umuhimu wa hekima katika Mabaraza yetu likiwa Baraza hili la Wawakilishi na Mabaraza mengine ambayo tunaungana nayo.

Mhe. Spika, hekima Mwenyezi Mungu ameitaja kwamba ni miongoni mwa mambo ya kheri yaliyo makubwa, nafikiri nikikariri maneno ya Mwenyezi Mungu anasema: "*Waman yuuta l-hikmata, faqad-uitiya khairan kathiira*", wale waliopewa hekima hakika wamepewa kheri zilizo nyingi na kubwa kabisa. Naliomba Baraza lako na viongozi mbali mbali waliopo hapa katika mazungumzo yetu mbali mbali tuliyonayo hapa na kwengine, hekima itawale vikao vyetu, ili hiyo kheri iliyo kubwa ipatikane, kinyume na hivyo basi tutakwenda kinyume na taratibu za kupata hiyo hekima na tutazikosa hizo kheri ambazo Mwenyezi Mungu amezitaja kwa watu wenye hekima.

Mhe. Spika, naendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa tano na wa sita katika kitabu hiki, niende katika *paragraph* ya nane, nanukuu: "Mhe. Spika, wakati tunaadhimisha sherehe hizi za miaka 50 nchi yetu imo katika kuandika historia nyengine ya kuandika Katiba; ambayo tunaamini itakapofanywa vizuri itachukua zaidi ya miaka 50 mingine ijayo. Hivyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Katiba kutumia fursa hii adhimu kutoa Katiba bora inayozingatia maslahi ya wananchi".

Mhe. Spika, nikiunganisha kidogo na kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha ukurasa wa tano ameanza *paragraph* ya 9 mpaka ya 11 kuhusiana na suala zima la mabadiliko haya ya Katiba. Mheshimiwa nataka niwaambie Watanzania, niwaambie na Wazanzibari tupo katika kipindi kizuri cha kuweka mabadiliko ya Katiba ambayo itawafaa wananchi kwa miaka 50 ijayo. Kwa sababu tendo hili la katiba limetajwa ndani ya vitabu viwili ambavyo tunavyo mbele yetu, nataka nizungumze kitu kimoja. Nataka nitoe kisa kimoja ambacho ni historia maarufu sana kwa wataalamu wa visa.

Kuna ndege mmoja alikamatwa akaingizwa katika tundu ikawa analishwa, anapewa kila kitu katika tundu, lakini ulifika wakati akafikiri kwao, na kwao ni kule ambako alizaliwa na kulelewa msituni. Kwa bahati akakata katika tundu, alipovunja lile tundu akarejea msituni, anafika katika uchanja akatembea huku na kule akaimba akasema, "*Alwatwanu bil-watwani, walaufauqal-jabal*", yaani mtu kwao ni kwao japo juu ya jabali.

Mhe. Spika, nakusudia kuwatanabahisha Wazanzibari, Watanzania, Watanganyika, mtu kwao ni kwao hata kama ni juu ya jabali, nawaambia kwamba umefika wakati wa Wazanzibari kuweza kutembea katika tawi zote za ulimwengu wakiwa huru, wakiwa na mamlaka kamili ya kutembea katika nchi mbali mbali.

Mhe. Spika, baada ya hapo niendeleo na ukurasa wa 11 katika kitabu cha Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, niende katika kifungu cha 16(1), "Kuimarika kwa Sekta ya Kilimo, Misitu na Uvuvi ambayo imekua kutoka asilimia 2.0 mwaka 2012 hadi asilimia 3.6 mwaka 2013", mwisho wa kunukuu. Hapa nataka nizungumzie sekta moja tu ya Kilimo.

Mhe. Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa Wazanzibari. Wakati Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein alipolizindua Baraza la Wawakilishi hili liliopo hivi sasa, alisema hivi katika kitabu chake ukurasa wa 22 Mapinduzi ya Kilimo. "Sekta ya Kilimo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar, kilimo ndio chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi walio wengi hasa vijijini na huchangia asilimia 27.3 ya pato la taifa katika uchumi wetu na kutoa ajira kwa asilimia 44 ya wananchi wa vijijini". Kuna maelezo mengi lakini hapo napenda nimalizie kunukuu.

Mhe. Spika, nina masikitiko makubwa kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili tokea ateuliwe Waziri wa Kilimo na Maliasili aliyepo sasa Mhe. Suleiman Othman Nyanga. Mheshimiwa kutokana na umuhimu wa kilimo, Mheshimiwa huyu tunapata taarifa anaumwa, lakini jambo la kufurahisha tunamshukuru Mwenyezi Mungu labda afya yake imekuwa nzuri katika Bunge la Katiba *Alhamdulillah*, mara nyingi tulikuwa tukimuona. Naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Wizara ya Kilimo iiangalie vizuri, kama Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili anaumwa au dharura nyengine yoyote na kunakuwa na Kaimu Waziri wa Kilimo, basi tuhakikishe kwamba Kaimu huyo wa Kilimo awe anazifanya kazi za kilimo vizuri sana kama waziri mwengine ili sekta hii iwe na waziri ambaye anafanya kazi zake kwa ufanisi.

Kwa kweli suala la kukosekana waziri makini katika kipindi hiki wizara hii niseme kwamba imedorora kiasi kikubwa, kwa nini? Kwa sababu kila siku tunaelezwa katika bajeti kwamba kuna kilimo cha umwagiliaji ambacho kimefikia asilimia ngapi lakini utekelezaji wake au muono wake hatuuoni, isipokuwa tunauona katika makaratasi tu. Naomba nimuulize Mhe. Waziri katika Sekta hii ya Kilimo ambayo ameleza kwa kina kabisa. Je, ni utaratibu gani wa usimamizi wa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili katika kipindi hiki ambacho waziri huyu ana dharura.

Mhe. Spika, ni hivi karibuni tu Kamati inayohusiana na kilimo ya Baraza lako iliakhirisha hata kazi zake pale mchana kwa sababu Waziri wa Kilimo na Maliasili alikosekana kuwepo. Mheshimiwa hili ni tatizo, na naiomba serikali ifanye juhudi ya kutosha katika suala zima la kuipatia wizara hii waziri ambaye atafanya kazi vizuri ili vijana wetu wanaoshughulika na kilimo wawe na mategemeo ya waziri ambaye anaendeleza suala la kilimo mabondeni na kwengeko.

Lakini nikiendelea katika suala hili hili Mheshimiwa, kuna mabwana shamba na mabibi shamba, mabwana na mabibi shamba kwa kweli sijui wanawajibika vipi mabondeni huko, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo hawa hawajulikani, wanajulikana katika maandishi lakini si wakulima wengi ambao wanapitiwa mabondeni kwao na mabwana hawa na mabibi shamba. Kwa hivyo, naiomba serikali kabla hatujafika katika ile bajeti ya kilimo, lakini Serikali Kuu ilianganalie vyema suala hili na ikiwa kuna upungufu wa mabwana na mabibi shamba basi waajiriwe wataalamu mbali mbali waliotoka katika vyuo vya kilimo ili wafuatilie suala hili kwa ufanisi wa kutosha.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa huo huo wa 11 kuhusiana na ukuaji wa pato la taifa. Ukuaji wa pato la taifa pameelezwa hapa vitu vingi tu ambavyo vimeingia katika kupatisha pato la taifa la nchi yetu hii ya Zanzibar. "Kuimarika kwa baadhi ya Sekta ya Viwanda kulikochangiwa na ongezeko la ukuaji wa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka asilimia 0.1 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 kwa mwaka 2013", imeendelea hiyo mpaka kipengele cha 5. Lakini mchango huu umeelezea mambo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa sekta ya huduma, nyengine ni kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini, lakini na ya mwisho ni kuendelea kwa hali ya amani na utulivu nchini.

Mhe. Spika, mchango wa zao la karafuu hatujauona hapa umechangia kiasi gani katika mapato ya serikali. Kwa kuwa zao la karafuu ni miongoni mwa mazao ambayo yanategemewa hapa Zanzibar, lakini katika kitabu hiki hatujaona kwamba zao la karafuu lina mchango gani ikiwa ni pamoja na duka lilioko Dar es Salaam limechangia kiasi gani katika pato la taifa, pamoja na lile duka lilioko Dubai limechangia kiasi gani.

Nikiendelea na mchango wangu niende katika kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Omar Yussuf Mzee ukurasa wa 5 na 6, lakini maelezo haya nimeshayaeleza yanayohusiana na masuala ya Muungano.

Niende katika ukurasa wa 8 *paragraph* ya 14 na 15, naomba ninukuu: "Mhe. Spika, kwanza ni msiba uliolikumba Bara letu la Afrika hapo tarehe 5 Disemba, 2013". Nikiendelea na *paragraph* ya 15 anasema tarehe hiyo niliyoitaja ndio alifariki mpendwa wetu Mwanaafrika na kioo cha utetezi wa haki Afrika na duniani kote; marehemu Nelson Mandela. Sifa na mchango wa Mzee huyu hasa katika kupigania haki za Afrika na duniani pamoja na mchango wake katika kuleta maelewano na kustahamiliana miongoni mwa makundi yanayohasimiana yakiwemo ya ubaguzi wa rangi ambayo yalimtesa yeye mwenyewe na kuendelea, mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Kwa kweli Mhe. Spika, matamko haya tunapaswa tujifunze, tunajifunza nini kwa kifo cha Mhe. Nelson Mandela? Tulinganisha tabia zetu za Wazanzibari katika kupigania kwetu nchi yetu na Nelson Mandela tunavyomsifu hapa katika ukurasa huu wa 8 wa hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha. Tunapaswa tukumbuke kwamba sote tutakufa kama alivyokufa Nelson Mandela, na tunahitaji kuweka kumbukumbu nzuri katika uhai wetu kwa ajili ya mauti yetu.

Nikirudi nyuma kidogo niende katika historia fupi tu ya Watu wa Makka na Madina walivyokuwa wakigombana hapo zamani, hasa watu wa Madina. Mtume (S.A.W) alipokwenda Madina aliwaunganisha watu wa Answare na Muhajirina wakawa kitu kimoja, tunapaswa viongozi tuwe kitu kimoja katika kuwaunganisha watu si katika kuwabagua watu.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wangu umebakia mchache niendeleo katika ukurasa wa 19 kifungu cha 39. Kifungu hiki kinaelezea mambo mengi lakini nataka nizungumzie jambo moja tu hapa katika kifungu, kuziba mianya iliyopo na kupunguza nakisi ya bajeti ya serikali.

Mhe. Waziri wa Fedha ana kazi kubwa ya kuiziba mianya na kwa kweli awe na *superglue* makini kweli kweli ili mianya hii iweze kuzibika. Kwa nini? Kwa sababu kila mwaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakuja na ripoti ambayo matumizi ya fedha yanayotumiwa yasiyofuata taratibu ni mengi, matumizi yanayotumiwa kwa kuharibu mali mbali mbali za serikali ni mengi, lakini serikali imetulia hatuoni *reaction* yoyote inayotendeka baada ya vitabu vya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, hili ni tatizo na kama kuna mwanya ambao unahitaji kuzibwa basi mwanya huu ni mwanya muhimu sana, kwa sababu hayo mapato ya serikali hapo ndipo yanapopenya. Mheshimiwa kwa haya machache niseme nakushukuru na ahsante sana.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii nikawa mzima wa afya na mimi nikawa miongoni mwa wachangiaji.

Mhe. Spika, nampongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora kwa hotuba zao, pia pongezi ziende kwa watendaji wao kwa kazi nzuri waliyotuletea. Bajeti hii ya mwaka 2014/2015 ni muhimu kwa uchumi wa Zanzibar hasa kwa vile mwakani 2015 ni mwaka wa uchaguzi.

Mimi nianze ukurasa wa 14 kipengele cha 19 katika kitabu hiki cha bajeti. Niipongeze *TRA* na *ZRB* kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato katika serikali yetu. Lakini namuomba Mhe. Waziri azidi kusimamia kazi hii ya kukusanya mapato kwa sababu bado kuna watendaji ambao si waaminifu, namuomba ajitahidi mikakati yake kama taarifa yake inavyojieleza kwamba mwaka 2013/2014 mapato yameongezeka. Kwa hivyo, namuomba jitihada hiyo izidi, ihakikishe watendaji waliokuwa si waaminifu anakwenda nao sambamba.

Mhe. Spika, pia niendeleo ukurasa wa 19, niipongeze serikali kwa kujitahidi kusimamia mapato kwa mwaka 2013/2014. Lakini bado namuomba Mhe. Waziri azidi kusimamia wizara zake ambazo zinakusanya mapato hasa kwa wale wanaonunua vifaa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri asimamie suala hili kwa sababu wale wasimamizi wanaonunua vifaa kusema kweli katika mawizara yetu vifaa wanavyonunua haviridhishi, vifaa hivyo vikinunuliwa kama gari mwaka tu inakuwa gari hiyo haifanyi tena kazi, imeharibika na tayari serikali imeingaa hasara.

Mhe. Spika, niendeleo kuhusu ada ya Bandari. Ada hii ya Bandari kama taarifa inavyosema kwamba imekusanya ada vizuri. Lakini nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anieleze kwa vile tulikubaliana ada hii iende katika madawati ya wanafunzi skuli. Nilikuwa naomba wakati anapokuja kutoa majibu anifahamisha kuhusu haya madawati Wizara ya Elimu wametengewa kiasi gani ili kutengeneza madawati hayo.

Pia kuhusu kuimarisha huduma za kijamii zikiwemo Elimu bora, huduma za Afya na upatikanaji wa maji safi na salama. Mhe. Spika, nianze na Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu kama tulipata taarifa tuliambiwa kwamba kuna miradi mingi katika Wizara ya Elimu. Lakini nikija katika Maskuli Mhe. Spika, Skuli zilizokuwa zinajengwa kipindi hiki ni Skuli mpya lakini baada ya muda mfupi tangu zianze kusomewa tayari zimeanza kubanduka *tiles* na kwenye *floor* pia.

Mhe. Spika, skuli nyingi hizi mpya zilizokuwa zimesimamiwa katika mradi huu katika Wizara ya Elimu skuli zimeanza kuharibika. Kwa hivyo, tukiangalia hapa serikali inazidi kupata hasara kwa sababu baada ya kuondoka mkandarasi skuli hizo zikisomewa mwaka mmoja tu zinaanza kutimbuka. Kwa hivyo, wakandarasi hawa wanakuwa hawatengenezi skuli zetu vizuri. Namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie vizuri pia.

Mhe. Spika, pia naiomba serikali kununua mashine ya *DNA* kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi kwamba hichi ni kifaa muhimu. Mashine hii ilikusudiwa kwenye Wizara ya Afya kwenye bajeti yao ndio wanunue, lakini namuomba Mhe. Waziri wa Fedha aliangalie vizuri suala hili kwa sababu Wizara ya Afya bajeti yao haitoshi. Kwa hivyo, hawawezi kununua mashine hii. Namuomba Mhe. Waziri wa Fedha suala hili alisimamie kwa

sababu sisi wanawake ndio tunaopata shida; watoto wetu wanabakwa kesi haziendi. Tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha suala hili alisimamie tuone mashine hii inapatikana.

Mhe. Spika, katika suala la maji namuomba Mhe. Waziri wa Fedha aangalie tena matatizo ya maji ili sisi wanawake tuondokane na shida hii ya maji hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, mwaka jana pia nilichangia kuhusu masuala ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharabi miradi tumeambiwa ipo lakini bado maji tatizo hasa wanawake katika Mkoa huu wa Mjini Magharibi tunasumbuka.

Mhe. Spika, mwisho kwa niaba yangu na wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono hoja mia juu ya mia. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana nimuombe basi Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi achangie wakati Mhe. Mohammed Haji Khalid anajitayarisha.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa bajeti yake ya mara hii ambayo imekiuka bajeti ya mwaka jana iliyokuwa na 658.5 tafauti na bajeti ya mwaka huu inayosema 707.8 nimpongeze Mhe. Waziri kwa bajeti yake hii nzuri na ukiangalia Mhe. Spika, bajeti hii kutokana na bajeti ya mwaka jana imepanda kidogo.

Mhe. Spika, madhumuni hasa ya bajeti ni kutatua matatizo ya wananchi yaliomo katika nchi. Lakini vile vile Mhe. Spika, bajeti hii haioneshi kutatua matatizo ya wananchi walioko chini, kwa mfano wakulima. Bajeti hii Mhe. Spika, haioneshi wakulima vipi watapata pembejeo na vipi watapata mbolea na vipi watapata mbegu za kuzalishia hicho kilimo. Bajeti hii inaonesha kikati kati tu, lakini hasa ukiangalia kwa wananchi wahusika ambao tayari ndiyo wanayoiunda hii bajeti haikuangalia.

Lakini vile vile niseme katika suala la uvuvi, ukiliangalia suala la uvuvi vile vile bajeti hii haikuangalia wavuvi walioko chini, wavuvi wote ambao ni wananchi walikuwa wanaisubiri kwa hamu bajeti hii itawaambia nini. Lakini Mhe. Spika, bajeti haikuwaambia kama wavuvi hawa watapata nyavu za kuvulia au watapata vyombo vya kuvulia au vipi watawua. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hilo alione katika bajeti yake.

Lakini vile vile pia katika kilimo uzalishaji ni mdogo hii inasababishwa na uwezeshwaji wa wakulima wetu ambao wanalima kilimo cha umwanguaji na vilimo vyengine vya aina nyengine. Mhe. Spika, bajeti hii pia haikuangalia soko la mazao kwa wananchi wetu ambao baada ya kulima wanahitaji soko na soko hili bado ni dogo. Mhe. Spika, pia haikuangalia soko ambalo litasarifu mazao ambayo tayari wakulima wetu wameshayavuna. Hili Mhe. Waziri ningelimumba aliangalie sana kwa wakulima wetu, kwa sababu wakulima wanapolima mazao wakati mwengine huwa yanafurutu hapa, ikawa hatuna pa kuyaweka, laiti kama pangukuwa na soko la kusarifu au kiwanda cha kusarifu mazao haya nadhani ingekuwa wakulima wetu hawapati shida.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nije katika nyongeza za mishahara. Mhe. Spika, nyongeza za mishahara zimeambiwa kwamba hazikupandishwa lakini ningesema kwamba mishahara iangaliwe kwa wananchi waliokuwa na mishahara ya kima cha chini; ambao hawa mapato yao ni madogo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hili angeliangalia kwa vizuri.

Lakini pia Mhe. Spika, nije katika kitabu ukurasa wa 21 unaosema mwenendo wa uingiaji wa watalii. Mhe. Spika, kwa mwaka 2013 mwenendo wa waingiaji wa watalii umeongezeka kwa asilimia 7.1 kufikia jumla ya watalii 181,301 kwa mwaka 2013. Mhe. Spika, bila ya kuendelea kwa watalii waliongia hapa inaonesha kwamba na kila miaka wamekuja watalii 50,966 inaonesha.

Lakini Mhe. Spika, ukiangalia mapato ya watalii hawa hayaonekani sijui huwa yanakwenda wapi? Watalii wanaingia kila leo lakini mapato hayaonekani. Mhe. Spika, naomba hili Mhe. Waziri aliangalie, inaweza mapato haya huwa yanaonekana kutokana na kuwepo chombo cha kurikodi watalii wanaoingia, ningemuomba Mhe. Spika, kuwepo na chombo cha kurikodi watalii wanaoingia na wanaotoka.

Vile vile Mhe. Spika, nije katika suala la afya, suala hili bado ni gumu; dawa hospitali bado hamna, na ukienda hospitali utaambiwa uende katika kituo chengine cha binafsi ununue dawa. Hili ni tatizo kubwa na sugu ambalo linatuzorotesha hata sisi wananchi, maana mgonjwa akifika pale ana uwezo wa kununua dawa ndivyo, lakini Mhe. Spika, ikiwa uwezo wa kununua dawa hana mtu kama huyu atakuwaje, si anakufa moja kwa moja.

Mhe. Spika, nije katika kitabu cha Ripoti ya Hali ya Uchumi katika kifungu namba 7 Upatikanaji wa maji safi. Mhe. Spika, matengenezo ya miundombinu ya usambazaji wa maji safi kwa ajili ya upotevu wa maji safi unafanyika katika maeneo ya Magogoni. Lakini Mhe. Spika, nisiseme kwamba ni Magogoni, kwa kweli maji safi na salama bajeti hii isiingalie usambazaji wa maji lakini iangalie na wale wananchi ambao wamefungiwa mifereji ndani ambao tayari watu wale maji yale hayapatikani.

Mhe. Spika, kweli wananchi wetu wanaumia sana, usambazaji wa maji mwema lakini tayari maji hayapatikani hili ni tatizo kubwa na gumu na sugu yapo maeneo mengi tayari mifereji imo ndani lakini maji hayatoki. Licha ya maji kutoka lakini pia ni tatizo la upatikanaji ya mapato ya serikali pia huwa yanakosekana hapa.

Mhe. Spika, nije katika kuimarisha miundombinu. Mhe. Spika, kila mwaka miundombinu inaimarishwa. Lakini ukiangalia miundombinu hii haiimariki inaimarishwa tu lakini haiimariki, sijui tuseme kwamba bajeti hii inakuwa ni ndogo au vipi, barabara nyingi Mhe. Spika, zinazojengwa sasa hivi hazikufika mwaka tayari zimeshabomoka sijui hili ni tatizo la fedha, au hili ni tatizo la hawa wajenzi, hatujui tatizo ni nini.

Aidha wakandarasi wanaochukuliwa si wakandarasi ambao wanaweza kutengeneza barabara isipokuwa watu wanachukua tufanye tuondoke. Hili Mhe. Spika, ni tatizo sugu na ukiangalia hata si barabara hizi tu hata za ndani kuna barabara ambazo tayari zimeshaekewa ahadi tangu Baraza lililopita la mwaka juzi mpaka limekuja la mwaka jana na leo bado kuna barabara hizi hazijatengenezwa. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi.

Nikija katika Kiwanja cha Ndege Pemba naona inabakia ni hadithi tu lakini bado utekelezaji wa kiwanja cha Ndege unatutia huzuni.

Mwisho nije katika zao la karafuu. Wananchi wengi wanategemea zao la karafuu na ndio pato kubwa la uchumi wetu. Kwa mwaka ujao Mhe. Spika, nimuilize Mhe. Waziri serikali imejipanga vipi kuwainua wananchi katika suala zima la uchumaji wa karafuu. Mhe. Spika, baada ya hapo nakushukuru ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadae tumsikilize Mhe. Marina Joel Thomas.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi kueleza machache niliyonayo juu ya vitabu viwili vilivyo mbele yetu.

Mhe. Spika, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima na kuweza kusimama katika Baraza lako hili.

Mhe. Spika, Zanzibar ilifanikiwa kufanya Mapinduzi mwaka 1964 hapa Zanzibar niseme tulijigomboa kisiasa. Kwa hivyo, hapa tulipata uhuru wa kisiasa kama huko nyuma tulitawaliwa Mapinduzi yalileta ukombozi wa Mzanzibari. Lakini ukombozi wa kisiasa, lakini je, ukombozi huu wa kisiasa unakidhi haja ya Wazanzibari? Kwa sababu nikitizama bajeti yetu ya Maendeleo ambayo Waziri amewasilisha asilimia 80 ni misaada, mikopo na ruzuku kwa mambo yetu ya maendeleo ni asimilia 19 na *point* tu ndio fedha za serikali. Kama mambo yetu ya maendeleo yote yanategemea misaada kutoka nje, je, hapa sisi tunao uhuru wa kiuchumi?

Kwa kweli tumetawaliwa kiuchumi na huu ndio unaitwa Ukoloni mambo leo. Utawala tulionao ni wa kisiasa tu, lakini wa kiuchumi bado tumetawaliwa; na kama hawa waliotajwa hawakutusaidia hakuna lolote la maendeleo kwa mwaka huu litakalofanyika. (*Makofi*)

Je, utawala huu wa siasa tu na uchumi tunategemea wengine tutafika wapi? Uchumi wa kuwapigia watu magoti tutafika wapi? Miaka 50 leo serikali ikimalizika mwaka huu uwezo wake wa maendeleo ni asilimia 19 ndio uwezo wake, asilimia 80 *point* ndio tunategemea mikopo, misaada na ruzuku.

Mhe. Spika, hii hatari tena kubwa mno. Niseme bado kumbe hata kukaa kitako hatujaweza licha ya kusimama dede, Bado hatujaweza, tuko hatarini, tena hatari kubwa kwa maendeleo yetu yanategemea misaada, mikopo na ruzuku. Hii ni hatari.

Mhe. Spika, mapato yetu ya ndani, asilimia 49 tunalipa mishahara . Kwa matumizi ya Serikali ni pesa chache sana, ndio maana Mhe. Spika, kwa sababu OC zetu ni ndogo, unakwenda hospitali hakuna dawa, unaenda skuli zaidi ya Mwalimu kupewa mishahara hakuna chaki, tunachangishana wazee, kila sekta unayokwenda, kwa sababu Serikali imeshindwa kutia pesa za kuiongoza, inachomudu angalau hivi sasa ni kutapatapa kuwalipa wafanyakazi, na bado huku nina khofu kubwa kuwa huenda ikarudia katika awamu iliyopita kwa wafanyakazi kuwa itafika siku washindwe kulipwa.

Huduma zote zile ambazo tunajitegemea wenyewe, zinasuasua, kwa hiyo tunao uhuru wa kisiasa lakini tumekosa uhuru wa kiuchumi. Ningeiomba Serikali inambie itafanya nini kujiondoa katika kutegemea watu wa nje katika maendeleo yetu. Vyenginevyo huu uhuru, haya Mapinduzi tunayojivunia tunajivunia nini na hatujiwezi.

Mhe. Spika, katika bajeti hii Mhe. Waziri kaonesha kuwa anatarajia kukusanya bilioni 707.8. Makusanyo ya ndani katika kitabu chake inaonesha ni bilioni 365.8 na ya nje ni 305.4, ukijumlisha hii haifiki haya matarajio yake. Kwa hiyo anataka kutumia ambacho hakukusanya. Na hii ndivyo tulivyo Wazanzibari, mfanyakazi tunamlipa fedha ambazo anatumia zaidi kuliko mapato yake. Kumbe na Serikalini ndio hivyo hivyo. Mhe. Waziri anataka kutumia ambacho hakimiliki. Kwa hiyo katika mpango wake anataka kutumia ambacho hakimiliki kama anavyotumia mfanyakazi wa kawaida analipwa shs. 150,000 anatumia 500,000 kumbe na serikalini ndio hivyo hivyo si mfanyakazi peke yake.

Jee hii nakisi iliyopo hapa, kwa sababu makusanyo haya yanaonesha kuwa atakusanya 671.2 badala ya 607.8 bilioni, huu upungufu uliopo ataupata wapi ili aweze kuendesha hiyo mipango aliyoipanga.

Mhe. Spika, hali hii ni mbaya, ngumu na inatisha. Twajisifu lakini hatuna tulipo. Mhe. Spika, tumezungumza kwenye ukuaji wa pato la taifa. Hapa Mhe. Waziri wa Nchi (Ikulu) na Utawala Bora, ametuonesha ongezeko kubwa la mapato na kasema kuna ongezeko la asilimia 7.5 ni nzuri. Kwa hivyo kuna ongezeko zuri la mapato. Lakini mapato yameongezeka kulingana na yeye lakini kwa nini miradi yetu inakwama, baada ya mfadhili kupewa mradi, ile sehemu ya serikali kwa nini ikwame wakati ambapo ikiwemo barabara tatu za Pemba za Kaskazini, kwa sababu Mkandarasi Serikali haikumlipa kwa wakati lakini serikali hiyo hiyo inasema kuwa mapato yetu yameongezeka, jee ongezeko hili limekwenda wapi?

Mhe. Spika, nchi hii inavyoonesha mapato yanakwenda sehemu mbili kubwa; moja kwa wanasisia na pili kwa watendaji wakuu wa Serikali, basi. Hawa wafanyakazi wengine wote tunawapa pipi tu, hatuwalipi. Tunawapa pipi. Mhe. Spika, pamoja na ongezeko hili alilolitaja Mhe. Waziri kwa wastani kwa siku, na kwa wastani huo aliofanya yeye kwa siku Mzanzibari anapata 20972.2. Alivyofanya Mhe. Waziri kwa mwaka anapata Bilioni moja poiti kadhaa, kwa siku kila Mzanzibari kwa wastani anapata hizo shs. 2,972. Ni Mzanzibari gani Mhe. Spika, anayeweza kuishi kwa shilingi 2000 kwa siku. Ingelikuwa miaka ya sabini alikuwa anaishi, lakini miaka ya elfu mbili ni kumdanganya. Na hii wastani, hizi 1,000,000 alizozitaja ni *average* ambazo kuna watu hawazifiki. Kwa mfano kama hesabu ingefanywa baina ya mkulima wa Sipwese kijiji changu, na mfanyabiasha maarufu yeyote mwenye pesa watu wawili hawa wakafanyiwa *average*, huyu mtu wa Sipwese mkulima ambaye hana chochote angelionekana kuwa ana pato kubwa lakini kabebwa na huyu mwenye nacho, kwa sababu *average* inamuangusha mwenye nacho kidogo na inampandisha aliyekuwa hana, halini uhalisia wake aliyekuwa hana ndo hana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, bajeti hii ni ngumu na nadhani kama hawatotaka kutusaidia kwa miradi yetu tuliyoipanga, basi hakuna mradi ambao utatendeka, hakuna mradi ambao utaendelea. Kwa hivyo tunasema kuwa "*mtegemea cha ndugu hufa masikini*". Sisi tunategemea misaada na mikopo, wenyewe wakija wakakunja makucha yao itakuwa sisi "*innaa lillahi wainna ilayhi raajiuun*" hakuna lolote la maendeleo ambalo tutalifanya. Hii ni hatari Mhe. Spika.

Mhe. Spika, makusanyo ya mapato sidhani kama yanasimamiwa vyema. Imani yangu ni kuwa watalii wanaoingia nchini ni wengi kuliko wale ambao serikali inapata takwimu zake. Kwa sababu wasimamizi ni wengi, watu wa forodha na watu wengine wanakusanya mapato haya ya watalii. Jee ni watalii wangapi ambao wanaingia. Takwimu ambazo zinaoneshwa na Serikali khofu yangu ni ndogo kuliko uhalisia wa watalii wanaoingia Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hali hii Serikali yetu itakuwa inasuasua katika mambo ya maendeleo. Inatambaa kuwa angalau inamudu kuwalipa wafanyakazi mishahara. Lakini Mhe. Spika, kwani hii serikali inakwenda kwa ilani ipi? Inakwenda kwa ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Hapa Serikali inategemea asilimia 80 ya Maendeleo yake kutoka kwa wafadhili, hii ndio ilani inakotupeleka. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Marina Joel Thomas na baadae Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti. Mhe. Spika nitaanza kuchangia Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.

Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake imara, makini hekima na utulivu katika kuingoza Zanzibar. Pia nawapongeza watendaji wake wa Tume ya Mipango na wafanyakazi wote kwa kumsaidia Waziri wa (OR) Ikulu na Utawala Bora katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, nitaanza kuchangia katika mwenendo mzima wa uchumi wa Zanzibar. Katika ukurasa wa 11 kitabu cha Mhe. Mwinyihaji, ukuaji wa pato la taifa kwa 2013 imeelezwa kuwa ulifikia thamani ya Tshs. 1442.8 bilioni ukilinganisha na mwaka 2012 ambapo imepatikana 1342.6 bilioni. Ongezeko hili Mhe. Spika, la pato limesababisha pia mafanikio katika ukuaji wa hali ya uchumi wa Zanzibar, kwa wastani wa asilimia 7.4 kwa mwaka 2013 na asilimia 7.1 kwa 2012. Na katika hotuba yake Mhe. Waziri ameeleza sababu mbali mbali ambazo zimechangia ukuaji wa hali ya uchumi hii. Hii ni hatua nzuri Mhe. Spika na naipongeza serikali kwa hilo.

Katika mafanikio amesema kuna sekta ya kilimo, misitu, uvuvi, viwanda, huduma, Utawala Bora na elimu ndizo sekta ambazo zimechangia kuongezeka hilo pato la Zanzibar. Katika sekta ya kilimo, misitu na Uvuvi mwaka 2012 imeeleza kuwa ni asilimia 2.0 na 2013 asilimia 3.6 hii ni hatua kubwa Mhe. Spika, na katika Viwanda 2012 asilimia 0.1 na 2013 asilimia 3.2 sekta ya huduma pia imeeleza kuwa katika mwaka 2012 asilimia 0.2 na imepanda katika mwaka 2013 asilimia 6.5.

Mhe. Spika hii ni hatua kubwa kwa serikali yetu, ambapo imeelezwa katika kitabu hichi cha Mhe. Waziri karibu miaka mingi ya hivi karibuni ambapo pato hili halijaongezeka, kwa hiyo ni hatua kubwa sana ya kuipongeza serikali yetu kwa hatua kubwa iliyofanya. Na imeelezwa kuwa sababu nyengine ni hali ya amani na utulivu, ambao upo nchini.

Mhe. Spika, bila ya amani na utulivu, haya yote tusingeyazungumza hii leo. Amani na Utulivu, ni muhimu katika nchi yetu, pia hapa naishauri serikali wasiwaache watu wachache kuichezea amani hii, amani hauichezewi. Pia namuomba Mhe. Waziri tusiridhike na mafanikio haya tuliyoyapata katika ukuaji wa pato la taifa pamoja na hali ya uchumi wa Zanzibar. Hapa ndipo nashauri zitumike mbinu za ziada ambazo ni kuziendeleza huduma hizi muhimu ili zisaidie pato la nchi na kutoa fursa za ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, nitakuja katika sekta ya uwekezaji binafsi; hii iko katika *page* ya 24 katika hotuba ya Mhe. Waziri. Sekta hii ni muhimu nayo, sekta ambayo inasaidia kuzalisha ajira, na imeelezwa katika takwimu katika mwaka 2012 sekta hii imezalisha ajira 1223; ambapo kwa 2013 imezidisha ajira 1365.

Jitihada hii ni nzuri, na hapa Zanzibar kuna tatizo la ajira ni kubwa. Si Zanzibar peke yake Tanzania na hata Dunia nzima. Na nakumbuka katika siku ya wafanyakazi Duniani Mhe. Rais katika hotuba yake Bwawani pale alizungumzia suala zima la tatizo la ajira na alisema takriban vijana 7,000 na zaidi wenye digirii, wenye diploma, *form six* hawana ajira.

Hapa ushauri wangu ni kuziimarisha hizi sekta binafsi; sekta za biashara za viwanda, sekta za Utalii, Kilimo ili kupunguza kiwango kikubwa cha tatizo la ajira kwa vijana wetu. Zikiimarishwa hizi sekta viwanda vitakuwepo, utalii ukaimarishwa, itaongeza kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ajira hapa nchini.

Pia katika suala hili la ajira naomba niwashauri wananchi au vijana wenzangu, ajira si ya serikali peke yake, ajira ni kazi yoyote ambayo ni halali. Kwa hiyo tuzitumie hizi fursa ambazo serikali inazileta ili tujikwamue katika kuendeleza maisha yetu. Na katika hotuba hii Mhe. Spika, kumeelezwa changamoto ambayo naomba niinukuu

“Changamoto 2013/14 imesema mchango mdogo wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa. Serikali ichukue juhudi za makusudi kuendeleza sekta hii ili kuongeza ajira na kukuza pato la Taifa. Katika utekelezaji wa mwaka 2012/13, imeelezwa kwamba suala la viwanda ni changamoto. Kwa hiyo naiomba Serikali uchukue jitihata za makusudi katika sekta hii ya viwanda ili kutengeneza ajira kwa vijana wetu. Mhe. Spika, kwa sababu viwanda vikiwa vingi ajira zitapatikana.

Nitaendelea katika Miradi, hii iko katika *page* 55. Hapa ilikuwa nina ushauri tu, suala la miradi ni vyema serikali ijipangie miradi michache ambayo itaweza kutekelezwa kwa wakati husika kuliko kujipangia miradi mingi kwa wakati mmoja na utekelezaji wake ukawa mgumu, na unakuwa mgumu kutokana na uhaba wa fedha ambazo zinapatikana.

Kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha akitoa *ceiling* atoe *celing* ambayo *at least* itatekelezeka kwa asilimia 80 au 90, kuliko akaweka *ceiling* kubwa katika wizara wakapata asilimia ndogo ya fedha za matumizi.

Mhe. Spika hapa kuna suala zima la kufuta hizi gharama za mitihani kidato cha sita na cha nne. Kwa kweli hapa Serikali imewatendea haki wananchi wanastahiki pongezi. Naipongeza Serikali kwa kufuta malipo yanayofanywa na wazazi kwa ajili ya mitihani ya kidato cha nne na cha sita; ambapo suala hili la ada hizi wazazi ndio walikuwa wakiwalipia watoto wao, lakini Serikali kwa jitihada zake ambayo ilituonea huruma imefuta ada hii ambayo wazazi ilikuwa ikiwahudumia.

Mhe. Spika, nikiangalia katika mapato ya ndani yalifikia shilingi za Tanzania 247.27 milioni sawa na asilimia 62.1 ya mapato yote. Hapa Mhe. Spika, kuhusu mapato ya ndani nilikuwa naomba pia nitoe ushauri, Serikali izidi kutafuta vyanzo vyengine vya mapato. Na ikitafuta vyanzo vyengine vya mapato itasaidia hata kupunguza ule utegemezi kwa wahisani. Na ikitafuta vyanzo vya ndani vya mapato ina maana pato la ndani litaongezeka. Mfano labda *property tax* na nyenginezo, Wizara ijitahidi kwa mbinu zote ili vyanzo vya mapato vya ndani viongezeke na kupunguza tatizo kubwa la utegemezi.

Mhe. Spika, utegemezi si mzuri, hii misaada ambayo tunapata kwa wahisani mengine inakuwa na masharti magumu, masharti ambayo pengine unaweza ukaipeleka hata nchi katika hali iliyokuwa si nzuri. Kwa hiyo ni vyema kujiiimarisha katika vyanzo vyetu vya mapato vya ndani ili kuondokana na Serikali yetu kuwa tegemezi.

Mhe. Spika, nitakwenda katika deni la nje. Katika kitabu cha Mhe. Waziri alisema kuna bilioni 203.8 ambapo asilimia 88 ya deni hili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania italilipa na asilimia 12 italipa Serikali ya Zanzibar. Hapa ni kutoa tu pongezi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatusaidia sana, kwa sababu asilimia 88 ya deni hili ambalo ni bilioni 203 si mchezo, kwa Serikali ya Zanzibar tusingeweza.

Mhe. Spika, naunga mkono asilimia mia moja bajeti hii.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na hotuba hizi mbili; moja iliyotolewa na Mhe. Waziri anayeshughulikia mambo ya Ikulu huko Dkt. Mwinyihaji Makame na nyengine iliyotolewa na Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wetu anayeshughulikia mambo ya madukhuli. Kwa hiyo hotuba yangu zaidi itajikita katika hotuba mbili hizi.

Mhe. Spika, bila kusahau kwamba nitatia pia nyalio katika hotuba hizi kupitia dira ya mabadiliko kwa ujenzi wa Zanzibar mpya yaani Ilani ya Chama cha Wananchi CUF ya mwaka 2010 ili kuona ingesaidia vipi katika mambo haya.

Mhe. Spika, katika mchango wangu nianze na hichi Kitabu cha Mhe. Mwinyihaji Makame kwa hotuba yake katika ukurasa wa 6 ibara ya 8. Mhe. Spika, naomba kunukuu.

"Mhe. Spika, wakati tunaadhimisha sherehe hizi za miaka 50 ya nchi yetu imo katika kuandika historia nyengine ya kuandika Katiba ambayo tunaamini itakapofanywa vizuri itachukua zaidi ya miaka 50 mengine ijayo.

Hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Bunge la Katiba kutumia fursa hii adhimu kutoa Katiba bora inayozingatia maslahi ya wananchi".

Na kwa bahati nzuri maneno haya haya aliyasema Mheshimiwa kama haya katika ibara ya 9 ukurasa wa 5 katika kitabu cha Bajeti hichi alichokizungumzia Mhe. Omar Yussuf Mzee, aliweza kuzungumza maneno kama haya kwamba tumo katika mchakato wa Katiba.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba nchi yetu imo katika kipindi kigumu sana cha mchakato wa Katiba. Mhe. Spika, katiba maana yake kwa juu juu huku tusiende kule walipo watu wa *Political Science* tuje katika sisi wanasiasa; katiba maana yake ni mkataba baina ya watawala na watawaliwa. Kwa hiyo katika Katiba Mhe. Spika, kunahitaji maridhiano makubwa baina ya pande mbili hizi hususan katika mawazo yanayohitajika zaidi ni ya upande wa watawaliwa. Sasa Katiba kama inahodhi zaidi upande wa utawala Mhe. Spika, basi katiba hiyo mara nyingi huwa haikubaliki na huweza kutokea mgogoro katika nchi.

Uzoefu wangu katika masuala ya siasa Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia katiba za nchi nyingi nikaona katika utaratibu wa kutunga katiba ni huu kama alioeleza Jaji Robert Makaramba katika kitabu chake kile alichokiita *Constitution and Constitution Making Process*. Hichi kitabu alikitoa Jaji Robert Makaramba. Utaratibu huu ndio unaounda Katiba nzuri, na ni ule ule ambao tunaufuata sasa hivi hapa Tanzania, kwa kuanza kuchukua maoni ya wananchi tukaleta rasimu na sasa sisi tupo kwenye Bunge la Katiba, na baadae kwenda kwenye kura ya maoni ili kuipa *legitimacy* katiba hiyo.

Mhe. Spika, katiba yetu kwa sasa ipo katika *stage* ya Bunge la Katiba. Mhe. Spika, napata wasiwasi kwamba ile rai aliyotupa Mhe. Waziri Mwinyihaji Makame na Mhe. Waziri Omar Yussuf Mzee ya kutoka na katiba ambayo itakubalika, itakayoridhiwa na watu, basi napata shida sana kwa sababu yale mawazo ya wananchi yameanza kuporwa na lile tabaka la juu yaani watawala. Hapa ni tatizo sana.

Mhe. Spika: Sasa hayo yaache uje ukamalize tarehe 5 Agosti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, mimi nadhani katiba ni ile inayoweza kulenga *unity* katika nchi. Mimi nafikiria kwamba na hawakutia kama programu hii kwa mara hii hatukuona katika hotuba zao kama ni katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Lakini kama kuleta *unity* katika nchi ni katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi basi nadhani hapa patakuwa nini. Kwa sababu katika miaka ya nyuma Mhe. Spika, mimi nakumbuka kabla ya Chama cha Mapinduzi kuzaliwa hapa tulikuwa na umoja mkubwa sana, ilikuwa huwezi kuweka *difference* yoyote kama huyu ni Mtumbatu, huyu ni Mpemba, huyu ni Muunguja kwa sababu ya viongozi waliokuwa wanasimamia sera za Afro Shirazi walikuwa makini sana katika kuleta *unity* katika nchi. Na ndio maana Mzee Abeid Amani Karume alioa wake wawili wa Kipemba, Mzee Aboud Jumbe alioa mke mmoja wa Kipemba, Mhe. Thabit Kombo Jecha alioa mke mmoja wa Kihindi, Brigedia Yussuf Himidi alioa mke mmoja wa Kiarabu na baadhi ya machotara wamo humu ndani. Kwa hiyo ilikuwa huwezi kubagua hata siku moja.

Leo tumo katika Bunge la Katiba tunapata tatizo la kwamba huyu Mpemba, huyu Mwarabu, huyu Muhindi, hebu tujirudisheni kabla ya pale Chama cha Mapinduzi hakijazaliwa mwaka 1976 ilikuwa hakuna mambo hayo. Nadhani tukifanya *reference* ya waasisi wa nchi hii akina Mzee Abeid Amani Karume, akina Mzee Thabit Kombo Jecha, akina Brigedia Yussuf Himidi, akina Bwana Edington Kissasi Kamishna. Nadhani mkifanya *reference* basi *unity* katika nchi itapatikana. Na haya mambo ya huyu Mwarabu, huyu Mpemba, huyu hivi yataondoka. Nadhani tuelekeze hilo.

Laiti Mhe. Spika, ingelikuwa Serikali ni kama gari au kama meli basi mimi ningemuomba Dkt. Ali Mohamed Shein aniazime kwa muda wa miezi mitatu kusudi nitumie dira nyengine ya kukiendesha hichi chombo mbadala. Ningetumia hii Ilani ya Chama cha Wananchi CUF kwa miezi mitatu tu nyote humu mngekuwa mnaamkiana mkiingia badala ya kutukanana, ingekuwa munaheshimiana badala ya kudharauliana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa sasa rudi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, naenda moja kwa moja katika Hali ya Uchumi Ibara ya 9. Mhe. Spika, katika ibara hii baada ya kufanya utafiti wa kina na upembuzi yakinifu nimeona kwamba ilani tunayoitumia sasa hivi haipo makini katika kuibua vyanzo vipya vya uchumi na kusimamia vile vilivyokuwepo. Kwa mfano Mhe. Spika, mpaka kufika mwaka 1976 Zanzibar ilikuwa ina zao hili la nazi na karafuu, ilikuwa inaongoza sana katika suala zima la uchumi wa nchi. Mnazi katika nchi hii ulikuwa ukichangia karibu asilimia 30 ya uchumi wa nchi. Inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba kipindi kile Waziri wa Kilimo alikuwa hata hana digrii lakini aliweza kutumia zao la mnazi kuweza kuleta tija kubwa katika nchi. Leo hii Serikali yetu ina madaktari, Serikali yetu ina maprofesa lakini mnazi unaweza kupotea na hakuna uwezo sasa wa kuibua chanzo kingine.

Mhe. Spika, naiomba Serikali isifanye muhali katika hili na kututafutia vyanzo vipya vya mapato. Vipo Mhe. Spika, lakini inaonekana kwamba katika utaratibu tuliona siasa za nchi zinatumiya uchumi, uchumi hautumikii siasa, na huu ni mwiko. Lazima tuhakikishe kwamba siasa siku zote Mhe. Spika, inatumikia uchumi. Ni dhambi kubwa katika nchi uchumi kutumikia siasa.

Mhe. Spika, sisi kule Bara kuna asilimia 4.5 ya misaada na mikopo kutoka nje. Naomba Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee atakapokuja hapa aje anipe *breakdown* ya fedha tulizozivuna kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kiasi gani katika kipindi hichi cha miaka 10 hiyo 4.5 tumepata katika mikopo na misaada. Ni kiasi gani tumetumia fedha zetu ambazo zimo katika Bodi ya Mikopo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasomeshea watoto wetu. Mimi nadhani Mhe. Spika, tusiogope kuhoji haya, Mawaziri wetu wasiogope. Hii Serikali imekaa madarakani na imewekwa na wananchi sisi tupo nyuma yenu. Mkifika pale mkikamata kamata maneno mkibabaisha hamjidhalilishi nyinyi mnatudhalilisha sisi kabisa kabisa. Mhe. Spika, mimi nadhani kuna fedha zetu nyingi sitaki niseme kama zimeporwa lakini hatujapewa. Nataka atuteletee atakapokuja kufanya *breakdown* hapa Mhe. Waziri wa Fedha ni mtoto wangu, najua ni mtaalamu sana katika mambo ya kutafiti na kukusanya maneno aje atuelezee hapa.

Mhe. Spika, tuje katika kilimo. Kilimo Mhe. Spika, ni tatizo katika nchi kwa sababu hivi sasa kimekabiliwa na matatizo mengi. Kuna matatizo haya ambayo yanalikabili taifa letu ni tatizo kubwa la mabadiliko ya tabia nchi. Sasa nimeangalia katika huu Mpango wa Uchumi wa Mhe. Waziri nikataka kujua *economic strategy* ameweka ili kuiwezesha Zanzibar kupambana vizuri na mabadiliko ya tabia nchi. Ninasikitika kwamba tunategemea zaidi wafadhili; ni tatizo, kwa sababu kilimo kimeajiri karibu asilimia 80 ya Wazanzibari, leo kuendelea kutegemea wafadhili tu ni kujiingiza katika utumwa wa khofu. Mhe. Spika, naogopa sana katika hili, kwa hiyo atakapokuja Waziri hapa kufanya *windup* aje atueleze ana mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kuweza kuifanya Zanzibar kupambana na haya mabadiliko ya tabia nchi.

Kuna mama mmoja nilipokuwa katika Bunge la Katiba alisema lazima mhakikishe kwamba mnataka Muungano kwa sababu visiwa vinazama vile ili vikija vikizama muwe mshakuwepo huku. Sasa hii atwambie. Mimi nataka yeye ili kuepusha kupelekwa kule Bara kwa sababu sisi wengine hatukuhusu kule, zaidi tumehusu upande wa Lamu na Pate kule. Basi atwambie ana mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kuhakikisha kwamba Zanzibar inapambana na haya mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Spika, nimuulize Waziri tatizo liko wapi, huyu Waziri wa mambo ya Uchumi na Mipango ya Nchi. Sisi na Mauritius sote ni visiwa katika Bahari ya Hindi. Na katika miaka ya 70 lile pato la Mauritius na pato la Mzanzibari sote tulikuwa tunapata dola 70 kwa mwaka. Inasikitisha sana Mhe. Spika, katika miaka hii sisi Wazanzibari pato la mwananchi kwa mwaka mzima ni dola 70. Wamauritus wao wale wale *population* yao 1.3 milioni na sisi 1.3 milioni, wao wana mwamba kule wanategemea kilimo na sisi tunategemea kilimo, wao *per capital income* yao ni dola 1,000 kwa mwananchi tatizo liko wapi? Kwa nini katika miaka ile ya Mzee Thabit Kombo akiwa ni Katibu Mkuu wa Afro Shirazi aliyesimamia masuala ya Uchumi ilikuwa wao wana 700 na sisi tuna 700, wao walikuwa 360 na sisi tulikuwa 360 mpaka mzee Thabit Kombo pale anayo Afro Shirazi yake akiwa Katibu Mkuu wao wana 360 na sisi tuna 360 wala hajaenda skuli.

Lakini sasa Wizara hii anayoongoza mtaalamu; *Doctor, per capital income* ya Mauritius ni dola 1,000 kwa mwaka, sisi Wazanzibari dola 70 aniambie Waziri tatizo liko wapi. *Population density* ni sawasawa, *area* sisi Zanzibar ni kubwa zaidi kuliko Mauritius tatizo liko wapi? Tunashindwa, uchumi unapenya, kama ni usomi mbona wale kina Mzee Thabit Kombo na wengine wale waliokuwa hata hawajaenda skuli walikuwa wakitufanyia vizuri. Tunataka

mtueleze wataalamu hapa ikiwa tatizo ni Ilani ya Uchaguzi basi tuachieni sisi hiki kilichobakia tutumie hii ya kwetu, nakuhakikishia mimi mambo yatakwenda vizuri na mtaendelea kuongoza nyie nyie.

Mhe. Spika, sasa niendemoja kwa moja kwenye suala zima la hawa wenzetu wa makundi maalum.

Mhe. Spika, ulimwengu mzima hawa wenzetu walemavu sasa hivi wanathaminiwa. Mimi hivi karibuni nilikuwepo London pale, nikaingia katika *public transport*, nilikuwa nimeshaka akaingia mlemavu nikaambiwa niinuke akae yeye na niliridhika. Wenzetu wanawatunza sana.

Juzi tulikuwa na mkutano sisi hapo juu wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika ukumbi wako hapo Mhe. Spika, anataka kupanda Mkurugenzi juu kwa bahati mbaya yule mama ni mlemavu akawa hajiwezi kaja pale, mimi nilikuwa Makamo Mwenyekiti nikasema hapana bwana! Huyu mama asijikalifishe, kwa bahati tena tukaenda tukafanya kule kwenye *cafeteria* pale, jambo ambalo sio kwamba tulimdhaliisha tu yule mama mpaka Kamati kwa sababu ilikuwa joto ni kali sana na sehemu hatusikilizani vizuri, lakini tulilazimika kufanya pale ili yule mama aweze kufika.

Mhe. Spika, sasa nilikuwa ninafikiria katika bajeti hii, ningeona kwamba serikali imeweka mkakati gani katika kuhakikisha inawawezesha hawa kuweza kukabiliiana na miundombinu iliyopo. Hawa ni binadamu, nataka serikali ijue kwamba hawa walemavu ni binadamu na Mwenyezi Mungu katuumba katika rangi na makabila tofauti tujuane tu, na binadamu wote ni sawa.

Sasa kumuweka mlemavu akadhaliika sio kwamba tunafanya *political betrayal* lakini mpaka tunafanya mpaka *humanism betrayal*. Kwa hivyo yule bwana mipango na uchumi anieleze ana mpango gani wa muda mrefu na mfupi kuhakikisha kwamba miundombinu ya nchi hii inakuwa rafiki kwa wale watu ambao wana ulemavu, aje anieleze hapa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwa sababu bado dakika 5. Ninaungana na hoja za Mhe. Mohammedraza Hassanali, nilikuwa nataka nijue, nifafanuliwe kwa sababu hawa wenzetu ni wajanja. Sisi tunasema ndugu zetu wa damu lakini nasema nataka kujua kuhusu hizi bilioni 27 ambazo amezitungumza mdogo wangu pale Mhe. Mohammedraza Hassanali. Huu kweli ni msaada au fedha za SMZ hizi? Tusipangaliane maneno tu.

Mhe. Spika, hilo nadhani nimalizie kwa kuwaambia wenzangu kwamba huu utalii. Utalii *is a volatile economic system; tourism is a volatile economic system*. Ikiwa ni kitu ambacho kinaruka tu kwa upepo. Sasa sisi tunasema kwamba nchi yetu inategemea *nearly 50 percent* ya uchumi wake kupitia *tourism*, uchumi ambao unahitaji utulivu wa hali juu, pakiwa na zogo kidogo tu, utalii unaruka; *is a volatile economic*. (Makofi).

Sasa wewe kama unakuja hapa unasema kwamba nchi hii haipatikani isipokuwa kwa bunduki, isipokuwa kwa nini, huku ikiwa bunduki zote. Kama mimi nasema tukishaharibu amani ya nchi, uchumi wetu wa utalii unategemea amani. Mukifanya mchezo hata mishahara tutashindwa kuwalipa hao, hata vikosi wanaweza wakaja wakatupiga kwa sababu tumeshindwa kuwalipa. (Makofi).

Mhe. Spika, utulivu uliopo tuenzi na musihubiri kwamba serikali hii imepinduliwa, haitolewi kwa vikaratasi. Sasa hebu gawa hizo risasi, bunduki na ndege zote zile za kivita, halafu mutangaze vita!

Mhe. Spika, ahsante sana. (Makofi).

Mhe. Spika: Ahsante. Ni zamu yake sasa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na anayefuata baadae tutamfahamu baada ya kuleta jina lake.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti yetu hii.

Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na timu yake kwa jumla kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya hadi hatimaye leo hii tumefika hapa na kuanza kuchambua bajeti yetu hii.

Mhe. Spika, mimi nianze tu kwa mapitio ya kitabu chetu cha kwanza; cha hali ya uchumi mwaka 2013 na utekelezaji wa mpango wa maendeleo Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwa kuanzia naanza kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka mwaka 2009-2013. Mimi ninaanza mwaka 2010 pale ambapo Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein amechukua madaraka na kuwa Rais wa nchi yetu ya Zanzibar hadi leo hii.

Mhe. Spika, mwaka 2010 uchumi wa Zanzibar ulikuwa asilimia 6.4 lakini mwaka 2011 uchumi wa Zanzibar umekua hadi kufikia asilimia 6.6. Mwaka 2012 uchumi wa Zanzibar umekua kutoka asilimia 6.6 hadi asilimia 7.1 na mwaka huu (2013/2014) uchumi wa Zanzibar umekua kwa asilimia 7.4.

Mhe. Spika, nilikuwa nikiyazungumza haya ili katika kitabu chetu hichi tulichokuwa nacho hapa nilijaribu kupitia chumi za nchi nyengine za Afrika zilizomo ndani ya Jangwa la Kusini mwa Afrika ambapo kuna vigezo vya nchi nyingi tu, zaidi ya nchi kumi lakini mimi kutokana na muda sitopendelea kupita huko. Lakini ningeliomba kuwafahamisha baadhi ya Wajumbe ili waweze kuangalia chumi za nchi za wenzetu.

Kwa mfano Nigeria mwaka 2009 ilikuwa uchumi wake ni asilimia 7.0. Mwaka 2010 asilimia 8.0 lakini mwaka 2013 ni asilimia 6.3. Sasa hapa watu waangalie namna gani mambo haya yanavyokwenda kwa upande wetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo mimi nakuja katika kitabu chetu hiki cha Mhe. Waziri wa Mipango ambaye aliyekuja kutoa hapa, naomba kunukuu baadhi ya mambo humu kwamba anasema taarifa hizi ni sehemu ya utekelezaji wa dira ya maendeleo ya 2020 kwa Zanzibar, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar (MKUZA II) lakini pia ni utekelezaji wa mipango ya miaka 5 ya MKUZA II na ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika kitabu ambacho Mhe. Waziri amekuja kutupatia hapa. Tumejaribu kwenda zaidi ndani ya kitabu hichi, tulisikiliza hotuba ya Mhe. Waziri lakini zaidi nilisikiliza vile vile hotuba ambayo ilitolewa na Mwenyekiti wa Wenyeviti. Taarifa ambayo ilikuwa inawahusu wenyeviti wote wa kamati zako zote saba ambazo zimo ndani ya Baraza hili.

Mhe. Spika, ningeliomba kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, ninamuomba Mhe. Waziri hotuba ile aichukue na aifanyie kazi na itamuongoza katika mambo mengi sana yatakyoweza kuleta maslahi na maendeleo katika nchi yetu. Mhe. Spika, katika hotuba ile yamezungumzwa mengi na yote ni ya msingi na yote ni ya maana na yote yanahitajiwa kufanyiwa kazi kwa namna ambavyo sisi wenyewe tuliona kwamba inafaa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa ninakuja katika kuiangalia taarifa ambayo Mhe. Waziri aliitoa hotuba yake katika Baraza lako hili tukufu. Mimi Mhe. Waziri wa Fedha nimeigawa katika maeneo sita. Tukiangalia baada ya hapo vile vile niliangalia suala zima la deni la taifa lakini pia niliangalia umakini wa mikataba ya miradi ya maendeleo ambayo inaendelea kutengenezwa na kufanyiwa kazi ndani ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia jambo la msingi zaidi kuliko yote haya ni kwamba ninaunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia 99.8 bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, baada ya hatua hiyo nije katika hotuba ya Mhe. Waziri. Hotuba ya Mhe. Waziri ya bajeti tukiiangalia katika eneo la kwanza tunakuta kwamba hotuba hii imezingatia uwezo wetu tulionao na ndani ya miaka mitatu, tulikuwa tupo katika hali gani ya kiuchumi na mambo gani ambayo tulikuwa tunayo, mambo gani yalitukwaza, mambo gani tuliweza kuyafanya, mambo gani yalikuwama, yale yote waliyazingatia na baadae kuweza kuyafanyia marekebisha na vile vile kuweza kujipanga kwa ajili ya utekelezaji na kutatua matatizo ambayo yanatukabili katika nchi yetu.

Mhe. Spika, na hili ni jambo ambalo limeonekana kwamba wizara kwa kuzingatia na vile vile kuwa na utaratibu mzuri wa kuangalia mafanikio na yale mambo ambayo hayakufanikiwa, wameweza kutengeneza utaratibu imara na makini ambao utaweza kutuvusha hapa tulipo na kuweza kutuletea maendeleo zaidi ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, lakini pia hotuba hii ya bajeti imejaribu kuelekeza nguvu zaidi kwenye bajeti ya kawaida, yaani ni matumizi ya kawaida. Na vile vile bajeti hii imezingatia zaidi kuendeleza miradi mikubwa na ambayo ni muhimu ambayo ilikwama katika kipindi kilichopita cha miaka mitatu iliyopita, na sasa wamejaribu kuikwama miradi ile, na kwa sasa hivi wamejaribu kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha kwamba miradi ile inafanikiwa. Lakini wakati

wanafanya hivyo mimi kwa upande wangu ningeliwaomba zaidi wazingatie ukomo wa kujiwekea wao wenyewe kuhakikisha kwamba miradi hii ilifana, na kwa wakati ambao walikuwa wamejipangia.

Mhe. Spika, vile vile hotuba hii ya bajeti imeelezea namna ya kodi ilivyoongezwa, ilivyokuwa haikuongezwa isipokuwa kilichofanyika ni marekebisho tu ndani ya baadhi ya maeneo, hususan katika sekta ya bandari na mambo ya anga. Hili ni jambo la kuridhisha na jambo ambalo litaweza kusaidia kuhakikisha kwamba tunajipanga vizuri ili katika mwaka wa fedha unaofuata mambo yetu yaweze kuwa mazuri.

Mhe. Spika, lakini pamoja na yote hayo niliangalia na nikakuta kwamba kuna ongezeko la asilimia 18.7 hivi katika masuala ya kutengeneza *scheme of service*. Hii haina maana kwamba kuna ongezeko la mishahara lakini kuna maslahi mazuri ambayo wafanyakazi wataweza kuyapata ili waweze kufanya masuala yao ya kimaisha yaweze kwenda vizuri.

Mhe. Spika, lakini pia bajeti hii imelenga zaidi kutumia raslimali zetu za ndani na kuondosha na kuepusha matumizi mabaya, kama vile mfano pale tulipoona kwamba badala ya kutumia fedha nyingi kwenda kufanya mikutano sehemu za nje katika mahoteli mbali mbali ya kitalii pamoja na kufanya safari za nje, bajeti hii imeonekana kwa kiasi gani kwamba wataendelea kutumia kumbi zetu za kawaida kama vile Hoteli ya Bwawani na maeneo mengine mengine na vile vile kufuta kwa kiasi kikubwa safari za nje kwa viongozi wetu na watendaji wetu ambao wamo ndani, isipokuwa zile safari za ulazima.

Mhe. Spika, lakini pia ningeliomba vile vile hii miradi ambayo iliyokuwa inatengenezwa ndani ya nchi yetu, izingatiwe sana suala la kuweka ukomo ili miradi hii iendane na wakati. Lakini pamoja na juhudi zote na mipango yoyote vile vile, niliangalia sekta ambayo zilikuwa zimepewa kipaumbele. Katika bajeti hii kipaumbele cha kwanza ilikuwa ni sekta ya utalii. Ni jambo zuri, ni jambo la busara, ni jambo la kutia moyo.

Mhe. Spika, lakini tunahitaji kuweka mikakati makini, mikakati imara ya kuhakikisha kwamba watalii wanaokuja Zanzibar wanaisaidia Zanzibar na watu wake, sio kwamba watalii wanaokuja Zanzibar wananeemesha watu wachache. Ningeliomba serikali kutengeneza utaratibu makini na imara utakaowezesha kuhakikisha kwamba watalii hawa wananufaisha Zanzibar na pato letu linanyanyuka. Kwa sababu ukiangalia katika takwimu zilizokuwemo katika vitabu, ongezeko la watalii ukilinganisha baina ya mwaka jana na mwaka huu, mwaka jana tulikuwa na watalii 161,000. Mwaka huu tuna watalii kama 180,000 naa. Bado ni ongezeko dogo ukilinganisha na yale malengo ambayo yamewekwa mpaka mwaka 2015 tuweze kuwa na watalii 500,000 katika visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Spika, ukiangalia sekta ya ajira vile vile ningelipenda sekta hii iangaliwe upya. Kwani bado tuna wimbi kubwa sana la vijana ambao bado hawana kazi za kuweza kujiendesha kimaisha. Ningeliomba vile vile Waziri atakapokuja baadae atusaidie kutufahamisha utaratibu gani uliowekwa, kwa sababu sote tunafahamu tu kwamba kuna mifuko ya JK na AK, kuna mfumo wa uwezesaji. Lakini watu wetu hawaelewi ni namna gani wanaweza kuneemeka na mifuko hiyo.

Mhe. Spika, tungelimuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako kuweza kupata maelekezo na namna ya watu wetu vipi wanaweza kufaidika na mifuko hii badala ya kufaidisha watu wachache.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimeliona ningelipenda kutilia mkazo vile vile kupata mwelekeo na maelezo hasa yatakayoweza kufanikisha suala zima la kilimo chetu hichi cha mpunga, jina la NERICA ambalo tulianza nalo toka mwaka 2010 hadi hivi sasa ambapo tunaomba suala hili liweze kufikia malengo ambayo tulikuwa tumejiwekea kwa ajili ya kutatua na kuwasaidia Wazanzibari kuondokana na tatizo la chakula, na vile vile kupunguza kasi pamoja na uingiaji mkubwa wa vyakula kutoka nje.

Mhe. Spika, wakati ninazungumzia hili vile vile ningeliomba serikali iangalie uwezekano wa kutimiza yale matakwa yanayohusiana na akiba ya chakula ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar na nchi yetu kwa ujumla. Pamoja na yote hayo ningeliomba vile vile kuishukuru serikali kwa namna ambavyo imeweza kuwasaidia vijana wetu hususan vijana wetu wa *form six*; ambapo wameondoshewa malipo yale ambayo yalikuwa ni mzigo mkubwa kwa wazee wetu, na sasa hivi serikali kuchukua dhamana ile. Tungeliomba utaratibu ule upangwe vizuri zaidi ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wote wanafaidika na utaratibu ule na suala la rushwa lisije likaingia hapa ili kuathiri elimu kwa watoto wetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono tena hotuba ya mapendekezo ya makadirio na mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2014/2015 kwa asilimia 99.8

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niseme tumeridhika na michango iliyotolewa, kama bado basi ningepata majina. Ingekuwa ni muda wa kutosha kumpa Mhe. Waziri ningemwambia sasa hivi afanye majumuisho. Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na nafasi ya kujadili bajeti hii ya 2014/2015.

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Sasa naomba nianze na mchango wangu kwenye ukurasa wa 10 au wa 19. *Paragraph* hii Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha ameendeleza maneno yake ya siku nyingi kama uchumi wetu unakua. Na mara hii maneno yake ameyatia chumvi.

Mhe. Spika, alipoandika naomba niyanukuu, "Uchumi umekua kwa asilimia 7.4 mwaka 2013 ikiwa ni kiasi kikubwa zaidi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar katika kipindi cha miaka 10 iliyopita".

Mhe. Spika, sasa bila shaka haya ni maneno ya kujifurahisha serikali yetu. Lakini ninalotaka kwa Mhe. Waziri anifahamishe ukuaji huu wa uchumi una faida gani kwa mwananchi mkulima? Nini faida ya ukuaji huu wa uchumi kwa mvuvi wa Zanzibar? Vile vile anifahamishe nini faida ya ukuaji huu wa uchumi kwa mfugaji wa Kizanzibari.

Mhe. Spika, vile vile namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ukuaji huu wa uchumi una faida gani kwa mzee wa Kizanzibari anayelazimika kutoa michango ya skuli ili mwanawe asome. Vile vile namuomba Mhe. Waziri anifahamishe nini faida ya ukuaji huu wa uchumi kwa kijana wa Kizanzibari aliyemaliza chuo, anahangaikia ajira, na ambaye kila mara anafanya usaili wa tangazo la ajira bila ya kupata kazi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aniambie ukuaji huu wa uchumi unaleta faida gani kwa kijana wa Kizanzibari ambaye ameanguka mkarafuu na kulazimika kwenda Bara kuhangaikia matibabu kwa gharama zake. Pia namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ni faida gani ya ukuaji huu wa uchumi kwa Wazanzibari waliostaafu, wakilipwa pencheni ndogo isiyokidhi chakula cha hata siku kumi katika mwezi.

Vile vile namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ni faida gani ya ukuaji huu wa uchumi kwa Wazanzibari wanyonge wasioweza hata kumudu mlo wa siku moja bila ya kusaidiwa na wasamaria wema.

Mhe. Spika, haya ndio baadhi ya maswali ambayo majigambo ya Mhe. Waziri kwamba uchumi wa Zanzibar umekua kwa kiwango kikubwa yangeweza kupata jawabu. Vyenginevyo ukuaji huu utabakia kwenye vitabu vya bajeti, lakini ukienda kwa wananchi utaendelea kuwaona wananchi wetu, umaskini na unyonge unazidi kuwaathiri sana.

Mhe. Spika, katika aya ya 33, ukurasa wa 16, Mhe. Waziri ameandika kwamba katika kipindi hiki misaada ya kibajeti iliyopatikana ni bilioni 27.2 ambapo ni ongezeko la asilimia 32. Mhe. Spika, kauli hii ya Mhe. Waziri unaweza ukaitafsiri kama ni mafanikio makubwa. Lakini kuna jambo limenipa utata na naomba nipate usahihi wake. Waziri wa Fedha, Mhe. Saada Mkuya alipokuwa akiwasilisha bajeti ya Muungano, tarehe 30 Aprili mwaka huu 2014, nilimfahamu aliposema mapato halisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yanayotokana na misaada na mikopo nafuu ya nje ni shilingi trilioni 1.163.

Swali langu Mhe. Spika, maneno haya ya Mhe. Saada yana ukweli kiasi gani, na ikiwa ni kweli katika fedha hizo Zanzibar inastahiki kiasi gani na kwa *formula* ipi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi mzuri, isije kuwa mfumo huu wa Muungano unatupunja mgao wetu.

Mhe. Spika, katika aya ya 68, ukurasa wa 34 Mhe. Waziri anasema kwamba mishahara ya wafanyakazi wa serikali itachukua asilimia 55 ya matumizi yote ya kazi za kawaida za serikali. Hapa maana yake ni kwamba Mhe. Spika,

wananchi wote wanalipa kodi mbali mbali katika shughuli zao za kawaida, lakini wanaonufaika kwa kutumia asilimia 55 ya pato ni wafanyakazi wachache wanaofanya kazi serikalini. Sasa Mhe. Spika, je sera hii ni ya haki.

Kodi hii inawanufaisha vipi wananchi wasio na kazi za serikali, na je ni haki kwamba mlipa kodi yeye alipe kodi, lakini wanaofaidika na kodi hiyo ni wale walioajiriwa. Mhe. Spika, maoni yangu ni kwamba sera hii inayotekelezwa ina mapungufu makubwa. Haiwezekani asilimia 55 ya makusanyo ya kodi ya wananchi wote itumike kulipa mishahara ya waajiriwa wachache na wananchi waliobaki wasifaidike na kodi zao. Sera hiyo ni mbovu na ndio inayowafanya wananchi wakwepe kulipa kodi.

Mhe. Spika, katika aya ya 69, ukurasa wa 35 Mhe. Waziri anaeleza kwamba uzalishaji wa mpunga umefikia tani 33.655. Mhe. Spika, hizi takwimu ni bora zikathibitishwa vizuri, ni bora tueleze uzalishaji huu umefanyika wilaya zipi na katika mabonde yepi? Kwa sababu Mhe. Spika, tunapopita kwenye mashamba ya mipunga, wakulima wa mipunga wanalalamika kwamba hali ya upatikanaji wa mpunga ni mbaya na hata sisi wenyewe Mhe. Spika, kama mimi ni mkulima hali hiyo naiona. Kwa hivyo, nahisi hizi ni *data* za kuchakachua na kujifurahisha zaidi.

Mhe. Spika, ningetaka kufahamu uzalishaji huu tulioambiwa ni kwa mpunga unaotegemea mvua au ni mpunga wa kumwagilia. Ni vizuri tukaambiwa uongezekaji huo umeongezeka kutoka tani ngapi kwa mpunga unaotegemea mvua hadi tani ngapi, na tani ngapi kwa mpunga wa umwagiliaji hadi tani ngapi? Vile vile katika wilaya zetu uongezekaji huo ukoje?

Pia Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atueleze, kuongezeka huko kwa mpunga kumepunguza vipi uangiziaji wa mchele kutoka Tanganyika na nchi za nje. Vile vile namuomba Mhe. Waziri aniambie kuongezeka huko kumeokoa pesa kiasi gani za fedha za kigeni katika kuagizia huo mchele.

Mhe. Spika, katika sekta ya mipango kuna jambo limetokea na bahati mbaya sana Waziri anayeshughulikia masuala ya uchumi hajalipa mazingatio. Jambo lenyewe ni kilimo cha mwani. Mhe. Spika, takwimu zinaonesha kilimo cha mwani kilianza kupata nguvu na kuwakomboa wananchi hasa wanawake vijijini, matokeo yake uzalishaji wa mwani uliongezeka hadi kufikia tani 14,000 mwaka jana, lakini taarifa nilizonazo mwaka huu uzalishaji wa mwani umepungua.

Mhe. Spika, utafiti mdogo niliufanya kupungua kwa uzalishaji wa mwani kumesababishwa na mambo mawili. Moja sera zinazotekelezwa zimeshindwa kutafuta bei nzuri kwa wanawake Wazanzibari wanaolima mwani, hivyo kuwafanya wavunjike moyo.

Pili, kumeingia maradhi yanayousababisha mwani kuharibika huku serikali ikishindwa kutafuta dawa ya maradhi hayo ya mwani. Mhe. Spika, serikali kushindwa kutafuta suluhisho na ufumbuzi wa matatizo ya mwani ni jambo baya sana kwa wanawake Wazanzibari na kwa kweli hawatutendei haki. Mhe. Spika, na hilo serikali lazima inipe majibu yatakayoleta ufumbuzi.

Mhe. Spika, naiomba sana serikali isipuuze shughuli za kiuchumi za wanawake, kwani wanawake wana mchango mkubwa katika taifa hili.

Mhe. Spika, kwa kumalizia bado bajeti hii na mipango yake haiwezi kumtoa Mzanzibari katika umaskini wa kipato alionao, na bila ya kuwa na mipango na sera nyengine madhubuti, kasi yetu ya maendeleo itakuwa ni ya kujikongoja sana.

Mhe. Spika, sitaki niitumie lugha ambayo niliitumia mara moja hapa, wenzangu wakaniambaia sio nzuri, lakini kwa kweli ukiangalia hii bajeti, utaona kwamba mara ile nilisema wanatambaa kwa nini, lakini nafikiria haitaweza hata serikali kukaa kitako, nakhofia kurudi kule kule nilikoambiwa nisije nikaendelea tena kuchangia hivyo.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na namuomba Mhe. Waziri anipe majibu ili nipate kuunga mkono haya mambo, lakini ikiwa hakuna jawabu nzuri hasa majibu ya mwani kwa wanawake, basi nafikiria waliona wasanii patachimbika. Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Nimkaribishe basi Mhe. Abdi Mossi Kombo.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii adhimu ya kutoa mchango wangu huu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu katika kitabu hiki aya 56, ukurasa wa 43 kwanza naanza kunukuu;

"Katika kuimarisha miundombinu muhimu ya usafiri, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara zinazolingia mjini, za Fuoni na Bububu".

Mhe. Spika, tumesahau Bunge la Katiba kule. Miundombinu ya barabara katika Zanzibar bado ina matatizo makubwa sana. Kwanza barabara zetu ni mbovu tena ni nyembamba, msongomano wa magari hususan mjini umekuwa ni mkubwa sana. Kwa hivyo, serikali naiomba iangalie sana miundombinu ya barabara.

Mhe. Spika, nikiondoka mjini nielekee upande wa Kaskazini Unguja. Ukitoka hapa mjini ukielekea Kaskazini Unguja utakuta barabara zetu ni mbovu, madaraja mabovu, hayakidhi haja, ni hatari tupu. Kwa hivyo, naiomba serikali iangalie sana miundombinu ya barabara tuliyonayo. Barabara ni moja katika uchumi wa nchi, wananchi wanahitaji barabara, maendeleo makubwa wanapata katika barabara, hususan barabara hii ya Kaskazini kutoka mjini hadi Mkwajuni, Chaani. Barabara hivi sasa zinachunwa kama samaki, zinaparwa. Sasa mparo ule unaoparwa barabara zile ni mashimo matupu. Kwa hivyo, naiomba serikali iangalie miundombinu hii ya barabara zetu hivi sasa ni hatari.

Tukiondoka Mkwajuni kwenda Mkokotoni mpaka Chaani. Nakwenda sasa eneo la Matemwe kunaitwa barabara ya Kijini. Barabara hii Mheshimiwa hivi sasa inafika miaka 50 kama Mapinduzi ya Zanzibar, lakini haifikiriwi, haijadiliwi na wala haitizamwi na serikali. Kwa hivyo, naiomba serikali bajeti ya mara hii iangalie sana barabara ya Kijini, kwa sababu hata watalii wetu hivi sasa wengi sana wanahitaji barabara hii, kwa sababu kuna Kisiwa cha Mnemba. Katika Kisiwa cha Mnemba watalii wengi wanaokuja Zanzibar wanakwenda katika Kisiwa cha Mnemba, lakini barabara wanayopitia ya Kijini ni mbovu haikidhi haja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akija hapa kutupa maelezo na majumuisho yake atuhakikishie ni lini serikali itajenga barabara ya Kijini. Barabara hii kwa kutoka ilani yetu ya uchaguzi, Mhe. Rais Ali Mohamed Shein wakati anakwenda kuomba kura kwa wananchi wa Kijini, aliwahakikishia kwamba pindipo mkinipa ridhaa basi nitafikiria kuijenga barabara ya Kijini, lakini hadi leo miaka ya Rais Mhe. Ali Mohamed Shein inataka kumalizika, barabara ya Kijini bado iko vile vile. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake, basi awahakikishie wananchi wa Kijini ni lini barabara yao itajengwa.

Nakwenda katika miundombinu ya Kilimo. Mhe. Spika, miundombinu ya kilimo Zanzibar bado iko katika hali duni ukilinganisha na wenzetu wa duniani. Kilimo chetu hivi sasa hakijawa na miundombinu ya aina yoyote angalau ya kuvuna mpunga.

a) Mimi namuomba Mhe. Waziri aje atuhakikishie, ni tani ngapi Zanzibar zinavunwa mpunga unaolimwa na wananchi na serikali yenyewe.

b) Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atuhakikishie kwamba kuna visima vingapi vinavyomwagilia maji hapa Zanzibar; ambavyo wakati wa kiangazi visima hivyo vinafanya kazi ili mazao ya mpunga yawe yanalimwa kama kawaida?

Mhe. Spika, tukienda katika miundombinu ya kilimo, bado zana za kilimo hasa pembejeo viko duni. Matrekta hatuna, dawa za kumwagilia mimea hafifu na zinapokuja wananchi wanakuwa na matatizo sana kuzipata na sana bei, wananchi wetu bado wangali duni sana yaani maskini wa kuweza kumiliki madawa. Kwa hivyo, naiomba serikali ifanye hafifu juu ya wakulima.

Mhe. Spika, nikienda katika utalii. Kama tunavyoambiwa kwamba idadi kubwa ya pato letu la Zanzibar linatokana na utalii, lakini bado miundombinu ya utalii hatujakuwanayo. Hasa utalii wetu zaidi uko katika Mashariki ya Zanzibar, kama Matemwe, Kiwengwa na Nungwi. Lakini bado miundombinu hasa hii ya barabara, kwa sababu barabara zetu ni chafu bado na watalii wanataka barabara ziwe safi na nzuri. Barabara zetu hata ukipita njiani usiku

basi uwe na tahadhari ya majambazi, hakuna taa wala hakuna chochote. Kwa hivyo, naiomba serikali iingalie sana miundombinu hii ya barabara katika mambo ya utalii.

Mhe. Spika, halafu ndani ya utalii, serikali imeweka utalii kwa ajili ya kupunguza matatizo ya vijana wetu kupata ajira, lakini bado vijana wetu wa Zanzibar, hususan sehemu zetu za Mashariki, bado vijana wanasumbuka sana kupata ajira katika mahoteli yao yaliyowekwa katika sehemu zao wanazoishi. Kwa hivyo, serikali ni lazima ijitahidi ili kuhakikisha kwamba vijana wa Zanzibar wanapata kazi katika mahoteli kuliko wale wageni.

Mhe. Spika, tatizo kubwa hivi sasa linalotupata katika hayo mahoteli ni wale ma-*PO*, ma-*PO* wanasumbua sana. Kwa sababu ma-*PO* wengi wanatoka sehemu za Bara, sasa ni tatizo sana kuwapatia vijana wa Zanzibar kazi ndani ya mahoteli. Leo *PO* anatoka Arusha, *PO* anatoka Morogoro, ni tatizo kubwa kumpatia kazi kijana wa Matemwe. Yuko radhi akamchukue kijana kutoka Arusha aje amlete pale, kijana wa Matemwe anamwambia hakusoma.

Kuna vijana sasa hivi wamesoma kikweli kweli. Kwa hivyo, hili ni tatizo kubwa ambalo linatupata ndani ya mahoteli yetu. Kwa hivyo, serikali ni lazima iingalie, wizara inayohusika ihakikishe kwamba vijana wetu wanapata kazi ndani ya mahoteli. Kwa sababu sisi wa Zanzibar tumeza maeneo yetu, tumeza minazi yetu ili tupate kazi ndani ya mahoteli, wale watoto wetu waje wafanye kazi mule. Sasa ikiwa leo wale watoto wetu tuliouza minazi mule na maeneo yetu ili kujengwa ule utalii, baadaye utalii ule sisi hatuupati, kuna faida gani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atuhakikishie kwamba vijana wa Zanzibar watapata kazi ndani ya mahoteli yale.

Mhe. Spika, nikimalizia nakwenda katika Wizara ya Afya. Wizara ya Afya bado nako kuna matatizo ya madawa, kuna baadhi ya mahospitali mengine yanavuja. Hasa kule katika Jimbo langu sehemu ya Kijini, kuna hospitali masika haya sasa hivi basi wale wagonjwa bora wakakae chini ya mibuyu, maana yake watapata usalama watavujiwa maji lakini kuna usalama wa kuvunjikiwa na ile nyumba, kwa hivyo naiomba Serikali iingalie jengo la Wizara ya Afya la Kijini ni bovu haliridhishi.

Mhe. Spika, ili kwa kuchunga wakati wako nisiseme sana naomba nikushukuru (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa jioni hii au magharibi haya na labda kwa mwaka wa nne sasa nitapata fursa ya kuzungumzia maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Spika, ukiangalia kitabu tulichopewa mwaka jana na kitabu cha mwaka juzi na mwaka huu unaona kama vile ni mwendeleo tu wa maneno, na kiujumla wataalamu wa siku hizi wanaweza kutumia kompyuta kuwa yale maneno yapo, kwa hivyo wanaweka na wanabadilisha badilisha baadhi ya *figure* tu, lakini baadhi ya maneno yanakuwa yapo pale pale, kidogo tu tunachobadilisha.

Mhe. Spika, mpango huu kila ukiuungalia unahisi kwamba ni mpango uliokuja au unaotayarishwa kwa kuwatunishia wale wanaofanya kazi Serikalini au watumishi wa umma wao kupata mishahara, lakini wale ambao hawapo katika sekta hii ya watumishi wa umma wao kazi yao kubwa ni kunyonywa; yaani kutozwa kodi ambayo mwisho wake wao haiwafikii, kwa sababu miradi mingi kama walivyosema wengine hiyo iliyotajwa ya maendeleo basi Mhe. Spika, Serikali haikuweka fungu la kutosha ya kuiendeleza. Kwa maana hiyo miradi hii inategemea ufadhili ambao nasema mpaka hivi sasa nathubutu kusema ni mwaka wa nne sijui ni mradi gani ambao tayari umemalizika na wananchi wanafaidika.

Kila bajeti inayokuja kiujumla Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo maneno ni yale yale, mwaka uliopita hapa kumbukumbu zangu tulibadilisha na tulifanya marekebisho ya sheria nne za kodi. Na mwaka huu tunataka kufanya tena mabadiliko ya sheria za kodi lakini sheria hizi hazibadiliki; ni sheria ya kodi ya mafuta, ada ya bandari, ada ya uwanja wa ndege, leseni ya njia, leseni ya mwenye kutumia chombo. Hizi zote Mhe. Spika, tukisema leseni ya njia sio ile barabara inayotoa hiyo ada, tukisema ada ya mafuta sio yale mafuta, ni mwananchi, ndiye anayetoa, sasa sijui *vision* yetu au muono wetu uko wapi, kiasi kwamba Serikali imeshindwa moja kwa moja kuibua vyanzo vyengine, chanzo kikuu chetu cha mapato basi ni mwananchi, hebu tubadilike.

Mhe. Spika, hebu niseme kidogo tu katika sekta ya Umwagiliaji. Mwaka jana tuliambiwa hapa kwamba tumepiga maendeleo katika sekta ya umwagiliaji na maendeleo yenyewe ni kwamba tumetoka katika mita 500 tumekwenda katika mita 800, mwaka huu tunaambiwa tena vile vile tumetoka katika mita 500 tumekwenda katika mita 800.

Ningemuomba Waziri *figure* hizi nyengine akazibakisha kwenye kompyuta asingezileta hapa kwa sababu naona kama ni kichekesho, kwamba Serikali inakuja hapa inatwambia kilimo cha umwagiliaji wamepiga hatua kwa kuwezesha miundombinu kutoka mita 300 kwenda 500 yaani *difference* ni mita 300 viwanja viwili vya mpira Mhe. Spika, mpaka lini hali hii?

Tatizo kubwa Mhe. Spika, mimi nafikiria tumeshindwa kudhibiti hayo mapato ambayo tunakusudia kuyakusanya, kila leo tukija hapa tunaambiwa kwamba ZRB wamekusanya wamepita lengo, sijui serikali imefanya utafiti au Waziri wamepita lengo hasa katika sekta gani haya mapato yao yameongezeka vipi, tunaambiwa tu TRA wameongeza pato, wameongeza vipi, kwa sababu wafanyabiashara wanajitahidi kuleta mizigo kwa sababu ndio sekta pekee nchi hii ya ajira sasa vipi pato hili limeongezeka, kuna wakati wao nafikiri wanafurahi kuona hivyo; kwamba pato limeongezeka, lakini je huu ni ukweli kwamba kuongezeka huku ndiko halisi.

Mimi nafikiri au labda Waziri angetwambia kuna mwaka au kuna wakati ambao wanafika na wanafanya utafiti wa kuona bidhaa zilizoingia zinalipiwa kodi halali, leo wafanyabiashara wetu wengi hapa wanaingiza magari, lakini je kweli kodi zinazolipiwa ndizo za uhalali au kuna tofauti katika kodi zinazoingizwa? Kuna mwaka au kuna wakati ambao wanafanya hivyo ili na sisi turidhike kwamba kweli haya mapato yaliyoongezeka yameongezeka na kwa sababu gani. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa akanisaidia wana utaratibu wa kufanya hivyo kwa kwenda katika vyanzo vile vya mapato na wakaangalia kweli hizi ni za uhakika au wanawaachia watu wafanye wanavyotaka.

Mhe. Spika, katika kuongeza mapato tumeelezwa kwamba wananchi ndio watakaobeba jukumu hili kwa sababu marekebisha yote hayo yatatokana na kodi ambazo wao moja kwa moja wataathirika.

Pendekezo jengine Mhe. Spika, niko katika vyanzo vyetu vyengine ambavyo ni taasisi za Serikali. Kiujumla nahisi Serikali ingeangalia tena mwaka huu wameshatia nia kwamba wanataka kuongeza gawio la taasisi za Serikali kama vile benki kutoka asilimia 10 kwenda asilimia 20. Mimi nafikiri umeshafika wakati sasa kama kuna faida inayopatikana basi asilimia 20 ikaongezeka, kwa maana kwamba tukiongeza hili gawio litakalotoka katika taasisi zetu basi kutampa nafuu mwananchi, hizi kodi za ongezeko la mafuta au leseni za udereva basi tukazipunguza kwa sababu moja kwa moja zinamuathiri mwananchi, kuna mashirika ya bandari gawio lake pia lingetizamwa upya likaongeza pato letu la taifa na sio kila siku kushadidia pale pale tu.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni kwamba sisi pia ninavyofahamu kwamba kuna gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania, na kwa mara hii sijaona kitabu chetu je mwaka jana tulipata gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania, na sijui mwaka huu tumeliweka katika mapato ambayo tunatarajia kuyapata kutoka gawio la Benki Kuu au tumebakia tu vile vile hatujui jinsi gani tufanye.

Lakini chanzo chengine cha mapato ni uvuvi wa Bahari Kuu. Sijaona katika kitabu chetu, je mara hii katika uvuvi wa bahari kuu umechangia kiasi gani, lakini haya yote kama yangeidhinishwa katika kitabu hichi tusingempunguzia mwananchi ule mzigo wa ada za bandari na ada nyengine ndogo ndogo zikaondoka.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kusema ni kwamba ninachokijua ni kwamba hivi sasa tunakwenda katika bajeti inayosomwa ni PBB (*Program Based Budget*) yaani bajeti inayotoa matokeo tuone tumefanya nini, sasa ninachokijua ni kwamba sisi kwa hivi sasa nchi hii uchumi wake mkubwa unategemea zaidi sekta ya utalii, je katika kuona kwamba ile sekta ya utalii imetoa tija kuna programu yoyote iliyoanzishwa ambayo itatusaidia sisi kupata mapato zaidi. Nasema hivyo kwa nini, kwa sababu hivi sasa Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Wajumbe wa Baraza kwamba mapato yatokanayo na *visa* hayaonekani au machache ukilinganisha na ujio wa hao ambao tunawatarajia walipe hayo mapato ya *visa*.

Katika ripoti za Serikali zilizotufikia kipindi kilichopita ilikuwa Serikali wana mpango wa kuweka benki katika maeneo ya viwanja vya ndege ili kufanya mapato walipaji wa *visa* waingize malipo yao moja kwa moja kwa njia ya benki, hapa tuliambiwa kwamba serikali wamepeleka ombi; jambo la kushangaza kuomba utawala wa uwanja wa ndege wawapatie eneo la kufanya mambo hayo. Sasa nina wasi wasi kwamba ikiwa sekta hii ndio sekta kiongozi kwa uchumi wetu, hebu programu yake hasa ya uzalishaji ili tufaidike na sekta hii ikoje.

Mhe. Spika, nafikiri kwa hayo machache niombe kwa leo nikae kitako. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna dakika kama 13, kama kuna Mjumbe ambaye anaweza kuzitumia hizo basi tunamkaribisha sana.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia bajeti hii ya Serikali, kwa kweli Mhe. Spika, hali ya kiuchumi imekua asilima 7.4 kwa jumla hali hii inaonekana kuwa imedidimia kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, mategemeo ya wakulima ni kuwa haikufikia kutokana na kukosekana na pembejeo za kilimo na kucheleweshwa pembejeo hizo; mfano wakulima wa mpunga kucheleweshwa kuburugiwa mashamba yao na hatimaye kulima kwa mkono, ambapo wanakosa kupata eneo kubwa ambalo wanalitegemea kwa mahitaji yao.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi zetu mbili zinaendelea na mchakato mzito wa Katiba; mchakato huo zoezi hili lilikuwa katika nyakati mbili tofauti, nyakati ya mwanzo tumemaliza ambapo hatukupata mafanikio yoyote ila ni matusi tu. Mhe. Spika, kwa kuwa nchi zetu ni mbili ambazo zimekwisha zoezi la kwanza jambo ambalo ni muhimu sana kukaa kama sisi Wazanzibari ni vyema tukae tuyazungumze ili wananchi wapate Katiba ambayo wanaitaka na ambayo wanahitajia na kuendesha taifa letu mbele.

Mhe. Spika, kimepita kipindi cha mwanzo ningepita bila ya mafanikio ila matusi tu, kwa kuwa wahenga walisema *ipitayo si ndwele tugange ijayo*; ningewaomba Wazanzibari tukae kama Wazanzibari ili tuyazungumze tusije tukarudia tena wananchi wanatusubiri, nafasi hii hatuipati tena tukiikosa kipindi hiki hatuwezi kupata tena.

Mhe. Spika, hali ya uvuvi wananchi walitegemea katika bajeti hii kupata angalau bajeti ya uvuvi wa Bahari Kuu. Na katika bajeti hii sijaona kipengele chochote ambacho kinahusu bajeti hii ya uvuvi wa bahari kuu, ambayo wananchi wengi vijijini wanategemea kazi hii ya uvuvi wa bahari kuu ndio ajira ya wananchi wetu wa vijijini.

Mhe. Spika, kuhusu miundombinu ya barabara ni mibovu kuanzia mjini hadi vijijini, Sogea *Branch* hadi Tunguu ni njia ambayo ni mbovu tena haifai, nategemea kwamba Mhe. Waziri katika bajeti hii atatenga pesa kwa miundombinu kuitengeneza barabara hiyo. Barabara ya Jambiani ya ndani ndiko kwenye utalii ndio kipaumbele cha kutuletea uchumi katika nchi yetu. Barabara ya ndani ya Jambiani haifai ni mbovu, ningepomba Wizara katika mfuko wake wa barabara ningepomba Serikali itengeneze njia hii naiomba tena, naiomba Mhe. Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa mashirikiano makubwa ya mjadala wa hotuba mbili za hali ya uchumi na mpango wa maendeleo, pamoja na hotuba ya bajeti ya Serikali. Muda uliobaki ni mchache, kwa hivyo wachangiaji waliobaki ambao ni Mheshimiwa Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Omar Ali Shehe watachangia kesho mara baada ya kipindi cha maswali; kwa hivyo niwaombe pamoja na Waheshimiwa wengine tufike mapema ili kuendelea na mjadala huu.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa tuakhrishe kikao chetu hichi hadi kesho tarehe 20/5/ 2014 Saa 3:00 Asubuhi.

(*Saa 1:45 usiku Baraza liliakhrishwa mpaka tarehe 20/5/2014 Saa 3:00 Asubuhi*)

